Biblia Inatufundisha Nini?




JW
.ORG
TM
Omba ufundishwe Biblia bila malipo.
bhs-SW
160113

Biblia Inatufundisha Nini?

KITABU HIKI NI CHA

Photo Credits:
■ Page 25: WHO photo by Edouard Boubat
■ Pages 96-97: Explosion: Based on USAF photo; child: Based on WHO photo by W. Cutting

Kitabu hiki hakiuzwi. Ni sehemu ya kazi ya elimu ya Biblia ya ulimwenguni pote inayotegemezwa kwa michango ya hiari.

Ikiwa ungependa kutoa mchango, tafadhali tembelea tovuti ya www.jw.org/sw.

Isipokuwa imeonyeshwa vingine, Maandiko yote yamenukuliwa kutoka katika *Biblia Takatifu—Tafsiri ya Ulimwengu Mpya.*

What Can the Bible Teach Us?
Chapa ya Juni 2016

Swahili (*bhs*-SW)
© 2015
Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania

WACHAPISHAJI
Printed by Watch Tower Bible and Tract Society of South Africa NPC
1 Robert Broom Drive East, Rangeview, Krugersdorp, 1739, R.S.A.

Made in the Republic of South Africa
Limechapishwa Katika Jamhuri ya Afrika Kusini

YALIYOMO

SURA **UKURASA**

Mungu Alituumba Akiwa na Kusudi Gani? **3**

1. Mungu Ni Nani? **8**
2. Biblia—Kitabu Kutoka kwa Mungu **19**
3. Kusudi la Mungu kwa Wanadamu Ni Nini? **29**
4. Yesu Kristo Ni Nani? **40**
5. Fidia—Zawadi Bora Kutoka kwa Mungu **52**
6. Tukifa Tunaenda Wapi? **62**
7. Kutakuwa na Ufufuo! **71**
8. Ufalme wa Mungu Ni Nini? **83**
9. Je, Mwisho wa Dunia Uko Karibu? **94**
10. Ukweli Kuhusu Malaika **105**
11. Kwa Nini Kuna Mateso Mengi Ulimwenguni? **116**
12. Jinsi Unavyoweza Kuwa Rafiki ya Mungu **124**
13. Heshimu Zawadi ya Uhai **135**
14. Jinsi Familia Yako Inavyoweza Kuwa na Furaha **145**
15. Jinsi ya Kumwabudu Mungu kwa Njia Inayofaa **154**
16. Amua Kumwabudu Mungu **164**
17. Zawadi ya Sala **174**
18. Je, Ninapaswa Kujiweka Wakfu kwa Mungu na Kubatizwa? **185**
19. Kaa Karibu na Yehova **197**

Maelezo ya Ziada **207**

MUNGU ALITUUMBA AKIWA NA KUSUDI GANI?



UNAPOSOMA magazeti, kutazama televisheni, au kusikiliza redio unapata habari nyingi kuhusu uhalifu, vita, na ugaidi. Huenda wewe pia unateseka kwa sababu ya ugonjwa au umefiwa na mpendwa wako.

Hebu jiulize:

- **Je, Mungu alikusudia maisha yangu na ya familia yangu yawe hivi?**
- **Ninaweza kupata wapi msaada wa kukabiliana na matatizo yangu?**
- **Je, inawezekana kuwa na amani duniani?**

Biblia inajibu maswali hayo kwa njia yenye kuridhisha.






BIBLIA INAFUNDISHA KWAMBA MUNGU ATAFANYA MAMBO MAZURI DUNIANI.

Hakutakuwa na maumivu, kuzeeka, au kifo.—Ufunuo 21:4

"Kilema atapanda juu kama vile paa anavyofanya." —Isaya 35:6

"Macho ya vipofu yatafunguliwa." —Isaya 35:5


Wafu watafufuliwa.
—Yohana 5:28, 29
Hakuna
atakayekuwa
mgonjwa.
—Isaya 33:24
Dunia itakuwa
na chakula tele.
—Zaburi 72:16

FAIDIKA NA MAFUNDISHO YA BIBLIA



Usidhani kwamba mambo uliyosoma kwenye kurasa zilizotangulia ni ndoto tu. Mungu ameahidi kutimiza mambo hayo hivi karibuni, na Biblia inaeleza jinsi atakavyofanya.

Biblia inafundisha mambo mengine mengi zaidi ya hayo. Inatueleza mambo ya kufanya ili tuwe na maisha yenye furaha sasa. Hebu fikiria mambo yanayokufanya uwe na wasiwasi. Labda ni kuhusu pesa, matatizo ya familia, afya, au kifo cha mpendwa wako. Biblia inaweza kukusaidia kukabiliana na matatizo hayo, na inaweza kukufariji kwa kujibu maswali yafuatayo:


- **Kwa nini tunateseka?**
- **Tunaweza kukabiliana jinsi gani na matatizo yetu?**
- **Je, inawezekana kuwa na familia yenye furaha?**
- **Inakuwaje mtu akifa?**
- **Je, tutawaona tena wapendwa wetu waliokufa?**
- **Kwa nini tunaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu atatimiza mambo yote aliyoahidi?**

Kusoma kitabu hiki kunaonyesha kwamba unataka kujua yale ambayo Biblia inafundisha. Kitabu hiki kitakusaidia. Chini ya kurasa kuna maswali ambayo yatakusaidia kuielewa vizuri Biblia. Mamilioni ya watu wamefurahia kujifunza Biblia pamoja na Mashahidi wa Yehova. Tunatumaini wewe pia utafurahia. Mungu na akubariki unapojitahidi kujifunza yale ambayo Biblia inafundisha!

IJUE BIBLIA YAKO

BIBLIA ina vitabu 66. Kila kitabu kina sura na mistari ili kurahisisha usomaji. Maandiko yanapotajwa katika kitabu hiki, namba inayofuata jina ni sura ya kitabu au barua katika Biblia, nayo namba inayofuata ni mstari. Kwa mfano, "2 Timotheo 3:16," ni barua ya pili kwa Timotheo, sura ya 3, mstari wa 16.

Ukifungua na kusoma maandiko yaliyo katika kitabu hiki, utazoea kuitumia Biblia. Pia, weka lengo la kusoma Biblia kila siku. Ukisoma sura tatu hadi tano hivi kila siku, unaweza kusoma Biblia nzima kwa mwaka mmoja.



MUNGU NI NANI?

KWA kawaida watoto huuliza maswali mengi sana. Huenda ukawajibu lakini bado wakauliza, 'Kwa nini?' Na kila unapojibu, wanaendelea kuuliza 'Kwa nini?'

2 Iwe ni watu wazima au watoto, sote tunakuwa na maswali. Huenda tukajiuliza kuhusu vitu tunavyohitaji kama vile chakula au mavazi. Au tunaweza kujiuliza maswali muhimu kuhusu wakati wetu ujao. Hata hivyo, huenda tukaacha kuuliza maswali kwa sababu ya kukosa majibu yanayoridhisha.

3 Je, Biblia ina majibu ya maswali muhimu tunayojiuliza? Huenda baadhi ya watu wakahisi kwamba Biblia ina majibu, lakini wanafikiri ni magumu kueleweka. Wanafikiri kwamba maswali hayo yanaweza kujibiwa tu na viongozi na walimu wa dini. Na wengine wanaogopa kuaibishwa. Wewe una maoni gani?

4 Huenda ungependa kujua majibu ya maswali kama vile: Kwa nini nilizaliwa? Nitakapokufa nitaenda wapi? Mungu ana utu gani? Mwalimu mkuu, Yesu, alisema hivi: "Endeleeni kuomba, nanyi mtapewa; endeleeni kutafuta, nanyi mtapata; endeleeni kupiga hodi, nanyi mtafunguliwa." (Mathayo 7:7) Usikate tamaa mpaka utakapopata majibu yenye kuridhisha.

1, 2. Watu hujiuliza maswali gani?

3. Kwa nini watu wengi wanafikiri kwamba hawawezi kupata majibu ya maswali yao muhimu?

4, 5. Ungependa kujua majibu ya maswali gani? Kwa nini unapaswa kuendelea kutafuta majibu?

5 Kwa kweli, ikiwa 'utaendelea kutafuta,' utapata majibu katika Biblia. (Methali 2:1-5) Si vigumu kuelewa majibu hayo. Mambo unayojifunza yatakusaidia uwe na maisha yenye furaha na tumaini zuri la wakati ujao. Hebu tuzungumzie swali moja ambalo linawahangaisha watu wengi.

JE, MUNGU ANATUJALI?

6 Baadhi ya watu wanafikiri kwamba Mungu hawajali. Wanasema kwamba ikiwa kweli Mungu anatujali, ulimwengu ungekuwa tofauti kabisa. Tunashuhudia vita, chuki, na mateso kila mahali. Watu wanaugua, wanateseka, na wanakufa. Baadhi ya watu wanajiuliza, 'Ikiwa Mungu anatujali kwa nini hazuii kuteseka?'

7 Nyakati nyingine baadhi ya viongozi wa dini huwafanya watu wafikiri kwamba Mungu ni katili. Jambo baya linapotokea, wanasema ni mapenzi ya Mungu. Wanasema kwamba Mungu alipanga jambo hilo litokee. Wanaposema hivyo, kwa kweli wanamlaumu Mungu. Hata hivyo, Biblia inafundisha kwamba **Mungu si chanzo cha uovu.** Yakobo 1:13 inasema kwamba Mungu hamjaribu yeyote kwa mambo maovu. Inasema hivi: "Mtu akiwa chini ya jaribu, yeye asiseme: 'Mungu ananijaribu.' Kwa maana Mungu hawezi kujaribiwa na mambo maovu wala yeye mwenyewe hamjaribu yeyote." Hilo linamaanisha kwamba Mungu **hasababishi** mambo mabaya ingawa

---

6. Kwa nini baadhi ya watu wanafikiri kwamba Mungu hajali mateso wanayopata?

7. (a) Baadhi ya viongozi wa dini wamewafundishaje watu kwamba Mungu ni katili? (b) Kwa nini tunaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu si chanzo cha uovu?

anayaacha yatukie. **(Soma Ayubu 34:10-12.)** Fikiria mfano huu.

8 Fikiria kijana anayeishi na wazazi wake. Baba yake anampenda sana na amemfundisha jinsi ya kufanya maamuzi mazuri. Baadaye kijana huyo anamwasi baba yake na kuondoka nyumbani. Anafanya mambo mabaya na kupata matatizo. Je, utamlaumu baba kwa sababu ya matatizo yaliyompata kijana huyo? Bila shaka hapana! (Luka 15:11-13) Kama tu ilivyo kwa baba huyo, Mungu hakuwazuia wanadamu walipoamua kuasi na kuanza kufanya mambo mabaya. Kwa hiyo, jambo fulani baya linapotukia, tunapaswa kukumbuka kwamba si Mungu aliyesababisha. Hatuna haki ya kumlaumu Mungu.

9 Kuna sababu nzuri sana inayomfanya Mungu asichukue hatua kuhusu mambo mabaya. Katika sura ya 11, utajifunza yale ambayo Biblia inasema kuhusu jambo hilo. Hata hivyo, uwe na hakika kwamba Mungu anatupenda na kwamba hatupaswi kumlaumu kwa sababu ya matatizo yanayotupata. Bila shaka, ni Yeye tu anayeweza kuyaondoa.—Isaya 33:2.

10 Mungu ni mtakatifu. (Isaya 6:3) Kila kitu anachofanya ni kizuri, safi na chema. Hivyo tunaweza kumtumaini. Wanadamu ni tofauti. Nyakati nyingine wanakosea. Hata viongozi wanyofu hawawezi kuondoa madhara yanayosababishwa na watu waovu. Hakuna mwanadamu aliye na nguvu kama

---

8, 9. Kwa nini hatupaswi kumlaumu Mungu kwa sababu ya matatizo yanayotupata? Toa mfano.

10. Kwa nini tunaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu ataondoa madhara yote yanayosababishwa na watu waovu?

Mungu. Mungu anaweza na ataondoa madhara yote yanayosababishwa na watu waovu. Ataondoa uovu wote milele.—**Soma Zaburi 37:9-11.**

MUNGU ANAHISIJE WATU WANAPOTESEKA?

11 Mungu anahisije kuhusu matatizo yanayotukia ulimwenguni na yale yanayokupata maishani? Biblia inafundisha kwamba Mungu 'anapenda haki.' (Zaburi 37:28) Anapenda mambo mazuri na kuchukia mambo mabaya. Anahuzunika kuona watu wakiteseka. Biblia inasema, "aliumia moyoni mwake "ulimwengu ulipojaa uovu wakati uliopita. (Mwanzo 6:5, 6) Mungu hajabadilika. (Malaki 3:6) Biblia inasema kwamba Mungu anakujali sana.—**Soma 1 Petro 5:7.**

12 Pia, Biblia inasema kwamba Mungu ametuumba kwa mfano wake. (Mwanzo 1:26) Hii inamaanisha kwamba Mungu ametuumba tukiwa na sifa kama zake. Hivyo, ikiwa unaumia unapoona watu wasio na hatia wanateseka, ni wazi kwamba Mungu anaumia hata zaidi! Tunajuaje?

13 Biblia inatufundisha kwamba "Mungu ni upendo." (1 Yohana 4:8) Kila jambo ambalo Mungu anafanya linachochewa na upendo. Tuna upendo kwa sababu Mungu ni upendo. Fikiria jambo hili: Ikiwa ungekuwa na uwezo, Je, ungeondoa mateso na ukosefu wa haki ulimwenguni? Bila shaka ungeondoa, kwa sababu unawapenda watu. Namna gani Mungu? Kwa kuwa ana uwezo na anatupenda, ataondoa

---

11. Mungu anahisije kuhusu mateso unayopata?

12, 13. (a) Kwa nini tuna sifa ya upendo, na unahisije unapoona watu wakiteseka? (b) Kwa nini tunaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu ataondoa mateso yote na ukosefu wa haki?

mateso yote na ukosefu wa haki. Uwe na uhakika kwamba Mungu atatimiza ahadi zote zilizotajwa mwanzoni mwa kitabu hiki! Lakini ili ufaidike na ahadi hizo, unahitaji kujifunza mengi kumhusu Mungu.

MUNGU ANATAKA UMJUE

14 Unapotaka kuanzisha urafiki na mtu fulani, kwa kawaida jambo la kwanza ni kumwambia jina lako. Je, Mungu ana jina? Dini nyingi zinafundisha kwamba jina lake ni Mungu au Bwana. Hata hivyo, hayo si majina yake binafsi, bali ni majina ya cheo kama vile "mfalme" au "rais." Mungu anatuambia kwamba jina lake ni Yehova. Zaburi 83:18 inasema: "Ili watu wajue kwamba wewe, ambaye jina lako ni Yehova, Wewe peke yako ndiye Uliye Juu Zaidi, juu ya dunia yote." Waandikaji wa Biblia walitumia jina la Mungu zaidi ya mara elfu saba. Yehova anataka ulijue jina lake na kulitumia. Anakwambia jina lake ili uwe rafiki yake.

Ukitaka kuwa rafiki ya mtu fulani, utamwambia jina lako. Mungu anatuambia jina lake kupitia Biblia



15 Jina la Mungu, Yehova, lina maana kubwa sana. Linamaanisha kwamba Mungu anaweza kutimiza ahadi

14. Mungu anaitwa nani, na kwa nini ni muhimu kulijua jina lake?
15. Jina Yehova linamaanisha nini?



Biblia inafundisha kwamba Yehova ni Muumba mwenye upendo wa ulimwengu mzima

zake zote na kusudi lake. Hakuna anayeweza kumzuia. Ni Yehova tu anayestahili kuitwa jina hilo.*


16 Kama tulivyosoma awali, Zaburi 83:18 inasema hivi kumhusu Yehova: "Wewe **peke yako** ndiye Uliye Juu Zaidi." Pia Ufunuo 15:3 inasema: "Matendo yako ni makuu na ya ajabu, Yehova Mungu, Mweza-Yote.

* Ikiwa Biblia yako haina jina Yehova, au ikiwa ungependa kupata habari zaidi kuhusu maana na jinsi ya kutamka jina la Mungu, tafadhali soma Maelezo ya Ziada 1.

16, 17. Ni nini maana ya majina (a) "Mweza-yote"? (b) "Mfalme wa umilele"? (c) "Muumba"?

Njia zako ni za uadilifu na za kweli, Mfalme wa umilele.” Jina la cheo “Mweza-Yote” linamaanisha nini? Linamaanisha kwamba Yehova ana nguvu kuliko yeyote katika ulimwengu. Nalo jina “Mfalme wa umilele” linamaanisha kwamba hana mwanzo wala mwisho. Zaburi 90:2 inaeleza kwamba yeye ni wa tangu milele na milele. Jambo hilo linastaajabisha kwelikweli!

17 Yehova pekee ndiye Muumba. Andiko la Ufunuo 4:11 husema: “Unastahili, Ee Yehova, naam, Mungu wetu, kupokea utukufu na heshima na nguvu, kwa sababu uliumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako navyo vikaumbwa.” Naam, Yehova ameumba malaika mbinguni, nyota angani, matunda kwenye miti, samaki baharini na kila kitu tunachoweza kufikiria!



Baba huwapenda watoto wake, lakini Baba yetu wa mbinguni anatupenda zaidi

JE, UNAWEZA KUWA RAFIKI YA YEHOVA?

18 Baadhi ya watu wanaposoma kuhusu sifa za Yehova, wanaogopa na kufikiri hivi, 'Kwa kuwa Mungu ni mwenye nguvu, cheo cha juu, na yuko mbali sana, je, ananijali?' Hata hivyo, je, Mungu anataka tuhisi hivyo? Hapana. Yehova anataka kutukaribia. Biblia inasema kwamba Mungu "hayuko mbali sana na kila mmoja wetu." (Matendo 17:27) Mungu anataka umkaribie na anaahidi kwamba 'atakukaribia.'—Yakobo 4:8.

19 Unawezaje kuwa rafiki ya Mungu? Yesu alisema: "Uzima wa milele ndio huu, waendelee kupata ujuzi juu yako wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na juu ya yule uliyemtuma, Yesu Kristo." (Yohana 17:3) Ukiendelea kujifunza, utamjua Yehova na Yesu. Hatimaye, unaweza kupata uzima wa milele. Kwa mfano, tayari tumejifunza kwamba "Mungu ni upendo." (1 Yohana 4:16) Hata hivyo, ana sifa nyingine nzuri. Biblia inatufundisha kwamba Yehova ni "mwenye rehema na neema, si mwepesi wa hasira naye ni mwingi wa fadhili zenye upendo na kweli." (Kutoka 34:6) Yehova ni 'mwema na yuko tayari kusamehe.' (Zaburi 86:5) Mungu ni mwenye subira na mshikamanifu. (2 Petro 3:9; Ufunuo 15:4) Utajua mambo mengi kuhusu sifa hizo nzuri kadiri unavyoendelea kujifunza kumhusu katika Biblia.

20 Unaweza kumkaribia Mungu jinsi gani ingawa

---

18. Kwa nini baadhi ya watu wanafikiri kwamba Mungu hawawezi kuwa rafiki yao? Biblia inasema nini kuhusu jambo hilo?
19. (a) Unawezaje kuwa rafiki ya Mungu? (b) Ni sifa gani za Mungu unazopenda zaidi?
20-22. (a) Unaweza kumkaribia Mungu jinsi gani ingawa humwoni? (b) Unapaswa kufanya nini ikiwa wengine wanakuzuia kujifunza Biblia?

humwoni? (Yohana 1:18; 4:24; 1 Timotheo 1:17) Unaposoma kumhusu Yehova katika Biblia, utajua kwamba yeye ni Mtu halisi. (Zaburi 27:4; Waroma 1:20) Kadiri unavyojifunza zaidi kumhusu Yehova, utampenda zaidi na utahisi uko karibu naye.

21 Utaelewa kwamba Yehova ni Baba yetu. (Mathayo 6:9) Alitupatia uhai, na pia anataka tuwe na maisha bora kabisa. Hivyo ndivyo baba yeyote mwenye upendo angetaka watoto wake wawe. (Zaburi 36:9) Naam, Biblia inafundisha kwamba unaweza kuwa rafiki ya Yehova. (Yakobo 2:23) Wazia jambo hilo. Yehova, Muumba wa ulimwengu mzima anataka wewe uwe rafiki yake!

22 Huenda baadhi ya watu wakakusihi uache kujifunza Biblia. Labda wanaogopa kwamba utabadili dini yako. Hata hivyo, usimruhusu mtu yeyote akuzuie kuwa rafiki ya Yehova. Yeye ni rafiki bora kuliko mtu mwingine yeyote.

23 Unapoendelea kujifunza Biblia, huenda usielewe mambo yote. Usione aibu kuuliza maswali au kuomba msaada. Yesu alisema kwamba tunapaswa kuwa wanyenyekevu, kama watoto wachanga. (Mathayo 18:2-4) Watoto wanauliza maswali mengi. Mungu anataka upate majibu. Hivyo, jifunze Biblia kwa makini ili kuhakikisha yale unayojifunza ni kweli.—**Soma Matendo 17:11.**

24 Njia bora ya kumjua Yehova ni kujifunza Biblia. Katika sura inayofuata, tutaona tofauti iliyopo kati ya Biblia na vitabu vingine.

23, 24. (a) Kwa nini unapaswa kuendelea kuuliza maswali? (b) Tutazungumzia nini katika sura inayofuata?

UKWELI WA 1 MUNGU NI NANI?

"Uliumba vitu vyote."—Ufunuo 4:11

Biblia inatufundisha nini kumhusu Mungu?

Ufunuo 15:3
Yeye ndiye Mweza-Yote, na mwenye mamlaka kuliko yeyote katika ulimwengu wote mzima.

Zaburi 90:2
Hana mwanzo wala mwisho.

Mathayo 6:9
Mungu ni Baba yetu. Anataka tuwe na maisha bora.

Matendo 17:27
Mungu anataka tumkaribie.

UKWELI WA 2 MUNGU ANA JINA

"Yehova . . . ndilo jina langu mpaka wakati usio na kipimo."—Kutoka 3:15

Kwa nini ni muhimu kulitumia jina la Mungu?

Zaburi 83:18
Mungu anatuambia kwamba jina lake ni Yehova. majina "Mungu" na"Bwana" hayo si majina yake binafsi. Ni majina ya cheo kama vile "mfalme" na "rais." Yehova anataka ulitumie jina lake.

Kutoka 3:14
Jina lake humaanisha "Yeye Husababisha Kuwa." Kwa kuwa Yehova aliumba vitu vyote, anaweza kutimiza ahadi yoyote anayoitoa na kutimiza kusudi lake.

UKWELI WA 3 YEHOVA ANATUPENDA

"Mungu ni upendo."—1 Yohana 4:8

Upendo wa Mungu unamaanisha nini kwetu?

Kutoka 34:6; Zaburi 37:28
Yeye ni mwenye rehema na huruma. Anapenda kweli na haki.

Zaburi 86:5
Ni mwenye kusamehe.

2 Petro 3:9
Ni mwenye subira kwetu.

Ufunuo 15:4
Ni mshikamanifu kwetu.

UKWELI WA 4 MUNGU ANAKUJALI

'Mtupieni mahangaiko yenu yote, kwa sababu yeye anawajali ninyi.'—1 Petro 5:7

Unajua jinsi gani kwamba Mungu anakujali?

Zaburi 37:9-11
Ameahidi kukomesha mateso na kuondoa madhara yote yanayosababishwa na watu wabaya.

Yakobo 4:8
Yehova anataka umkaribie.

Yohana 17:3
Kadiri unavyoendelea kujifunza mengi zaidi kumhusu Mungu ndivyo utakavyozidi kumpenda zaidi.

BIBLIA —KITABU KUTOKA KWA MUNGU

WEWE huhisije unapopewa zawadi na rafiki yako mpendwa? Unatazamia kwa hamu kuifungua na unafurahi sana kwa sababu rafiki yako anakupenda. Unamshukuru.

2 Biblia ni zawadi kutoka kwa Mungu, kwa sababu inatueleza habari ambazo hatuwezi kuzipata mahali pengine popote. Kwa mfano, hutueleza kwamba Mungu aliumba mbingu, dunia, na mwanaume na mwanamke wa kwanza. Ina kanuni zinazoweza kutusaidia kukabiliana na matatizo. Katika Biblia, tunajifunza jinsi Mungu atakavyotimiza kusudi lake la kuifanya dunia kuwa mahali bora pa kuishi. Biblia ni zawadi bora sana.

3 Unapoendelea kujifunza Biblia, utaelewa kwamba Mungu anataka uwe rafiki yake. Kadiri unavyojifunza zaidi kumhusu, uhusiano wako pamoja naye utaimarika.

4 Mabilioni ya nakala za Biblia yametafsiriwa na kuchapishwa katika lugha 2,600 hivi. Zaidi ya asilimia 90 ya watu ulimwenguni wanaweza kujisomea Biblia katika lugha zao. Kwa kuongezea, zaidi ya watu milioni moja hupata Biblia **kila**

1, 2. Kwa nini Biblia ni zawadi nzuri kutoka kwa Mungu?
3. Unapoendelea kujifunza Biblia utaelewa jambo gani?
4. Ni nini kinachokuvutia kuhusu kutafsiriwa kwa Biblia?



Biblia Takatifu—Tafsiri ya Ulimwengu Mpya
inapatikana katika lugha mbalimbali

kila juma! Kwa kweli, hakuna kitabu kingine kama Biblia.

5 Biblia ‘imeongozwa na roho ya Mungu.’ **(Soma 2 Timotheo 3:16.)** Hata hivyo, huenda wengine wakafikiri hivi: ‘Kwa kuwa Biblia iliandikwa na wanadamu inawezaje kuwa kitabu kutoka kwa Mungu?’ Biblia inajibu: “Wanadamu walisema yaliyotoka kwa Mungu kama walivyoongozwa na roho takatifu.” (2 Petro 1:21) Ni kama vile tu babu akimwomba mjukuu wake amwandikie barua. Barua hiyo ni ya nani? Hiyo ni barua ya babu wala si ya mjukuu. Vivyo hivyo, Mtungaji wa Biblia ni Mungu, wala si wanadamu

5. Kwa nini tunaweza kusema kwamba Biblia ‘imeongozwa na roho ya Mungu’?

aliowatumia kuiandika. Mungu aliwaongoza kuandika mawazo yake. Kwa kweli, Biblia ni "neno la Mungu." —1 Wathesalonike 2:13; soma Maelezo ya Ziada 2.

BIBLIA NI SAHIHI

6 Biblia iliandikwa kwa zaidi ya miaka 1,600. Waandikaji wake waliishi nyakati tofauti-tofauti. Wengine walikuwa na elimu ya juu ilhali wengine walikuwa na elimu ya kawaida. Kwa mfano, mwandikaji mmoja alikuwa daktari. Wengine walikuwa wakulima, wavuvi, wachungaji, manabii, waamuzi, na wafalme. Ingawa waandikaji walikuwa tofauti, Biblia yote inapatana. Ujumbe wake haupingani.*

7 Kitabu cha kwanza cha Biblia kinaeleza jinsi matatizo yalivyoanza, na kitabu cha mwisho kinaeleza jinsi ambavyo Mungu atayaondoa na kuifanya dunia kuwa paradiso. Biblia inaeleza historia ya mwanadamu ya tangu zamani na inaonyesha kwamba sikuzote makusudi ya Mungu hutimia.

8 Biblia si kitabu cha sayansi, hata hivyo, inazungumzia mambo ya sayansi kwa usahihi. Kitabu kutoka kwa Mungu kinapaswa kuwa hivyo. Kwa mfano, kitabu cha Mambo ya Walawi kina maagizo ambayo Mungu aliwapa Waisraeli ili kuzuia kuenea kwa magonjwa. Mambo hayo yaliandikwa miaka mingi kabla

* Watu fulani husema kwamba ujumbe wa Biblia unatofautiana, hata hivyo madai hayo si ya kweli. Ona sura ya 7 ya kitabu *Biblia —Neno la Mungu au la Binadamu?* kilichochapishwa na Mashahidi wa Yehova.

6, 7. Kwa nini tunasema kwamba Biblia inapatana?
8. Toa mifano inayoonyesha kwamba Biblia ni sahihi inapozungumzia mambo ya sayansi.

ya wanasayansi kugundua jinsi bakteria na virusi wanavyoeneza magonjwa. Pia, Biblia inaeleza kwa usahihi kwamba dunia imetundikwa pasipo na kitu. (Ayubu 26:7) Hata wakati ambapo watu wengi waliamini kwamba dunia ni tambarare, Biblia ilisema kwamba dunia ni mviringo.—Isaya 40:22.

9 Biblia ni sahihi inapozungumzia historia. Hata hivyo, vitabu vingi vya historia si sahihi kabisa kwa sababu waandikaji wake hawakuwa wanyofu. Kwa mfano, nyakati nyingine hawakuandika mataifa yao yaliposhindwa vitani. Tofauti na hao, waandikaji wa Biblia walikuwa wanyofu na waliandika hata taifa lao la Israeli liliposhindwa vitani. Waliandika pia kuhusu makosa yao. Kwa mfano, katika kitabu cha Hesabu, Musa aliandika kosa zito alilofanya na hivyo akaadhibiwa na Mungu. (Hesabu 20:2-12) Unyofu wa waandikaji wa Biblia unathibitisha kwamba ni kitabu kutoka kwa Mungu. Hivyo tunaweza kuiamini Biblia.

KITABU CHENYE USHAURI MZURI

10 Biblia 'imeongozwa na roho ya Mungu nayo ni yenye faida kwa kufundisha, kwa kukaripia, kwa kunyoosha mambo, kwa kutia nidhamu katika uadilifu.' (2 Timotheo 3:16) Naam, ushauri wake una faida kwetu pia. Yehova ndiye aliyetuumba, kwa hiyo anaelewa jinsi tunavyohisi na kufikiri. Anatujua vizuri zaidi kuliko tunavyojijua, na anataka tuwe na furaha. Anajua mambo yanayotufaa na yasiyotufaa.

---

9. Tunajifunza nini kutokana na unyofu wa waandikaji wa Biblia?
10. Kwa nini ushauri wa Biblia ni wenye faida kwetu?

11 Katika Mathayo sura ya 5 hadi ya 7, Yesu alitoa ushauri mzuri kuhusu jinsi ya kuwa na furaha, kusuluhisha matatizo, kusali, na mtazamo kuelekea mali. Ingawa alitoa ushauri huo miaka 2,000 iliyopita, bado ni wenye nguvu na unatufaidi leo pia.

12 Pia, katika Biblia Yehova anatufundisha kanuni ambazo zinaweza kutusaidia kuwa na familia yenye furaha, wafanyakazi bora, na kuishi kwa amani pamoja na wengine. Sikuzote kanuni za Biblia ni zenye faida, kwa watu wa namna na hali zote.**—Soma Isaya 48:17;** soma Maelezo ya Ziada 3.

KWA NINI UAMINI UNABII WA BIBLIA?

13 Unabii mwingi wa Biblia umetimizwa. Kwa mfano, Isaya alitabiri kwamba jiji la Babiloni lingeharibiwa. (Isaya 13:19) Alieleza waziwazi **jinsi** ambavyo jiji hilo lingeharibiwa. Jiji hilo lilikuwa na kuta, malango na lilizungukwa na mto mkubwa. Hata hivyo, Isaya alitabiri kwamba mto huo ungekaushwa na malango yangeachwa wazi. Majeshi yangeingia jijini bila kupigana. Isaya hata alitabiri kuhusu mfalme ambaye angeharibu jiji la Babiloni, yaani, Koreshi.**—Soma Isaya 44:27–45:2;** soma Maelezo ya Ziada 4.


14 Miaka mia mbili baada ya unabii huo kutolewa, jeshi lilifika likiwa tayari kushambulia jiji la Babiloni. Ni nani aliyekuwa kiongozi wa jeshi hilo? Kama ilivyotabiriwa, Koreshi, mfalme wa

---

11, 12. (a) Yesu alitoa ushauri gani mzuri katika Mathayo sura ya 5 hadi ya 7? (b)Ni mambo gani mengine tunayoweza kujifunza katika Biblia?

13. Nabii Isaya alitabiri nini kuhusu jiji la Babiloni?

14, 15. Unabii wa Isaya ulitimizwa jinsi gani?



Mwandikaji wa Biblia Isaya alitabiri kuhusu kuharibiwa kwa jiji la Babiloni

Uajemi. Utimizo wa sehemu ya mwisho ya unabii huo ulikuwa umewadia.

15 Wababiloni walishambuliwa siku ambayo walikuwa na sherehe. Walidhani walikuwa salama kwa sababu jiji lilizungukwa na mto mkubwa na lilikuwa na kuta kubwa. Nje ya jiji, Koreshi na jeshi lake waligeuza mkondo wa mto ili kupunguza kina chake. Maji ya-

lipungua na jeshi la Uajemi likavuka. Hata hivyo, jeshi la Koreshi lingeingiaje jiji la Babiloni lenye kuta kubwa? Kama ilivyotabiriwa, malango ya jiji yalikuwa wazi, hivyo, jeshi liliingia bila kupigana.

16 Isaya alitabiri kwamba jiji la Babiloni halingekaliwa tena. Aliandika: "Hatakaliwa kamwe, wala hatakuwa na makao kwa kizazi baada ya kizazi." (Isaya 13:20) Je, unabii huo ulitimia? Ni Magofu tu yaliyobaki katika eneo ambalo Babiloni lilikuwa, kilomita 80 hivi kusini mwa Baghdad, nchini Iraq. Hakuna wakaaji wowote katika eneo hilo hadi leo. Yehova alilliharibu jiji la Babiloni "kwa ufagio wa maangamizi."—Isaya 14:22, 23.*

17 Kwa kuwa unabii mwingi wa Biblia umetimia,

* Ikiwa ungependa kujifunza mengi zaidi kuhusu unabii wa Biblia, unaweza kusoma broshua *Kitabu kwa Ajili ya Watu Wote,* ukurasa wa 27 hadi 29, iliyochapishwa na Mashahidi wa Yehova.

16. (a) Isaya alitabiri nini kuhusu jiji la Babiloni? (b) Tunajua jinsi gani kwamba unabii wa Isaya ulitimia?
17. Kwa nini tunaweza kuamini ahadi zote za Mungu?

Magofu ya Babiloni



tunaamini yale ambayo Biblia inasema kuhusu wakati ujao. Tunaweza kuwa na uhakika kwamba Yehova atatimiza ahadi ya kuifanya dunia kuwa paradiso. **(Soma Hesabu 23:19.)** Naam, tuna tumaini la "uzima wa milele ambao Mungu, asiyeweza kusema uwongo, aliahidi nyakati za zamani za kale."—Tito 1:2.*

BIBLIA INAWEZA KUBADILISHA MAISHA YAKO

18 Tumejifunza kwamba Biblia ni tofauti na vitabu vingine. Biblia ina upatano, na ni sahihi kisayansi na kihistoria. Pia, hutupatia ushauri mzuri na ina unabii mwingi ambao umetimia. Hata hivyo, Biblia ina faida kubwa zaidi. Mtume Paulo aliandika hivi: "Neno la Mungu liko hai nalo lina nguvu." Andiko hilo linamaanisha nini?**—Soma Waebrania 4:12.**

19 Biblia inaweza kubadilisha maisha yako. Inaweza kukusaidia kujichunguza. Inaweza kukusaidia kujua hisia na mawazo yako. Kwa mfano, huenda tukafikiri kwamba tunampenda Mungu. Hata hivyo, ili kuthibitisha kwamba tunampenda, tunahitaji kutumia yale tunayojifunza katika Biblia.

20 Kwa kweli, Biblia ni kitabu kutoka kwa Mungu. Anataka uisome, ujifunze na uipende. Thamini zawadi hiyo na uendelee kujifunza. Hatimaye utaelewa kusudi la Mungu kwa wanadamu. Katika sura inayofuata tutajifunza kuhusu kusudi hilo.

---

* Kuharibiwa kwa Babiloni ni mfano mmoja tu wa unabii wa Biblia ambao ulitimizwa. Unaweza kupata habari zaidi za unabii unaomhusu Yesu Kristo katika Maelezo ya Ziada 5.

---

18. Paulo alisema nini kuhusu "neno la Mungu"?

19, 20. (a) Biblia inawezaje kukusaidia kujichunguza? (b) Unawezaje kuonyesha kwamba unathamini Biblia ikiwa zawadi?

UKWELI WA 1 BIBLIA KITABU KUTOKA KWA MUNGU

"Andiko lote limeongozwa na roho ya Mungu."
—2 Timotheo 3:16

Biblia inatofautiana jinsi gani na vitabu vingine?

Biblia imetafsiriwa katika lugha zipatazo 2,600 hivi, na mabilioni ya nakala yamechapishwa.

Inatueleza habari ambazo hatuwezi kuzipata mahali pengine.

1 Wathesalonike 2:13
Mungu ndiye mtungaji wa Biblia.

2 Petro 1:21
Mungu aliwaongoza wanadamu kuandika mawazo yake.

UKWELI WA 2 BIBLIA NI KITABU CHA UNABII

'Mungu hasemi uwongo.'—Tito 1:2

Kwa nini uamini Biblia?

Isaya 44:27—45:2
Biblia ilitabiri uharibifu wa Babiloni miaka mingi kabla ya jiji hilo kuharibiwa.

2 Timotheo 3:1-5
Unabii wa Biblia unatimizwa sasa.

Hesabu 23:19
Tunaamini yale ambayo Biblia inasema kuhusu wakati ujao yatatimia.

UKWELI WA 3 BIBLIA IMEKUSUDIWA KUKUSAIDIA

"Mimi, Yehova, ni Mungu wako, Yeye anayekufundisha ili ujifaidi mwenyewe."—Isaya 48:17

Umejifunza nini kuhusu Biblia?

Ayubu 26:7; Isaya 40:22
Biblia ni sahihi kisayansi.

Hesabu 20:2-12
Waandishi wa Biblia walikuwa wanyofu.

Mathayo 5-7
Yesu alitushauri jinsi ya kuwa na furaha, kuwatendea wengine, kusali, na kuwa na mtazamo unaofaa kuhusu pesa.

UKWELI WA 4 BIBLIA INAWEZA KUBADILI MAISHA YAKO

"Neno la Mungu liko hai nalo lina nguvu."
—Waebrania 4:12

Neno la Mungu linaweza kukusaidia jinsi gani?

- Linaweza kukusaidia kuelewa kusudi la Mungu.
- Linaweza kukusaidia kujichunguza utu wako.
- Linaweza kukusaidia kuelewa yale ambayo Mungu anataka ufanye.

Mungu anataka usome, ujifunze na kuipenda Biblia.

KUSUDI LA MUNGU KWA WANADAMU NI NINI?

MUNGU ana kusudi zuri ajabu kwa wanadamu. Aliwaumba Adamu na Hawa, mwanamume na mwanamke wa kwanza ili waishi katika bustani maridadi. Alikusudia wazae watoto, waifanye dunia yote kuwa paradiso, na kuwatawala wanyama.—Mwanzo 1:28; 2:8, 9, 15; soma Maelezo ya Ziada 6.

2 Je, unafikiri ni kweli kwamba tutaishi katika dunia paradiso? Yehova anatuambia: "Mimi nimesema hilo; pia nitalitimiza." (Isaya 46:9-11; 55:11) Naam, atatenda kama alivyokusudia, hakuna kitu kinachoweza kumzuia. Yehova anasema kwamba aliiumba dunia akiwa na kusudi. "Hakuiumba tu bila sababu." (Isaya 45:18) Anataka watu waishi duniani pote. Mungu anataka watu gani waishi duniani, na kwa muda gani? Biblia inasema: "**Waadilifu** [au, watiifu] wenyewe wataimiliki dunia, nao **watakaa milele** juu yake."—Zaburi 37:29; Ufunuo 21:3, 4.

3 Leo watu huugua na kufa. Katika sehemu nyingi, watu hupigana na kuuana. Kwa kweli, hilo halikuwa kusudi la Mungu. Basi, ni nini kilitukia, na kwa nini? Biblia pekee inaweza kutupatia majibu.

---

1. Mungu aliwaumba wanadamu kwa kusudi gani?
2. (a) Tunajuaje kwamba Yehova atatenda kama alivyokusudia? (b) Biblia inasema nini kuhusu kuishi milele?
3. Kwa kuwa wanadamu wanaugua na kufa, huenda ukauliza swali gani?

ADUI YA MUNGU

4 Biblia inatuambia kwamba Mungu ana adui "anayeitwa Ibilisi na Shetani." Shetani alitumia nyoka kuzungumza na Hawa katika bustani ya Edeni. (Ufunuo 12:9; Mwanzo 3:1) Alifanya ionekane kana kwamba nyoka ndiye anayezungumza.—Soma Maelezo ya Ziada 7.

5 Je, Mungu alimuumba Shetani Ibilisi? Hapana! Yeye alikuwako mbinguni akiwa **Malaika** Mungu alipoumba dunia kwa ajili ya Adamu na Hawa, **alibadilika na kuwa Ibilisi.** (Ayubu 38:4, 7) Hilo liliwezekanaje? Fikiria jambo hili: Mtu mwema anaweza kubadilika jinsi gani na kuwa mwizi? Hakuna mtu anayezaliwa akiwa mwizi. Lakini huenda akatamani au kutaka kitu kisicho chake. **Anapoendelea kukifikiria,** ndivyo tamaa yake mbaya inavyozidi kukua. Mwishowe anapopata fursa, anaiba. Amebadilika mwenyewe na kuwa mwizi. **—Soma Yakobo 1:13-15;** soma Maelezo ya Ziada 8

6 Malaika huyo [Shetani] alifanya hivyo. Yehova alipowaumba Adamu na Hawa, aliwaambia wazae watoto na 'waijaze dunia.' (Mwanzo 1:27, 28) Huenda malaika huyo aliwaza hivi, 'Watu hawa wanapaswa kuniabudu mimi badala ya Yehova!' Tamaa yake ilizidi kuongezeka alipoendelea kufikiria jambo hilo. Malaika huyo alitaka watu wamwabudu yeye badala ya kumwabudu Yehova. Mwishowe alimdanganya na kumpotosha Hawa. **(Soma Mwanzo 3:1-5.)** Kwa kufanya hivyo, akawa Shetani Ibilisi, yaani, adui ya Mungu.

4, 5. (a) Ni nani aliyemtumia nyoka kuzungumza na Hawa katika bustani ya Edeni? (b) Mtu mwema anaweza kubadilika jinsi gani na kuwa mwizi?

6. Malaika alibadilika jinsi gani na kuwa adui ya Mungu?

7 Adamu na Hawa walikataa kumtii Mungu kwa kula tunda walilokatazwa. (Mwanzo 2:17; 3:6) Kwa kuwa walitenda dhambi dhidi ya Yehova, hatimaye walikufa, kama tu Yehova alivyokuwa amesema. (Mwanzo 3:17-19) Kwa sababu hiyo, watoto wa Adamu na Hawa wakarithi dhambi, kwa hiyo wao pia wakafa. **(Soma Waroma 5:12.)** Ili kuelewa ni jinsi gani wazao wa Adamu na Hawa walirithi dhambi, fikiria mfano huu. Tuseme unaoka mkate kwenye chombo kilichobonyea. Mkate huo utabonyea kama chombo hicho. Adamu alitenda dhambi alipokosa kumtii Mungu. Kwa kuwa sisi ni wazao wa Adamu, tumerithi "kasoro" ileile ya dhambi. Na kwa sababu ya dhambi, tunazeeka na kufa.—Waroma 3:23.

8 Shetani aliasi dhidi ya Yehova alipowashawishi Adamu na Hawa wakatae kumtii Mungu. Alitaka Adamu na Hawa waamini kwamba Yehova ni mwongo na mtawala mbaya asiyetaka wafurahie maisha. Shetani alidai kwamba wanadamu hawahitaji kuongozwa na Mungu na kwamba Adamu na Hawa walipaswa kujiamulia wenyewe mambo yanayofaa na yasiyofaa. Yehova angetendaje? Angeweza kuwaua waasi hao na kuukomesha uasi. Hata hivyo, je, unafikiri jambo hilo lingethibitisha kwamba Shetani ni mwongo? Hapana.


9 Kwa hiyo, Yehova hakuwaangamiza waasi hao punde tu baada ya kuasi. Aliruhusu muda upite ili wanadamu wajitawale wenyewe. Kufanya hivyo kungethibitisha kwamba Shetani ni mwongo na kwamba Yehova

---

7. (a) Kwa nini Adamu na Hawa walikufa? (b) Kwa nini tunazeeka na kufa?

8, 9. (a) Shetani alitaka Adamu na Hawa waamini nini? (b) Kwa nini Yehova hakuwaangamiza waasi hao mara moja?

ndiye anayejua mambo yanayowafaa wanadamu. Tutajifunza mengi kuhusu hilo katika Sura ya 11. Hata hivyo, unaonaje uamuzi ambao Adamu na Hawa walifanya? Je walikuwa na sababu ya kutomtii Mungu na kumwamini Shetani? Yehova ndiye aliyewapa kila kitu walichohitaji. Aliwapa uhai mkamilifu, makao mazuri ya kupendeza, na kazi waliyofurahia. Lakini Shetani hakuwapa chochote. Ikiwa ungekuwa wewe, ungefanya nini?



Ikiwa falme zote za ulimwengu hazikuwa za Shetani, je angeahidi kumpa Yesu?

10 Leo, sisi sote tuna uhuru wa kuamua kufanya jambo lolote, na maisha yetu yatategemea uamuzi huo. Tunaweza kuamua kumtii Yehova kuwa mtawala wetu na kuthibitisha kwamba Shetani ni mwongo. Au tunaweza kuchagua Shetani awe mtawala wetu. (Zaburi 73:28; **soma Methali 27:11.)** Leo, ni watu wachache ulimwenguni wanaoamua kumtii Mungu. Hilo linathibitisha kwamba Mungu si mtawala wa ulimwengu huu. Basi ikiwa Mungu si mtawala wa ulimwengu huu, ni nani anayeutawala?

NI NANI ANAYEUTAWALA ULIMWENGU?

11 Yesu alimjua mtawala wa ulimwengu. Pindi moja, Shetani 'alimwonyesha falme zote za ulimwengu na utukufu wazo.' Kisha Shetani akamwahidi Yesu: "Nitakupa mambo yote haya ukianguka chini na kunifanyia tendo la ibada." (Mathayo 4:8, 9; Luka 4: 5, 6) Jiulize, 'Ikiwa falme hizo hazikuwa za Shetani, je angeahidi kumpa Yesu?' Hapana. Serikali zote za ulimwengu ni mali ya Shetani.

12 Huenda ukajiuliza: 'Inawezekanaje Shetani kuwa mtawala wa ulimwengu huu? Je, si Yehova, Mungu Mweza Yote, aliyeumba ulimwengu?' (Ufunuo 4: 11) Bila shaka, Yehova ndiye aliyeumba, lakini Yesu alisema waziwazi kuwa Shetani ndiye "mtawala wa ulimwengu huu." (Yohana 12:31; 14:30; 16:11) Mtume Paulo alimwita Shetani Ibilisi "mungu wa mfumo huu wa mambo." (2 Wakorintho 4:3, 4) Na mtume Yohana

---

10. Sote tuna uhuru wa kufanya uamuzi gani?

11, 12. (a) Ahadi ya Shetani inaonyesha jinsi gani kwamba yeye ndiye mtawala wa ulimwengu? (b) Ni maandiko gani yanayoonyesha kwamba Shetani ndiye mtawala wa ulimwengu?

aliandika kwamba "ulimwengu mzima unakaa katika nguvu za yule mwovu."—1 Yohana 5:19.

ULIMWENGU WA SHETANI UTAHARIBIWA JINSI GANI?

13 Ulimwengu unazidi kuwa hatari hata zaidi. Umejaa vita, ufisadi, unafiki, na jeuri. Hata wanadamu wakijitahidi kadiri gani, hawawezi kuondoa matatizo hayo. Hata hivyo, hivi karibuni Mungu atauharibu ulimwengu huu mwovu katika vita vya Har–Magedoni na kuleta ulimwengu mpya wenye uadilifu.—Ufunuo 16:14-16; soma Maelezo ya Ziada 10.

14 Yehova alimchagua Yesu Kristo kuwa Mfalme wa serikali au Ufalme wake Mbinguni. Miaka mingi iliyopita, Biblia ilitabiri kwamba Yesu angetawala akiwa "Mkuu wa Amani" na serikali yake haingekuwa na mwisho. (Isaya 9:6, 7) Yesu aliwafundisha wafuasi wake wasali kwa ajili ya serikali hiyo aliposema: "Ufalme wako na uje. Mapenzi yako na yatendeke duniani kama ilivyo mbinguni." (Mathayo 6:10) Katika Sura ya 8, tutajifunza jinsi ambavyo Ufalme wa Mungu utaharibu serikali za ulimwengu huu na kuanza kuitawala dunia. **(Soma Danieli 2:44.)** Hatimaye, Ufalme wa Mungu utaifanya dunia kuwa paradiso.—Soma Maelezo ya Ziada 11.

ULIMWENGU MPYA U KARIBU!

15 Biblia inasema hivi: "Kulingana na ahadi yake tunangojea mbingu mpya na dunia mpya," na "humo uadilifu utakaa." (2 Petro 3:13; Isaya 65:17) Nyakati fulani

---

13. Kwa nini tunahitaji ulimwengu mpya?
14. Mungu amemchagua nani awe Mfalme wa Ufalme Wake? Biblia ilitabiri nini kumhusu Yesu?
15. "Dunia mpya" ni nini?

neno "dunia" katika Biblia linamaanisha watu wanaoishi duniani. (Mwanzo 11:1) Kwa hiyo "dunia mpya" yenye uadilifu inamaanisha watu wote wanaomtii Mungu na kupata kibali chake.

16 Yesu aliahidi kwamba wale watakaoishi katika ulimwengu mpya wa Mungu watapewa "uzima wa milele". (Marko 10:30) Tunapaswa kufanya nini ili tupate uzima wa milele? Ili kupata jibu tafadhali **soma Yohana 3:16 na sura ya 17:3.** Acheni tuone Biblia inavyosema kuhusu maisha yatavyokuwa katika dunia paradiso.

17 Uovu, vita, uhalifu, na jeuri havitakuwapo. Watu wote waovu hawatakuwapo. (Zaburi 37:10, 11) Yehova 'atakomesha vita mpaka kwenye mwisho wa dunia.' (Zaburi 46:9; Isaya 2:4) Dunia yote itajaa watu wanaompenda na kumtii Mungu. Kutakuwa na amani milele. —Zaburi 72:7.

18 Watu wa Yehova watakuwa salama. Katika nyakati za Biblia Waisraeli walipomtii Mungu, walikuwa salama kwa sababu aliwalinda. (Mambo ya Walawi 25:18, 19) Katika dunia paradiso hatutaogopa mtu yeyote wala kitu chochote. Tutakuwa salama wakati wote!—**Soma Isaya 32:18; Mika 4:4.**

19 Kutakuwa na chakula kingi. "Kutakuwa na wingi wa nafaka duniani; Juu ya milima kutakuwa na mafuriko." (Zaburi 72:16) Yehova, "Mungu wetu, atatubariki," na "dunia itatoa mazao yake."—Zaburi 67:6.

20 Dunia yote itakuwa paradiso. Watu watakuwa na

---

16. Mungu atawapa zawadi gani nzuri wale watakaoishi katika dunia mpya, nasi tunapaswa kufanya nini?
17, 18. Tunajuaje kwamba kutakuwa na amani na usalama duniani?
19. Kwa nini tuna uhakika kwamba kutakuwa chakula kingi katika dunia mpya ya Mungu?
20. Tunajuaje kwamba dunia itakuwa paradiso?

nyumba na bustani nzuri. **(Soma Isaya 65:21-24; Ufunuo 11:18.)** Dunia yote itakuwa maridadi kama tu bustani ya Edeni ilivyokuwa. Yehova atatutimizia mahitaji yetu yote. Biblia inasema hivi kumhusu: "Unaufumbua mkono wako na kutosheleza tamaa ya kila kitu kilicho hai."—Zaburi 145:16.

21 Kutakuwa na amani kati ya wanyama na wanadamu. Wanyama hawatawadhuru wanadamu tena. Watoto watajihisi salama, hata wakiwa katikati ya wanyama ambao leo ni hatari.—**Soma Isaya 11:6-9; 65:25.**

22 Hakutakuwa na Magonjwa. Yesu aliwaponya watu wengi alipokuwa duniani. (Mathayo 9:35; Marko 1:40-42; Yohana 5:5-9) Akiwa Mfalme wa Ufalme wa Mungu, Yesu atamponya kila mtu. Hakuna mtu atakayesema: "Mimi ni mgonjwa."—Isaya 33:24; 35:5, 6.

23 Wafu watafufuliwa. Mungu anaahidi kwamba atafufua mamilioni ya watu. "Kutakuwa na ufufuo wa waadilifu na wasio waadilifu pia."—**Soma Yohana 5:28, 29;** Matendo 24:15.

24 Sote tuna uhuru wa kuchagua. Tunaweza kuamua kujifunza na kumtumikia Yehova, au kufanya tunachotaka. Tukichagua kumtumikia Yehova tutafurahia mambo mazuri wakati ujao. Mwanamume fulani alimwambia Yesu amkumbuke atakapokufa, naye Yesu akamwahidi hivi: "Utakuwa pamoja nami katika Paradiso." (Luka 23:43) Na tuendelee kujifunza mengi zaidi kumhusu Yesu Kristo na jinsi atakavyotimiza ahadi nzuri sana za Mungu.

---

21. Tunajuaje kwamba kutakuwa na amani kati ya wanadamu na wanyama?
22. Yesu atawafanyia nini wagonjwa?
23. Mungu anaahidi nini kuhusu wafu?
24. Unahisije kuhusu kuishi katika Paradiso?



UKWELI WA 1 MUNGU ALITUUMBA AKIWA NA KUSUDI

"Waadilifu wenyewe wataimiliki dunia, nao watakaa milele juu yake."—Zaburi 37:29

Kusudi la Mungu nini kwa wanadamu?

Mwanzo 1:28
Mungu alitaka familia zifanye duniani kuwa paradiso na kutunza wanyama.

Isaya 46:9-11; 55:11
Mungu atafanya yale aliyokusudia, wala hakuna kitakachomzuia.

UKWELI WA 2 KWA NINI MAISHA NI MAGUMU

"Ulimwengu mzima unakaa katika nguvu za yule mwovu."—1 Yohana 5:19

Ni nani anayeutawala ulimwengu?

Yohana 12:31
Yesu alisema Shetani ni mtawala wa ulimwengu.

Yakobo 1:13-15
Shetani alitamani ibada isiyo yake.

Mwanzo 2:17; 3:1-6
Shetani alimdanganya Hawa, kisha Adamu na Hawa wakamwasi Mungu, hatimaye Adamu na Hawa wakafa.

Waroma 3:23; 5:12
Tunakufa kwa sababu tumerithi dhambi kutoka kwa Adamu.

2 Wakorintho 4:3, 4
Shetani anawapotosha watu.

UKWELI WA 3 UFALME WA MUNGU UTAONDOA MATATIZO

"Ufalme wako na uje. Mapenzi yako na yatendeke duniani."—Mathayo 6:10

Yehova atafanya nini?

Danieli 2:44
Ufalme wa Mungu utachukua mahali pa serikali zote za ulimwengu.

Ufunuo 16:14-16
Mungu atauharibu ulimwengu huu mwovu katika vita vya Har–Magedoni.

Isaya 9:6, 7
Yehova amemchagua Yesu kuwa Mfalme wa serikali Yake ya mbinguni. Yesu ataitawala dunia yote.

UKWELI WA 4 UFALME WA MUNGU UTAIFANYA DUNIA KUWA PARADISO

"Unaufumbua mkono wako na kutosheleza tamaa ya kila kitu kilicho hai."—Zaburi 145:16

Ufalme wa Mungu utatufanyia nini?

Zaburi 46:9
Vita, jeuri, na uhalifu havitakuwapo.

Isaya 32:18; 65:21-24
Katika ulimwengu mpya, watu wote watakuwa na nyumba na bustani maridadi na wataishi kwa amani.

Zaburi 72:16
Kutakuwa na chakula tele.

Isaya 11:6-9
Kutakuwa na amani kati ya wanadamu na wanyama.

Isaya 33:24; Matendo 24:15
Hakuna atakayekuwa mgonjwa, na wafu watafufuliwa.

YESU KRISTO NI NANI?

KUNA watu wengi sana mashuhuri ulimwenguni. Huenda unalijua jina la mtu fulani mashuhuri. Hata hivyo, kujua jina lake hakumaanishi kwamba unamjua vizuri. Haimaanishi kwamba unajua kila jambo linalomhusu.

2 Huenda unajua mambo fulani kumhusu Yesu Kristo, ingawa aliishi duniani karibu miaka 2,000 iliyopita. Hata hivyo, watu wengi hawajui alikuwa na utu gani. Wengine wanasema alikuwa mtu mwema, wengine nabii, na wengine waamini kwamba ni Mungu. Wewe una maoni gani?—Soma Maelezo ya Ziada 12.

3 Ni muhimu kujua ukweli kumhusu Yesu. Kwa nini? Biblia inasema: "Uzima wa milele ndio huu, waendelee kupata ujuzi juu yako wewe, Mungu wa pekee wa kweli, **na juu ya yule uliyemtuma, Yesu Kristo.**" (Yohana 17:3) Kwa kweli, ikiwa utajua ukweli kumhusu Yehova na Yesu, unaweza kuishi milele katika dunia paradiso. (Yohana 14:6) Pia, kumjua Yesu kutakusaidia kwa sababu ametuwekea mfano bora wa jinsi ya kuishi na kuwatendea wengine. (Yohana 13: 34, 35) Katika sura ya kwanza, tulijifunza ukweli ku-

---

1, 2. (a) Je, kujua tu jina la mtu fulani mashuhuri kunamaanisha unamjua vizuri? Eleza. (b) Watu wana maoni gani yanayotofautiana kumhusu Yesu?

3. Kwa nini ni muhimu umjue Yehova Mungu na Yesu Kristo?

mhusu Mungu. Sasa tutajifunza yale ambayo Biblia inafundisha kumhusu Yesu.

TUMEMPATA MASIHI!

4 Miaka mingi kabla ya Yesu kuzaliwa, Yehova aliahidi katika Biblia kwamba angemtuma Masihi, au Kristo. Neno "Masihi" linatokana na lugha ya Kiebrania, na neno "Kristo" linatokana na lugha ya Kigiriki. Majina hayo yanaonyesha kwamba Mungu angemchagua Masihi na kumpa cheo cha pekee. Masihi atatimiza ahadi zote za Mungu. Hata sasa, Yesu anaweza kukusaidia. Hata hivyo, kabla ya Yesu kuzaliwa, watu wengi walijiuliza, 'Ni nani atakayekuwa Masihi?'

5 Wanafunzi wa Yesu hawakuwa na shaka kwamba alikuwa Masihi. (Yohana 1:41) Kwa mfano, Simoni Petro alimwambia hivi Yesu: "Wewe ndiye Kristo." (Mathayo 16:16) Tuna uhakika gani kwamba Yesu ni Masihi?

6 Miaka mingi kabla ya Yesu kuzaliwa, Manabii wa Mungu waliandika habari nyingi ambazo zingewasaidia watu kumtambua Masihi. Kwa nini habari hizo ni muhimu? Tuseme umeombwa uende kituo cha basi kumpokea mtu ambaye hujawahi kumwona. Bila shaka, unaweza kumtambua ikiwa umepewa maelezo ya kutosha kumhusu. Vivyo hivyo, Yehova aliwatumia manabii wake waandike mambo ambayo Masihi angefanya na yale ambayo yangempata. Kutimia kwa unabii huo kunawasaidia

4. Maneno "Masihi" na "Kristo" yanaonyesha nini?
5. Je, wanafunzi wa Yesu waliamini kwamba Yesu alikuwa Masihi?
6. Yehova alifanya nini ili kuwasaidia watu wenye mioyo minyofu wamtambue Masihi?



watu wenye mioyo minyofu kujua kwamba Yesu ni Masihi.

7 Fikiria mifano miwili. Kwanza, miaka 700 kabla ya Yesu kuzaliwa, Mika alitabiri kwamba Masihi angezaliwa katika mji mdogo wa Bethlehemu. (Mika 5:2) Hivyo ndivyo ilivyokuwa! (Mathayo 2:1, 3-9) Pili, nabii Danieli alitabiri kwamba Yesu angekuwa Masihi mwaka wa 29 W.K. (Danieli 9:25) Hiyo ni mifano miwili tu ya unabii ambao unathibitisha kwamba Yesu ni Masihi aliyeahidiwa.—Soma Maelezo ya Ziada 13.

8 Yehova alifunua waziwazi kwamba Yesu ni Masihi. Mungu aliahidi kumpa Yohana mbatizaji ishara ili amtambue Masihi. Yohana aliona ishara hiyo, Yesu alipomwendea ili abatizwe katika mto Yordani mwaka wa 29 W.K. Biblia inatuambia mambo yaliyotukia: "Baada ya kubatizwa Yesu akapanda mara moja kutoka katika maji; na, tazama! mbingu zikafunguliwa, naye akaona roho ya Mungu ikishuka kama njiwa, ikija juu yake. Tazama! Kulikuwa pia na sauti kutoka mbinguni iliyosema: 'Huyu ni Mwanangu, mpendwa, ambaye nimemkubali.' " (Mathayo 3:16, 17) Yohana aliposikia na kuona ishara hiyo, alitambua kwamba Yesu ndiye Masihi. (Yohana 1:32-34) Yehova alipomi-


---

7. Ni mifano gani miwili ya unabii inayothibitisha kwamba Yesu ni Masihi?

8, 9. Ni mambo gani yalitukia Yesu alipobatizwa yanayothibitisha kwamba yeye ni Masihi?

mina roho yake juu ya Yesu, siku hiyohiyo Yesu akawa Masihi. Akawa Kiongozi na Mfalme aliyechaguliwa na Mungu.—Isaya 55:4.

9 Unabii wa Biblia, maneno ya Yehova mwenyewe, na ishara iliyotokea Yesu alipokuwa akibatizwa ni uthibitisho kwamba Yesu ni Masihi. Lakini Yesu alitoka wapi na alikuwa na utu gani? Acheni tuone jinsi Biblia inavyosema.



Baada ya kubatizwa, Yesu akawa Masihi au Kristo

YESU ALITOKA WAPI?

10 Biblia inafundisha kwamba Yesu aliishi mbinguni kwa miaka mingi kabla ya kuja duniani. Mika alisema kwamba Masihi ni wa "kutoka nyakati za kale." (Mika 5:2) Yesu mwenyewe mara nyingi alisema kwamba aliishi mbinguni kabla ya kuzaliwa akiwa mwanadamu. **(Soma Yohana 3:13; 6:38, 62; 17:4, 5.)** Hata kabla ya kuja duniani, Yesu alikuwa na uhusiano wa pekee na Yehova.

11 Yehova anampenda Yesu sana. Kwa nini? Kwa sababu Mungu alimuumba kwanza kabla hajaumba vitu vingine vyote. Kwa hiyo Yesu anaitwa "mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote."* (Wakolosai 1:15) Pia, Yehova anampenda sana Yesu kwa kuwa Yesu pekee ndiye aliyeumbwa moja kwa moja na Yehova. Hiyo ndiyo sababu anaitwa "Mwana wake mzaliwa-pekee." (Yohana 3:16) Pia, Yesu pekee ndiye aliyetumiwa na Yehova kuumba vitu vingine vyote. (Wakolosai 1:16) Yesu peke yake anaitwa "Neno," kwa sababu Yehova alimtumia kuwapa ujumbe na maagizo malaika na wanadamu.—Yohana 1:14.

12 Baadhi ya watu wanaamini kwamba Yesu ni sawa na Mungu Mweza-Yote. Lakini Biblia haifundishi hivyo. Biblia inafundisha kwamba Yesu aliumbwa. Ja-

* Yehova anaitwa Baba kwa sababu yeye ni Muumba. (Isaya 64:8) Yesu anaitwa Mwana wa Mungu kwa sababu aliumbwa na Yehova. Pia, Malaika na wanadamu, wanaitwa wana wa Mungu.—Ayubu 1:6; Luka 3:38.

10. Biblia inafundisha nini kuhusu maisha ya Yesu kabla ya kuja duniani?
11. Kwa nini Yehova anampenda Yesu?
12. Tunajuaje kwamba Yesu na Mungu hawako sawa?

mbo hilo linamaanisha kwamba alikuwa na mwanzo. Lakini Yehova aliyeumba vitu vyote hana mwanzo. (Zaburi 90:2) Akiwa Mwana wa Mungu, Yesu hakujaribu kamwe kujilinganisha na Mungu. Biblia inafundisha wazi kwamba Baba ni mkuu kuliko Mwana. **(Soma Yohana 14:28;** 1 Wakorintho 11:3.) Yehova peke yake ndiye "Mungu Mweza-Yote." (Mwanzo 17:1) Yeye ndiye mkuu na mwenye nguvu katika ulimwengu wote mzima.—Soma Maelezo ya Ziada 14.

13 Yehova na Mwana wake, Yesu, walifanya kazi kwa ukaribu kwa miaka mingi kabla ya kuumbwa kwa mbingu na dunia. Ni lazima walipendana sana! (Yohana 3:35; 14:31) Yesu aliiga sifa za baba yake kikamilifu hivi kwamba Biblia inamwita "mfano wa Mungu asiyeonekana."—Wakolosai 1:15.

14 Mwana mpendwa wa Yehova alikuwa tayari kuondoka mbinguni na kuzaliwa duniani akiwa mwanadamu. Iliwezekanaje? Yehova alimhamisha kimuujiza Mwana wake kutoka mbinguni hadi kwenye tumbo la uzazi la bikira aliyeitwa Maria. Kwa sababu hiyo, Yesu hakuwa na baba wa kibinadamu. Hivyo, Maria alimzaa mwana mkamilifu, na akamwita jina Yesu. —Luka 1:30-35.

YESU ALIKUWA NA UTU GANI?

15 Unaweza kujifunza mengi zaidi kuhusu Yesu, maisha yake, na sifa zake kwa kusoma vitabu vya

13. Kwa nini Biblia inasema Yesu ni "mfano wa Mungu asiyeonekana"?
14. Mwana mpendwa wa Yehova alizaliwa akiwa mwanadamu jinsi gani?
15. Unaweza kumjua vizuri Yehova jinsi gani?

Biblia vya Mathayo, Marko, Luka na Yohana. Vitabu hivyo vinaitwa Injili. Kwa kuwa Yesu ana sifa kama za Baba yake, yale utakayosoma yatakusaidia kumjua vizuri Yehova. Ndiyo sababu Yesu alisema: "Yule ambaye ameniona mimi amemwona Baba pia."—Yohana 14:9.

16 Watu wengi walimwita Yesu "Mwalimu." (Yohana 1:38; 13:13) Jambo muhimu ambalo Yesu alifundisha lilikuwa "habari njema ya Ufalme." Ufalme huo ni nini? Ni serikali ya Mungu iliyopo mbinguni itakayotawala ulimwengu mzima na kuwaletea baraka watu wanaomtii Mungu. (Mathayo 4:23) Kila jambo ambalo Yesu alifundisha lilitoka kwa Yehova. Yesu alisema: "Yale ninayofundisha si yangu, bali ni yake yeye aliyenituma." (Yohana 7:16) Yesu alijua kwamba Yehova anataka watu wasikie habari njema kwamba Ufalme wa Mungu utatawala ulimwengu mzima.

17 Yesu alifundisha wapi? Kila mahali penye watu. Alifundisha vijijini, mijini, sokoni, sehemu za ibada na kwenye nyumba za watu. Hakusubiri watu wamfuate. Aliwafuata walipokuwa. (Marko 6:56; Luka 19:5, 6) Yesu alikuwa na bidii sana, alitumia nguvu na wakati mwingi kuwafundisha watu. Kwa nini? Kwa sababu alijua kwamba Mungu alitaka afanye hivyo na sikuzote alimtii Baba yake. (Yohana 8:28, 29) Pia, Yesu alihubiri kwa sababu aliwasikitikia watu. **(Soma Mathayo 9:35, 36.)** Viongozi wa dini hawakufundisha watu kweli kumhusu Mungu na Ufalme wake. Hivyo, alitaka kuwasaidia watu wengi wasikie habari njema.

---

16. Yesu alifundisha nini? Mafundisho ya Yesu yalitoka wapi?
17. Yesu alifundisha wapi? Kwa nini Yesu alikuwa na bidii sana kuwafundisha watu?

18 Yesu aliwapenda na kuwajali watu. Alikuwa mwenye fadhili na urafiki. Hata watoto walipenda kuwa karibu naye. (Marko 10:13-16) Yesu alipenda haki. Alichukia ufisadi na ukosefu wa haki. (Mathayo 21:12, 13) Aliishi wakati ambao wanawake walidharauliwa na kunyimwa baadhi ya haki zao. Lakini sikuzote Yesu aliwaheshimu na kuwastahi wanawake. (Yohana 4:9, 27) Pia, Yesu alikuwa mnyenyekevu sana. Kwa mfano, siku moja aliwaosha wanafunzi wake miguu, jambo ambalo kwa kawaida lilifanywa na watumwa.—Yohana 13:2-5, 12-17.

19 Yesu alijua mahitaji ya watu, na alitaka kuwasaidia. Jambo hilo lilionekana waziwazi alipotumia nguvu za Mungu kuwaponya kimuujiza. (Mathayo 14:14) Kwa mfano, mwanamume mwenye ukoma alimwendea Yesu na kumwambia: "Ikiwa tu unataka, unaweza kunitakasa." Ndipo akamsikitikia, naye akanyoosha mkono wake akamgusa, akamwambia: "Ninataka. Takasika." Mwanaume huyo akapona! (Marko 1:40-42) Unafikiri mwanamume huyo alihisije?

SIKUZOTE ALIKUWA MWAMINIFU KWA BABA YAKE

20 Yesu ni mfano bora wa kumtii Mungu. Licha ya hali au kutendewa vibaya na maadui wake, aliendelea kuwa mwaminifu kwa Baba yake. Kwa mfano, Yesu hakutenda dhambi Shetani alipomjaribu. (Mathayo 4:1-11) Baadhi ya watu wa familia yake hawakuamini kwamba alikuwa Masihi, hata walisema kwamba


18. Ni sifa gani za Yesu zinazokuvutia?
19. Ni mfano gani unaoonyesha kwamba Yesu alijua mahitaji ya watu na kwamba alitaka kuwasaidia?
20, 21. Yesu ametuwekea jinsi gani mfano bora wa kumtii Mungu?



Yesu alihubiri mahali popote penye watu

“amerukwa na akili” hata hivyo, Yesu aliendelea kufanya kazi ya Mungu. (Marko 3:21) Alipotendewa jeuri na adui zake, Yesu aliendelea kuwa mwaminifu kwa Mungu na hakujaribu kuwadhuru.—1 Petro 2: 21-23.

21 Hata alipokabili kifo cha kikatili na maumivu makali, Yesu aliendelea kuwa mwaminifu kwa Yehova. **(Soma Wafilipi 2:8.)** Wazia jinsi alivyohitaji kuvumilia siku aliyokufa. Alikamatwa, akashtakiwa na mashahidi wa uwongo, akahukumiwa na mahakimu fisadi, akachekwa na umati, na askari walimtesa na kumtundika kwenye mti wa mateso. Alipokuwa anakufa alipaaza sauti: “Imetimizwa! (Yohana



19:30) Siku tatu baada ya Yesu kufa, Yehova alimfufua na kumfanya hai katika roho. (1 Petro 3:18) Majuma machache baadaye, alirudi mbinguni, na "kuketi kwenye mkono wa kuume wa Mungu," akingojea Mungu amweke rasmi kuwa Mfalme.—Waebrania 10: 12, 13.

22 Kwa kuwa Yesu alibaki mwaminifu kwa Baba yake, sasa tuna fursa ya kuishi milele katika dunia paradiso, kama tu Yehova alivyoahidi. Katika sura inayofuata, tutazungumzia jinsi kifo cha Yesu kinavyotuwezesha kupata uzima wa milele.

---

22. Ni fursa gani tunayopata kwa sababu Yesu alikuwa mwaminifu kwa Baba yake?

UKWELI WA 1 YESU NDIYE MASIHI

"Wewe ndiye Kristo."—Mathayo 16:16

Tunajua jinsi gani kwamba Yesu ndiye Masihi?

Mathayo 3:16, 17; Yohana 1:32-34
Yehova alimtambulisha Yesu kuwa Mwanaye.

Mika 5:2; Mathayo 2:1, 3-9
Yesu alitimiza unabii unaomhusu Masihi.

UKWELI WA 2 YESU ALIKUWA MALAIKA KABLA YA KUJA DUNIANI

"Nimeshuka kutoka mbinguni."—Yohana 6:38

Yesu alikuwa akifanya nini mbinguni?

Wakolosai 1:15, 16
Yehova alimuumba Yesu kwanza, kisha akamtumia kuumba vitu vingine vyote. Yesu alijifunza kutoka kwa Baba yake kwa mabilioni ya miaka.

Luka 1:30-35
Yehova alimtuma Yesu duniani.

UKWELI WA 3 YESU ANAWAPENDA WATU

"Waacheni watoto wachanga waje kwangu."—Marko 10:14

Ni sifa gani za Yesu zinazokuvutia?

Marko 10:13-16
Yesu ni mwenye fadhili, na watu walifurahia kuzungumza naye.

Yohana 4:9, 27
Yesu aliwaheshimu na kuwastahi wanawake.

Yohana 13:2-5, 12-17
Yesu alikuwa mnyenyekevu.

Mathayo 9:35, 36; Marko 1:40-42
Yesu anapenda kuwasaidia wengine.

UKWELI WA 4 YESU HUFANYA MAPENZI YA MUNGU SIKUZOTE

"Nimemaliza kazi ambayo umenipa niifanye."—Yohana 17:4

Mfano wa Yesu unatusaidia jinsi gani kuendelea kuwa waaminifu?

Mathayo 4:1-11
Yesu alikuwa mwaminifu alipojaribiwa na Ibilisi.

Marko 3:21
Yesu aliendelea kufanya mapenzi ya Mungu ingawa ndugu zake walimdhihaki.

1 Petro 2:21-23
Yesu hakulipiza kisasi.

Wafilipi 2:8
Yesu aliendelea kuwa mwaminifu hata alipokabili kifo.

Waebrania 10:12, 13; 1 Petro 3:18
Yehova alimfufua Yesu akaishi mbinguni.

FIDIA —ZAWADI BORA KUTOKA KWA MUNGU

NI ZAWADI gani bora ambayo umewahi kupewa? Si lazima zawadi iwe ya bei ghali ili uithamini. Zawadi bora ni ile unayofurahia au inayotimiza mahitaji yako.

2 Kuna zawadi moja tu kutoka kwa Mungu ambayo wanadamu wanahitaji sana. Ni zawadi muhimu sana ambayo Mungu amewapa wanadamu. Katika sura hii, tutajifunza kwamba Yehova alimtuma Mwana wake, Yesu Kristo, ili tuweze kuishi milele. **(Soma Mathayo 20:28.)** Yehova amethibitisha kwamba anatupenda sana kwa kumtuma Yesu duniani ili awe fidia.

FIDIA NI NINI?

3 Fidia ni njia ya Mungu ya kuwakomboa wanadamu kutokana na dhambi na kifo. (Waefeso 1:7) Ili tuelewe umuhimu wa fidia, tunahitaji kujua kilichotokea miaka mingi iliyopita katika bustani ya Edeni. Wazazi wetu wa kwanza, Adamu na Hawa, walifanya dhambi. Kwa sababu hiyo, walikufa. Sisi pia, tunakufa kwa sababu tumerithi dhambi kutoka kwa Adamu na Hawa.—Soma Maelezo ya Ziada 9.

1, 2. (a) Wewe ungependa zawadi ya aina gani? (b) Kwa nini fidia ni zawadi muhimu sana ambayo Mungu amewapa wanadamu?
3. Kwa nini wanadamu wanakufa?

4 Yehova alipomuumba mwanadamu wa kwanza, Adamu, alimpa kitu chenye thamani. Alimpa uhai mkamilifu. Alikuwa na mwili na akili kamilifu. Adamu hangekuwa mgonjwa, hangezeeka, na kufa. Yehova alikuwa baba yake kwa sababu ndiye aliyemuumba. (Luka 3:38) Yehova alizungumza kwa ukawaida na Adamu. Alimweleza waziwazi mapenzi yake na kumpa kazi yenye kuridhisha.—Mwanzo 1:28-30; 2: 16, 17.

5 Adamu aliumbwa "kwa mfano wa Mungu." (Mwanzo 1:27) Inamaanisha Adamu aliumbwa akiwa na sifa kama za Yehova, yaani, upendo, hekima, haki, na nguvu. Adamu alipewa uhuru wa kuchagua na hakuwa kama mashine. Aliumbwa na Mungu akiwa na uhuru wa kuchagua kufanya mambo yanayofaa au yasiyofaa. Ikiwa Adamu angechagua kumtii Mungu, angeishi milele katika dunia Paradiso.

6 Adamu alipokosa kumtii Mungu, alihukumiwa kifo na kusababisha hasara kubwa sana. Alipoteza uhusiano wake pamoja na Yehova, uhai mkamilifu, na makao yake katika Paradiso. (Mwanzo 3: 17-19) Adamu na Hawa walipoteza tumaini kwa sababu walichagua kutomtii Mungu. Uamuzi huo wa Adamu ulifanya 'dhambi iingie katika ulimwengu na kifo kupitia dhambi, na hivyo kifo kikaenea kwa watu wote kwa sababu wote walikuwa wamefanya dhambi.' (Waroma 5:12) Adamu alipofanya dhambi 'alijiuza'

---

4. Adamu alikuwa nani, na alikuwa na nini?
5. Biblia inamaanisha nini inaposema kwamba Adamu aliumbwa "kwa mfano wa Mungu"?
6. Adamu alipoteza nini alipokosa kumtii Mungu? Hali hiyo inatuathirije?

mwenyewe na wazao wake katika utumwa wa dhambi na kifo. (Waroma 7:14) Je, wazao wa Adamu wana tumaini lolote? Ndiyo.

7 Fidia ni nini? Fidia inahusisha mambo mawili ya msingi. Kwanza, fidia ni bei inayolipwa ili kumkomboa mtu au kurudisha kitu. Pili, fidia ni gharama ambayo mtu hulipia kitu fulani alichopoteza au kuharibu.

8 Hakuna mwanadamu ambaye angeweza kulipia hasara kubwa ambayo Adamu alisababisha alipofanya dhambi na hivyo kutuletea kifo. Hata hivyo, Yehova aliandaa njia ya kutukomboa kutokana na dhambi na kifo. Hebu tuzungumzie fidia na jinsi ambavyo tunaweza kufaidika.

JINSI AMBAVYO YEHOVA ALIANDAA FIDIA

9 Hakuna mwanadamu ambaye angeweza kulipia fidia kwa ajili ya uhai mkamilifu ambao Adamu alipoteza. Kwa nini? Kwa sababu hatujakamilika. (Zaburi 49:7, 8) Fidia hiyo ingeweza kulipwa na uhai mwingine mkamilifu wa mwanadamu. Ndiyo sababu inaitwa "fidia inayolingana." (1 Timotheo 2:6) Fidia hiyo ilipaswa kuwa na thamani inayolingana na uhai ambao Adamu aliupoteza.

10 Yehova aliandaa fidia jinsi gani? Yehova alimtuma duniani Mwana wake mpendwa. Mwana huyo, Yesu, ndiye uumbaji wa kwanza wa Mungu. (1 Yohana 4:9, 10) Yesu alikuwa tayari kumwacha Baba na makao yake ya mbinguni. (Wafilipi 2:7) Yehova ali-

---

7, 8. Fidia ni nini?
9. Fidia ingelipwa jinsi gani?
10. Yehova aliandaa fidia jinsi gani?

mhamisha Yesu kutoka mbinguni hadi duniani, naye akazaliwa akiwa mwanadamu mkamilifu, asiye na dhambi.—Luka 1:35.

11 Mwanadamu wa kwanza, Adamu, alipoteza uhai mkamilifu wa wanadamu wote alipokosa kumtii Yehova. Je, ingewezekana mwanadamu mwingine kuondoa kifo kwa wanadamu wote? Ndiyo. **(Soma Waroma 5:19.)** Yesu, ambaye hajawahi kutenda dhambi alitoa uhai wake mkamilifu uwe fidia. (1 Wakorintho 15:45) Uhai wake mkamilifu ungewaondolea kifo wazao wote wa Adamu.—1 Wakorintho 15:21, 22.

12 Biblia hueleza jinsi Yesu alivyoteseka kabla ya kifo chake. Alipigwa mijeledi, akatundikwa katika mti wa mateso, na kuvumilia kifo chenye maumivu. (Yohana 19:1, 16-18, 30) Kwa nini ilikuwa lazima Yesu ateseka sana? Ni kwa sababu Shetani alidai kwamba wanadamu hawawezi kuendelea kuwa waaminifu kwa Mungu wanapojaribiwa. Yesu alithibitisha kwamba mwanadamu mkamilifu anaweza kuendelea kuwa mwaminifu kwa Mungu licha ya mateso. Naam, uaminifu wa Yesu ulimfurahisha sana Yehova! —Methali 27:11; soma Maelezo ya Ziada 15.

13 Fidia ililipwa jinsi gani? Yesu alimpa Baba yake uhai wake mkamilifu. Mwaka wa 33, Nisani 14, kulingana na kalenda ya Kiyahudi, Yehova aliruhusu mwana wake auawe na maadui zake. (Waebrania 10:10) Baada ya siku tatu, Yehova alimfufua Yesu akiwa kiumbe wa roho. Yesu aliporudi mbinguni, alimpa Yehova thamani ya uhai wake mkamilifu wa

---

11. Mtu mmoja angewezaje kuwa fidia kwa ajili ya wanadamu wote?
12. Kwa nini ilikuwa lazima Yesu ateseke?
13. Fidia ililipwa jinsi gani?

kibinadamu uwe fidia. (Waebrania 9:24) Kwa kuwa fidia imelipwa, tumewekwa huru kutokana na dhambi na kifo.**—Soma Waroma 3:23, 24.**

JINSI TUNAVYOFAIDIKA NA FIDIA


14 Tunafaidika na zawadi bora ya Mungu. Hebu tuzungumzie jinsi tunavyofaidika sasa na wakati ujao.

15 Tunasamehewa dhambi zetu. Si rahisi kufanya yaliyo sawa kila wakati. Mara nyingi sisi hutenda au kusema mambo mabaya. (Wakolosai 1:13, 14) Tunapaswa kufanya nini ili tusamehewe? Ni lazima tutubu na kumwomba Yehova atusamehe dhambi zetu. Tuwe na uhakika kwamba dhambi zetu zitasamehewa.—1 Yohana 1:8, 9.

16 Tunakuwa na dhamiri safi. Dhamiri yetu inapotushtaki kwamba tumetenda dhambi, tunajihisi hatufai au wenye hatia. Hata hivyo, tusikate tamaa. Tuna uhakika kwamba Yehova atatusikiliza na kutusamehe ikiwa tutamwomba msamaha. (Waebrania 9:13, 14) Yehova angependa tumweleze matatizo na udhaifu wetu pia. (Waebrania 4:14-16) Kwa njia hiyo, tunakuwa na uhusiano mzuri na Mungu.

17 Tuna tumaini la kuishi milele. "Kwa maana mshahara ambao dhambi hulipa ni kifo, lakini zawadi ambayo Mungu hutoa ni uzima wa milele kupitia Kristo Yesu Bwana wetu." (Waroma 6:23) Kwa kuwa Yesu alikufa kwa ajili yetu, tuna tumaini la kuishi milele na kuwa na afya kamilifu. (Ufunuo 21:3, 4) Hata hivyo, tunapaswa kufanya nini ili tupate baraka hizo?

14, 15. Ni lazima tufanye nini ili tusamehewe dhambi zetu?
16. Ni lazima tufanye nini ili tuwe na dhamiri safi?
17. Tutapata baraka gani kwa sababu ya kifo cha Yesu?



Yehova alimtoa
Mwana wake
mpendwa awe
fidia kwa ajili yetu

ITHAMINI FIDIA!


18 Fikiria jinsi unavyofurahi ukipewa zawadi. Fidia ni zawadi bora sana, na tunapaswa kumshukuru Yehova kwa zawadi hiyo. Andiko la Yohana 3:16 linasema kwamba "Mungu aliupenda ulimwengu sana hivi kwamba akamtoa Mwana wake mzaliwa-pekee." Naam, Yehova anatupenda sana hivi kwamba alimtoa Mwana wake mpendwa, Yesu. Tunajua kwamba Yesu anatupenda kwa sababu alikubali kufa kwa ajili yetu. (Yohana 15:13) Zawadi hiyo ya fidia inapaswa kukusadikishia kwamba Yehova na Yesu wanakupenda sana. —Wagalatia 2:20.

19 Kwa kuwa umejifunza kuhusu upendo mkubwa wa Mungu, ufanye nini ili uwe rafiki yake? Si rahisi kumpenda mtu usiyemjua. Andiko la Yohana 17:3 linasema kwamba **tuendelee kupata ujuzi juu ya Yehova.** Kadiri unavyomjua, utazidi kumpenda, kumfurahisha, na kuwa rafiki yake. Kwa hiyo, endelea kumjua Yehova kwa kujifunza Biblia.—1 Yohana 5:3.

20 Thamini dhabihu ya fidia ya Yesu. Biblia inasema kwamba "yule anayemwamini Mwana ana uzima wa milele." (Yohana 3:36) Kuwa na imani kuna maanisha nini? Humaanisha kufanya mambo ambayo Yesu alifundisha. (Yohana 13:15) Haitoshi tu kusema tunamwamini Yesu. Ili tuonyeshe kwamba tunaithamini fidia ni lazima tutende kulingana na imani yetu. Tunasoma hivi katika Yakobo 2:26, "Imani bila matendo imekufa."

---

18. Tunajua jinsi gani kwamba Yehova anatupenda?
19, 20. (a) Unaweza kufanya nini ili uwe rafiki ya Yehova? (b) Unaweza kuonyesha jinsi gani kwamba unathamini dhabihu ya fidia ya Yesu?



Tukiendelea kujifunza kumhusu Yehova tutakuwa rafiki zake na tutampenda zaidi

21 Hudhuria Ukumbusho wa kifo cha Kristo. Kabla ya kifo chake, Yesu alitufundisha kwamba tunapaswa kukumbuka kifo chake. Tunakumbuka kifo cha Yesu kila mwaka, na tukio hilo huitwa Ukumbusho au "Mlo wa Jioni wa Bwana." (1 Wakorintho 11:20; Mathayo 26:26-28) Yesu angependa tukumbuke kwamba alitoa uhai wake mkamilifu kuwa fidia kwa ajili yetu. Alisema hivi: "Endeleeni kufanya hivi kwa kunikumbuka mimi." **(Soma Luka 22:19.)** Kwa kuhudhuria Ukumbusho, unaonyesha kwamba unathamini fidia na jinsi Yehova na Yesu wanavyotupenda sana. —Soma Maelezo ya Ziada 16.

22 Fidia ndiyo zawadi bora zaidi ambayo tunaweza kupata. (2 Wakorintho 9:14, 15) Zawadi hiyo yenye thamani itawanufaisha hata mamilioni ya watu ambao wamekufa. Habari hiyo itazungumziwa katika sura ya 6 na ya 7.

21, 22. (a) Kwa nini tunapaswa kuhudhuria Ukumbusho wa kifo cha Yesu kila mwaka? (b) Tutazungumzia nini katika Sura ya 6 na ya 7?

UKWELI WA 1 SOTE TUNAHITAJI FIDIA

‘Mwana wa binadamu alikuja kutoa nafsi yake kuwa fidia badala ya wengi.’—Mathayo 20:28

Kwa nini tunahitaji fidia?

Mwanzo 3:17-19
Adamu alipomwasi Mungu alipoteza uhusiano wake wa pekee na Yehova, uhai mkamilifu, na Paradiso.

Waroma 5:12
Kwa sababu ya kosa la Adamu, tumerithi dhambi na kifo.

Waefeso 1:7
Fidia ni mpango wa Yehova wa kuwakomboa wanadamu kutoka katika dhambi na kifo.

UKWELI WA 2 YEHOVA ALIANDAA FIDIA

“Mungu alimtuma Mwana wake mzaliwa-pekee kuja ulimwenguni ili tupate uzima kupitia yeye.” —1 Yohana 4:9

Yehova aliandaa fidia jinsi gani?

Zaburi 49:7, 8
Hakuna mwanadamu ambaye angeweza kulipia fidia kwa ajili ya uhai mkamilifu ambao Adamu alipoteza.

Luka 1:35
Yehova alimtuma duniani Mwana wake wa pekee ili aje azaliwe akiwa mwanadamu mkamilifu.

Waroma 3:23, 24; Waebrania 9:24
Yesu alipofufuliwa alirudi mbinguni, akiwa huko alimpa Yehova thamani ya uhai wake mkamilifu wa kibinadamu uwe fidia.

UKWELI WA 3 FIDIA HUTUPATIA TUMAINI HAKIKA

"Naye atafuta kila chozi kutoka katika macho yao, na kifo hakitakuwapo tena."—Ufunuo 21:4

Tunaweza kufaidika jinsi gani kutokana na fidia?

1 Yohana 1:8, 9
Dhambi zetu zinaweza kusamehewa.

Waebrania 9:13, 14
Tunaweza kuwa na dhamiri safi mbele za Mungu.

Waroma 6:23
Tuna tumaini la uzima wa milele.

Wagalatia 2:20
Zawadi ya fidia ni uthibitisho kwamba Yehova na Yesu wanatupenda sana.

UKWELI WA 4 TUNAHITAJI KUKUBALI FIDIA

'Mungu alimtoa Mwana wake mzaliwa-pekee, ili kila mtu anayemwamini awe na uzima wa milele.'—Yohana 3:16

Tunaweza kuonyesha jinsi gani kwamba tunaithamini zawadi ya Mungu ya fidia?

Yohana 17:3
Mjue Yehova na Yesu na uwaige.

Luka 22:19
Hudhuria Ukumbusho wa kifo cha Kristo kila mwaka.

Yohana 3:36; Yakobo 2:26
Fanya mengi zaidi ya kusema tu ninamwamini Yesu. Tenda yale ambayo Yesu alitufundisha.

TUKIFA TUNAENDA WAPI?

BIBLIA inatuahidi kwamba “kifo hakitakuwapo tena.” (Ufunuo 21:4) Katika sura ya 5, tulijifunza kwamba fidia inatuwezesha kupata uzima wa milele. Lakini bado tunaendelea kufa. (Mhubiri 9:5) Hivyo swali ni, Tukifa tunaenda wapi?

2 Jibu la swali hilo ni muhimu hasa tunapofiwa na mtu tunayempenda. Huenda tukajiuliza: ‘Ameenda wapi? Je, anatuona? Je, anaweza kutusaidia? Je, tutamwona tena?’

3 Dini nyingi hujibu maswali hayo kwa njia tofauti. Baadhi hufundisha kwamba ikiwa unatenda mema utaenda mbinguni na ikiwa unatenda mabaya utaenda motoni. Nyingine hufundisha kwamba ukifa unabadilika na kuwa roho kisha unaenda kuishi na ndugu zako waliokufa. Na nyingine hufundisha kwamba baada ya kufa na kuhukumiwa, unazaliwa upya, au kuwa hai tena ukiwa na mwili tofauti, labda ukiwa mwanadamu au mnyama.

4 Mambo ambayo dini hufundisha hutofautiana. Hata hivyo, karibu dini hizo zote hufundisha wazo moja kuu. Zinafundisha kwamba mtu akifa, sehemu fulani ya mwanadamu huendelea kuishi. Je, ni kweli?

1-3. Huenda ukauliza maswali gani kuhusu kifo, na baadhi ya dini hujibuje?

4. Ni wazo gani kuu ambalo dini nyingi hufundisha kuhusu kifo?

TUKIFA TUNAENDA WAPI?

5 Yehova anajua hali ya wafu, na ametueleza kwamba **mtu akifa, uhai wake unakoma.** Kifo ni kinyume cha uhai. Kwa hiyo mtu akifa, **haendelei** kuishi mahali pengine, hisia na mawazo yake hupotea.* Tukifa hatuwezi kuona, kusikia, wala kufikiri.

6 Mfalme Sulemani aliandika kwamba "wafu hawajui **lolote kamwe.**" Wafu hawawezi kupenda au kuchukia, na "hakuna kazi, wala utungaji wala ujuzi wala hekima katika Kaburi." **(Soma Mhubiri 9:5, 6, 10.)** Na katika Zaburi 146:4, Biblia inatuambia kwamba, mtu akifa "mawazo yake" hupotea.

YESU ALISEMA NINI KUHUSU KIFO?

7 Rafiki yake mpendwa Lazaro alipokufa, Yesu aliwaambia wanafunzi wake: "Lazaro rafiki yetu amelala usingizi." Lakini Yesu hakumaanisha kwamba Lazaro alikuwa amepumzika. Yesu akaendelea kusema: "Lazaro amekufa." (Yohana 11:11-14) Kwa hiyo Yesu alilinganisha kifo na usingizi. Hakusema kwamba Lazaro alikuwa mbinguni au pamoja na watu wa familia yake waliokufa zamani. Wala hakusema Lazaro anateseka katika moto wa mateso au amezaliwa upya akiwa mwanadamu au mnyama. Alimaanisha kwamba ni kama Lazaro alikuwa amelala usingizi mzito. Maandiko mengine hufananisha kifo na usingizi mzito. Biblia inasema kwamba Stefano alipouawa, 'alilala

* Baadhi ya watu huamini kwamba roho huendelea kuishi baada ya mtu kufa. Ili kupata habari zaidi, tafadhali soma Maelezo ya Ziada 17 na 18.

5, 6. Tukifa tunaenda wapi?
7. Yesu alisema nini kuhusu kifo?

usingizi katika kifo.' (Matendo 7:60) Pia, mtume Paulo aliandika kwamba baadhi ya Wakristo walikuwa "wamelala usingizi katika kifo."—1 Wakorintho 15:6.

8 Je, Mungu aliwaumba Adamu na Hawa ili wafe? Hapana! Yehova aliwaumba wafurahie maisha milele wakiwa na uhai mkamilifu. Yehova aliwaumba wanadamu wakiwa na tamaa ya kuishi milele. (Mhubiri 3: 11) Wazazi hawapendi watoto wao wazeeke na kufa na Yehova pia anahisi hivyo kutuhusu. Hata hivyo, ikiwa Yehova alituumba tuishi milele, kwa nini tunakufa?

8. Tunajuaje kwamba Yehova hakuwaumba wanadamu ili wafe?



Yehova aliwaumba wanadamu ili waishi milele duniani

KWA NINI TUNAKUFA?

9 Katika bustani ya Edeni, Yehova alimwagiza Adamu hivi: "Matunda ya kila mti wa bustani unaweza kula mpaka ushibe. Lakini kuhusu matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula, utakufa hakika." (Mwanzo 2:9, 16, 17) Haikuwa vigumu kutii amri hiyo iliyo wazi na Yehova alikuwa na haki ya kuwaeleza Adamu na Hawa jambo linalofaa na lisilofaa. Kwa kumtii Yehova, wangeonyesha kwamba wanaheshimu mamlaka yake. Pia, utii ungeonyesha kwamba wanathamini mambo yote ambayo Yehova aliwapa.

10 Inasikitisha kwamba Adamu na Hawa waliamua kutomtii Yehova. Shetani alimwuliza Hawa hivi: "Je, ni kweli kwamba Mungu alisema msile matunda ya kila mti wa bustani?" Hawa akamjibu: "Tunaweza kula matunda ya miti ya bustani. Lakini kuhusu kula matunda ya mti ulio katikati ya bustani, Mungu amesema, 'Msiyale, wala msiyaguse ili msife.' "—Mwanzo 3:1-3.

11 Ndipo Shetani akamwambia: "Hakika hamtakufa. Kwa maana Mungu anajua kwamba siku ileile mtakapokula matunda yake macho yenu yatafunguliwa, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya." (Mwanzo 3:4-6) Shetani alitaka Hawa afikiri kwamba angeweza kujiamulia mwenyewe mambo mema na mabaya. Pia, alimdanganya kuhusu matokeo ya kutomtii Mungu. Shetani alimwambia Hawa

---

9. Kwa nini Adamu na Hawa walipaswa kutii amri ya Yehova?

10, 11. (a) Shetani aliwadanganya Adamu na Hawa jinsi gani? (b) Kwa nini Adamu na Hawa hawakuwa na sababu ya kutotii amri ya Mungu?

kwamba hangekufa, hivyo akala tunda na baadaye akampa mume wake. Adamu na Hawa walijua kabisa kwamba Mungu **aliwakataza** kula matunda hayo. Hivyo walipokula tunda hilo, walikosa kutii amri rahisi na iliyo wazi. Jambo hilo lilionyesha wazi kwamba walimdharau Baba yao mpendwa wa mbinguni. Hawakuwa na sababu ya kutotii amri ya Mungu!

12 Inasikitisha kwamba wazazi wetu wa kwanza hawakumheshimu Muumba wao! Ungehisije ikiwa umejitahidi kuwalea vizuri watoto wako lakini baadaye wanakuasi na kufanya mambo tofauti kabisa na uliyowafundisha? Je, hungeumia sana?

13 Walipomwasi Mungu, Adamu na Hawa walipoteza fursa ya kuishi milele. Yehova alimwambia Adamu hivi: "Kwa maana wewe ni mavumbi nawe utarudi mavumbini." (**Soma Mwanzo 3:19.**) Jambo hilo lilimaanisha kwamba Adamu angekuwa mavumbi kana kwamba hakuwahi kuishi. (Mwanzo 2:7) Baada ya Adamu kutenda dhambi alikufa na hayupo tena.

Adamu aliumbwa kwa mavumbi na alirudi kuwa mavumbi



14 Kama Adamu na Hawa wangemtii Mu-

12. Kwa nini inasikitisha kwamba Adamu na Hawa walimwasi Yehova?

13. Yehova alimaanisha nini aliposema "utarudi mavumbini"?

14. Kwa nini tunakufa?

ngu, wangekuwa hai mpaka leo. Lakini walipokataa kumtii, walitenda dhambi na hatimaye walikufa. Dhambi ni kama ugonjwa hatari tuliorithi kutoka kwa wazazi wetu wa kwanza. Sote huzaliwa tukiwa na dhambi na ndiyo sababu tunakufa. (Waroma 5:12) Lakini hilo halikuwa kusudi la Mungu alipowaumba wanadamu. Mungu hakutaka wanadamu wafe, ndiyo sababu Biblia hukiita kifo "adui."—1 Wakorintho 15:26.

UKWELI UNATUWEKA HURU

15 Kujua ukweli kuhusu wafu hutuweka huru na maoni yaliyopotoka. Biblia inatufundisha kwamba wafu hawahisi maumivu wala huzuni. Hatuwezi kuwasiliana nao. Hatuwezi kuwasaidia, wala hawawezi kutusaidia. Hawawezi kutudhuru, hivyo hatupaswi kuwaogopa. Hata hivyo, dini nyingi hufundisha kwamba wafu wanaendelea kuishi mahali fulani na tunaweza kuwasaidia kwa kuwapa viongozi wa kidini au watakatifu kiasi fulani cha pesa ili wawaombee. Lakini tukijua ukweli kuhusu kifo hatutadanganywa.

16 Shetani anatumia dini za uwongo kutupotosha na kufanya tuhisi kwamba wafu wapo hai. Kwa mfano, baadhi ya dini hufundisha kwamba tunapokufa, roho huendelea kuishi mahali fulani. Je, dini yako imekufundisha hivyo au je, inakufundisha mambo ambayo Biblia hufundisha kuhusu wafu? Shetani anatumia uwongo kuwatenganisha watu na Yehova.

17 Mambo ambayo dini nyingi hufundisha

15. Kwa nini kujua ukweli kuhusu kifo hutuweka huru?
16. Dini nyingi hufundisha uwongo gani kuhusu wafu?
17. Kwa nini fundisho la moto wa mateso linamshushia heshima Yehova?

yanatisha. Kwa mfano, baadhi ya dini hufundisha kwamba Mungu huwatesa watu waovu motoni milele. Uwongo huo humshushia heshima Yehova. Hawezi kamwe kuwatesa hivyo wanadamu! **(Soma 1 Yohana 4:8.)** Ungehisije ikiwa mzazi anamwadhibu mtoto wake kwa kumchoma moto mikono? Bila shaka utamwona kuwa katili sana. Hata, hungependa awe rafiki yako. Hivyo ndivyo Shetani anataka tuhisi hivyo kumhusu Yehova!

18 Baadhi ya dini hufundisha kwamba watu wakifa, hubadilika na kuwa viumbe wa roho. Dini hizo hufundisha kwamba wanapaswa kuwaheshimu na kuwaogopa roho hao kwa sababu wanaweza kuwa rafiki au maadui. Watu wengi wanaamini uwongo huo. Wanawaogopa wafu, kwa hiyo huwaabudu badala ya kumwabudu Yehova. Kumbuka kwamba wafu hawahisi chochote, hivyo basi hatuna sababu ya kuwaogopa. Yehova ndiye aliyetuumba. Yeye ndiye Mungu wa kweli, na tunapaswa kumwabudu peke yake.—Ufunuo 4:11.

19 Kujua ukweli kuhusu kifo, hutuweka huru kutokana na mafundisho ya uwongo. Pia, ukweli huo unatusaidia kuelewa vizuri sana ahadi za Yehova za wakati ujao.

20 Miaka mingi iliyopita, mtumishi wa Mungu, Ayubu, aliuliza hivi: “Mtu akifa, je, anaweza kuishi tena?” (Ayubu 14:14) Je, kweli mtu aliyekufa anaweza kufufuka? Mungu anatupatia jibu zuri sana katika Biblia. Tutajifunza jambo hilo katika sura inayofuata.

---

18. Kwa nini hatupaswi kuogopa wafu?
19. Kuna faida gani kujua ukweli kuhusu kifo?
20. Tutajifunza nini katika sura inayofuata?

UKWELI WA 1 MTU AKIFA, UHAI WAKE UNAKOMA

‘Wafu hawajui lolote kamwe.’—Mhubiri 9:5

Ni nini hutokea tukifa?

Zaburi 146:3, 4; Mhubiri 9:6, 10
Tukifa hatuwezi kuona, kusikia, wala kufikiri.

Yohana 11:11-14
Yesu alilinganisha kifo na usingizi.

UKWELI WA 2 YEHOVA HAKUKUSUDIA WATU WAFE

“Kuhusu matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula, utakufa hakika.”—Mwanzo 2:17

Kwa nini tunakufa?

Mwanzo 3:1-6
Shetani alimdanganya Hawa kuhusu matokeo ya kutotii sheria ya Mungu. Adamu na Hawa walipomwasi Yehova, walitenda dhambi na hatimaye wakafa.

Mwanzo 3:19
Adamu alipokufa, alikoma kuwapo.

Waroma 5:12
Dhambi ni kama ugonjwa hatari ambao tumerithi kutoka kwa wazazi wetu wa kwanza. Sote tunazaliwa tukiwa na dhambi, na ndiyo sababu tunakufa.

1 Wakorintho 15:26
Biblia inasema kwamba kifo ni adui.

UKWELI WA 3 UKWELI KUHUSU KIFO HUTUWEKA HURU

"Mtu akifa, je, anaweza kuishi tena? Mimi nitangojea . . . mpaka kitulizo changu kije."—Ayubu 14:14

Kujua ukweli kuhusu kifo hutuweka huru jinsi gani kutokana na mafundisho ya uwongo?

1 Yohana 4:8
Fundisho la moto wa mateso linamshushia heshima Yehova. Hawezi kamwe kuwatesa watu.

Ufunuo 4:11
Watu wengi huwaogopa wafu, kwa sababu hiyo huwaabudu badala ya kumwabudu Yehova. Yehova ndiye Mungu wa kweli, na tunapaswa kumwabudu yeye pekee.

KUTAKUWA NA UFUFUO!

WAZIA kwamba umehukumiwa kifungo cha maisha kwa kosa ambalo hukutenda. Hakuna uwezekano wa kuachiliwa huru. Umekata tamaa, na huna la kufanya. Hata hivyo, ukiwa umekata tamaa kabisa, unagundua kwamba mtu fulani ana uwezo wa kukuweka huru na hata ameahidi kukusaidia! Utahisije?

2 Sote tumehukumiwa kifo. Hata tufanye nini, hatuwezi kukiepuka. Hata hivyo, Yehova ana nguvu za kutuweka huru kutoka kwenye kifo. Ameahidi kwamba "adui wa mwisho atakayeangamizwa ni kifo." —1 Wakorintho 15:26.

3 Wazia jinsi utakavyohisi wakati ambao watu hawatakufa! Yehova hataondoa kifo tu, bali atawafufua wale ambao wamekufa. Fikiria jinsi mambo yatakavyokuwa. Anaahidi kwamba "wasiojiweza katika kifo" wataishi. (Isaya 26:19) Katika Biblia tukio hilo linaitwa ufufuo.

MPENDWA WETU AKIFA

4 Mtu wa familia au rafiki wa karibu akifa, tunalemewa na uchungu na huzuni. Tunahisi hatuna msaada. Hatuna uwezo wa kumrudishia uhai. Lakini tunaweza kupata faraja ya kweli katika Biblia. **(Soma 2 Wakorintho 1:3, 4.)** Acheni tuone mfano

---

1-3. Sote tumehukumiwa nini, na Yehova atatuweka huru jinsi gani?
4. (a) Tunaweza kupata wapi faraja mtu wa familia au rafiki akifa? (b) Baadhi ya rafiki za Yesu wa karibu walikuwa nani?

unaoonyesha kwamba Yehova na Yesu wanatamani kuwafufua wapendwa wetu. Yesu alipokuwa duniani, mara nyingi alimtembelea Lazaro na dada zake, Martha na Maria. Wote watatu walikuwa marafiki wazuri wa Yesu. Biblia inasema: "Yesu alimpenda Martha na dada yake na Lazaro." Lakini siku moja Lazaro alikufa.—Yohana 11:3-5.

5 Yesu alienda kuwafariji Martha na Maria. Martha aliposikia kwamba Yesu anakuja, alienda jijini kumpokea. Alifurahi kumwona Yesu, lakini akamwambia: "kama ungekuwa hapa ndugu yangu hangekufa." Martha alifikiri Yesu amechelewa. Kisha, Yesu akamwona Maria akilia. Alipoona huzuni yao aliumia moyoni naye akalia. (Yohana 11:21, 33, 35) Aliumia sana kama vile tunavyohisi tunapofiwa na mtu tunayempenda.

6 Tunafarijika tunapojua kwamba Yesu ana hisia kama zetu kuhusu kifo. Yesu ana sifa kama za Baba yake. (Yohana 14:9) Yehova ana uwezo wa kuondoa kifo na atafanya hivyo hivi karibuni.

"LAZARO, NJOO HUKU NJE!"

7 Yesu alipofika kwenye kaburi ambalo Lazaro alikuwa amezikwa, mwingilio ulikuwa umefunikwa na jiwe kubwa. Yesu akawaambia: "Liondoeni jiwe." Lakini Martha akapinga. Mwili wa Lazaro ulikuwa kaburini kwa siku nne. (Yohana 11:39) Hakujua kile

---

5, 6. (a) Yesu alifanya nini alipoona familia na marafiki wa Lazaro wakiomboleza? (b) Kwa nini inafariji kujua jinsi Yesu alivyohisi kuhusu kifo?

7, 8. Kwa nini Martha hakutaka jiwe liondolewe kwenye kaburi la Lazaro, lakini Yesu alifanya nini?

ambacho Yesu alitaka kufanya ili kumsaidia ndugu yake.

8 Yesu akamwambia Lazaro: "Njoo huku nje!" Martha na Maria walishangaa sana. "Huyo mtu aliyekuwa mfu akatoka miguu na mikono yake ikiwa imefungwa vitambaa." (Yohana 11:43, 44) Lazaro akawa hai tena! Aliungana tena na familia na rafiki zake. Wangeweza kumkumbatia, kumshika, na kuzungumza naye. Huo ulikuwa muujiza mkubwa sana! Yesu alikuwa amemfufua Lazaro.

'MSICHANA MDOGO, INUKA!'

9 Je, Yesu aliwafufua wafu kwa nguvu zake? Hapana. Yesu alimwomba Yehova ampe nguvu kabla ya kumfufua Lazaro. **(Soma Yohana 11:41, 42.)** Si Lazaro pekee aliyefufuliwa. Biblia inatueleza kuhusu msichana mwenye umri wa miaka 12 aliyekuwa mgonjwa sana. Baba yake, Yairo, alikuwa amekata tamaa, akamsihi Yesu amponye. Alikuwa mtoto wake pekee. Alipokuwa akizungumza na Yesu, wanaume fulani walikuja na kusema: "Binti yako amekufa! Kwa nini uendelee kumsumbua mwalimu?" Lakini Yesu akamwambia Yairo: "Usiogope, uwe tu na imani, naye ataokolewa." Kisha wakaenda nyumbani kwa Yairo. Walipokuwa wakikaribia nyumbani kwa Yairo, Yesu aliona na akasikia watu wakilia. Yesu akawaambia: "Acheni kulia, kwa maana hakufa bali analala usingizi." Lazima wazazi wa binti huyo walishangazwa sana na maneno ya Yesu. Yesu akaamuru

9, 10. (a) Ni nani aliyempa Yesu nguvu za kufufua wafu? (b) Kwa nini masimulizi ya ufufuo ni muhimu sana kwetu?

watu wote waondoke kisha akawachukua wazazi wa binti hadi mahali binti alipolazwa, akamshika mkono na kumwita, akisema: "Msichana, inuka!" Wazia shangwe waliyohisi wazazi wake mara alipoinuka na kuanza kutembea! Yesu alikuwa amemfufua binti yao. (Marko 5:22-24, 35-42; Luka 8:49-56) Kuanzia wakati huo na kuendelea kila walipomtazama binti yao, wangekumbuka jambo ambalo Yehova aliwatendea kupitia Yesu.*

10 Watu ambao Yesu aliwafufua walikufa tena baadaye. Lakini mambo tunayosoma kuwahusu ni muhimu sana kwetu kwa sababu yanatupa tumaini hakika. Yehova anatamani kuwafufua watu na atafanya hivyo.


MAMBO TUNAYOJIFUNZA KUTOKANA NA MASIMULIZI YA UFUFUO

11 Biblia inasema waziwazi kwamba "wafu hawajui lolote kamwe." Kifo cha Lazaro kilithibitisha ukweli huo. (Mhubiri 9:5) Kama Yesu alivyosema, ilikuwa kana kwamba Lazaro alikuwa amelala usingizi tu. (Yohana 11:11) Alipokuwa kaburini Lazaro hakujua "lolote kamwe."

12 Yesu alimfufua Lazaro mbele ya watu wengi. Hata maadui wa Yesu walijua kwamba alifanya

* Katika masimulizi mengine, Biblia inatueleza kuhusu ufufuo wa vijana na watu wazima, wanaume na wanawake, Waisraeli na wakaaji wageni. Unaweza kusoma masimulizi hayo katika 1 Wafalme 17:17-24; 2 Wafalme 4:32-37; 13:20, 21; Mathayo 28:5-7; Luka 7:11-17; 8:40-56; Matendo 9:36-42; 20:7-12.

11. Kifo cha Lazaro kinathibitishaje ukweli wa andiko la Mhubiri 9:5?
12. Tunajuaje kwamba ufufuo wa Lazaro ulitukia?



Eliya alimfufua mwana wa mjane.—1 Wafalme 17:17-24

Mtume Petro alimfufua mwanamke Mkristo Dorkasi. —Matendo 9:36-42

Wazia shangwe waliyohisi familia ya Lazaro alipofufuliwa! —Yohana 11:38-44

muujiza huo. Lazaro alikuwa hai tena na hilo lilithibitisha waziwazi kwamba ufufuo huo ulitukia. (Yohana 11:47) Pia, watu wengi walimtembelea Lazaro nao wakaanza kuamini kwamba Yesu alitumwa na Mungu. Jambo hilo liliwachukiza adui za Yesu, hivyo wakapanga kumuua Yesu na Lazaro.—Yohana 11:53; 12:9-11.

13 Yesu alisema kwamba "wale wote walio katika makaburi ya ukumbusho" watafufuliwa. (Yohana 5: 28) Jambo hilo linamaanisha kwamba watu wote ambao Yehova anawakumbuka watafufuka. Lakini ili Yehova amfufue mtu, anahitaji kukumbuka kila kitu kuhusu mtu huyo. Je, kweli anaweza kukumbuka? Kuna mabilioni ya nyota angani. Biblia inasema kwamba Yehova anajua majina ya nyota hizo zote. **(Soma Isaya 40:26.)** Kama anaweza kukumbuka jina la kila nyota, ni wazi kwamba atakumbuka kwa urahisi kila kitu kuhusu wale ambao atawafufua. Zaidi ya yote, Yehova aliumba kila kitu, kwa hiyo tuna uhakika kwamba ana uwezo wa kuwafufua wafu.

14 Ayubu, aliyekuwa mwaminifu, aliamini ufufuo. Aliuliza hivi: "Mtu akifa, je, anaweza kuishi tena?" Kisha akamwambia Yehova: "Wewe utaita, na mimi mwenyewe nitakujibu. Kwa kuwa utaitamani sana kazi ya mikono yako." Kwa kweli, Ayubu alijua kwamba Yehova amepanga wakati ambao atawafufua wafu.—Ayubu 14:13-15.

15 Unahisije kuhusu tumaini la ufufuo? Huenda ukajiuliza, 'Je, ndugu na rafiki zangu waliokufa wata-

---

13. Kwa nini tuwe na uhakika kwamba Yehova atawafufua wafu?
14, 15. Tunajifunza nini kutokana na maneno ya Ayubu kuhusu ufufuo?

fufuliwa?' Tunafarijika kujua kwamba Yehova anatamani sana kuwafufua wafu. Acheni tuchunguze jinsi Biblia inavyosema kuhusu wale watakaofufuliwa na mahali watakapoishi.

"WATAISIKIA SAUTI YAKE NA KUTOKA"

16 Zamani, wale ambao walifufuliwa waliungana na familia na marafiki zao tena duniani. Jambo hilo litatukia pia wakati ujao, lakini kwa njia bora hata zaidi. Kwa nini? Kwa sababu wale watakaofufuliwa watapata nafasi ya kuishi milele duniani na hawatakufa tena kamwe. Pia wataishi katika dunia iliyo tofauti sana na leo. Hakutakuwa vita, uhalifu, na magonjwa.

17 Ni nani watakaofufuliwa? Yesu alisema kwamba "wale **wote** waliomo ndani ya makaburi ya ukumbusho wataisikia sauti yake na kutoka." (Yohana 5:28, 29) Pia, andiko la Ufunuo 20:13 linasema: "Na bahari ikawatoa wale wafu waliokuwa ndani yake, na kifo na Kaburi vikawatoa wale wafu waliokuwa ndani yake." Ndiyo, mabilioni ya watu watakuwa hai tena. Mtume Paulo alisema kwamba "waadilifu na wasio waadilifu" watafufuliwa. **(Soma Matendo 24:15.)** Alimaanisha nini?

18 "Waadilifu" wanatia ndani watumishi waaminifu wa Yehova walioishi kabla ya Yesu kuja duniani. Watu kama Noa, Abrahamu, Sara, Musa, Ruthu, na Esta watafufuliwa waishi hapa duniani. Unaweza kusoma kuhusu baadhi ya wanaume na wanawake hao katika Waebrania sura ya 11. Vipi kuhusu watumishi

16. Wale watakaofufuliwa wataishi maisha ya aina gani?
17. Ni nani watakaofufuliwa?
18. "Waadilifu" watakaofufuliwa ni nani?

waaminifu wa Yehova wanaokufa katika siku zetu? Wao pia ni “waadilifu,” kwa hiyo watafufuliwa.

Katika Paradiso, wafu watafufuliwa na kuungana na wapendwa wao



19 "Wasio waadilifu" ni mabilioni ya watu ambao hawakupata fursa ya kujifunza kumhusu Yehova. Ingawa walikufa, Yehova hajawasahau. Atawafufua, na kuwapa fursa ya kujifunza kumhusu na kumtumikia.

20 Je, hilo linamaanisha kwamba kila mtu aliyekufa atafufuliwa? Hapana. Yesu alisema kwamba baadhi ya watu hawatafufuliwa. (Luka 12:5) Ni nani atakayeamua ikiwa mtu anastahili kufufuliwa au la? Yehova ndiye mwamuzi mkuu, lakini amempa pia Yesu mamlaka ya "kuwa mwamuzi wa walio hai na wafu." (Matendo 10:42) Wote watakaohukumiwa kuwa waovu hatafufuliwa.—Soma Maelezo ya Ziada 19.

WANAOFUFULIWA KWENDA MBINGUNI

21 Biblia inatuambia pia kwamba baadhi ya watu wataishi mbinguni. Watu wanaofufuliwa kwenda mbinguni, hawafufuliwi na mwili wa nyama. Wanafufuliwa wakaishi mbinguni wakiwa na mwili wa roho.

22 Yesu alikuwa mwanadamu wa kwanza kupata ufufuo huo. (Yohana 3:13) Yehova alimfufua Yesu siku tatu baada ya kifo chake. (Zaburi 16:10; Matendo13:34, 35) Yesu hakufufuliwa akiwa na mwili wa kibinadamu. Mtume Petro anaeleza kwamba "aliuawa katika mwili, lakini akafanywa kuwa hai katika roho." (1 Petro 3:18) Yesu alifufuliwa akiwa mtu wa roho

---

19. "Wasio waadilifu" ni nani? Yehova atawapa fursa gani?
20. Kwa nini si watu wote watakaofufuliwa?
21, 22. (a) Wale watakaofufuliwa kwenda mbinguni watakuwa na mwili gani? (b) Ni nani aliyekuwa wa kwanza kupata ufufuo wa mbinguni?

mwenye nguvu! (1 Wakorintho 15:3-6) Hata hivyo, Biblia inasema kwamba hatakuwa peke yake.

23 Kabla ya kifo chake, Yesu aliwaambia hivi wanafunzi wake waaminifu: "Ninaenda kuwatayarishia ninyi mahali." (Yohana 14:2) Jambo hilo linamaanisha kwamba baadhi ya wafuasi wake wangefufuliwa ili waishi pamoja naye mbinguni. Idadi yao ni ngapi? Yesu alisema kwamba wangekuwa wachache tu, "kundi dogo." (Luka 12:32) Mtume Yohana aliona idadi kamili alipomwona Yesu "amesimama juu ya Mlima Sayuni [mbinguni], na pamoja naye 144,000." —Ufunuo 14:1.

24 Wakristo 144,000 walianza kufufuliwa lini? Biblia inaeleza kwamba ufufuo huo ungeanza baada ya Yesu kuanza kutawala mbinguni. (1 Wakorintho 15:23) Sasa tunaishi katika kipindi hicho, wengi kati ya hao 144,000 tayari wamefufuliwa kwenda mbinguni. Wale waliobaki duniani hufufuliwa mara tu baada ya kufa ili wakaishi mbinguni. Hata hivyo, watu wengi watafufuliwa wakati ujao ili waishi katika Paradiso duniani.

25 Hivi karibuni, Yehova atawaweka huru wanadamu wote kutokana na kifo wala hakitakuwapo tena! **(Soma Isaya 25:8.)** Hata hivyo, wale wanaofufuliwa kwenda mbinguni watafanya nini huko? Biblia inaeleza kwamba watatawala pamoja na Yesu katika Ufalme wa Mungu. Tutajifunza mengi kuhusu ufalme huo katika sura inayofuata.

23, 24. "Kundi dogo" ambalo Yesu alizungumzia ni nani na ni wangapi?

25. Tutajifunza nini katika sura inayofuata?

UKWELI WA 1 YEHOVA ATAONDOA KIFO

"Adui wa mwisho atakayeangamizwa ni kifo."
—1 Wakorintho 15:26

Biblia inaweza kutufariji jinsi gani tunapofiwa?

2 Wakorintho 1:3, 4
Tunaweza kuvunjika moyo, mtu wa familia au rafiki mpendwa anapokufa. Lakini Biblia inatupatia faraja.

Isaya 25:8; 26:19
Yehova ana uwezo wa kuondoa kifo milele. Pia, atawafufua wale waliokufa.

UKWELI WA 2 TUNAWEZA KUAMINI UFUFUO

"Mwanamwali, ninakuambia, Simama!"—Marko 5:41

Kwa nini tunaweza kuamini ufufuo?

Yohana 11:1-44
Yesu alimfufua Lazaro.

Marko 5:22-24, 35-42
Yesu alimfufua msichana mdogo.

Yohana 11:41, 42
Yesu aliwafufua wafu kwa kutumia nguvu za Yehova.

Yohana 12:9-11
Watu wengi walishuhudia Yesu alipowafufua wafu. Hata adui za Yesu walijua jambo hilo.

UKWELI WA 3 YEHOVA ATAFUFUA MABILIONI YA WAFU

"Wewe utaita, na mimi mwenyewe nitakujibu. Kwa kuwa utaitamani sana kazi ya mikono yako." —Ayubu 14:13-15

Ni nani watakaofufuliwa?

Yohana 5:28, 29
Wale wote walio katika kumbukumbu la Yehova watafufuliwa.

Matendo 24:15
Waadilifu na wasio waadilifu watafufuliwa.

Isaya 40:26
Yehova anaweza kukumbuka majina ya nyota zote, hivyo anaweza kukumbuka kila kitu kuhusu wale ambao atawafufua.

UKWELI WA 4 WENGINE WANAFUFULIWA WAKAISHI MBINGUNI

"Ninaenda kuwatayarishia ninyi mahali." —Yohana 14:2

Ni nani wanaofufuliwa wakaishi mbinguni?

1 Petro 3:18
Yesu alikuwa mtu wa kwanza kufufuliwa kwenda kuishi mbinguni.

Luka 12:32
Yesu alisema kwamba ni idadi ndogo tu ya wanafunzi wake ambao wangefufuliwa wakaishi mbinguni.

Ufunuo 14:1
Yehova amechagua jumla ya watu 144,000 wakaishi mbinguni.

UFALME WA MUNGU NI NINI?

MAMILIONI ya watu wanaijua ile sala maarufu ya Baba yetu au Sala ya Bwana. Yesu alitumia sala hii kuwafundisha wanafunzi wake jinsi ya kusali. Alisali kuhusu nini? Kwa nini sala hiyo ni muhimu kwetu leo?

2 Yesu alisema: "Basi, ninyi msali hivi: 'Baba yetu uliye mbinguni, jina lako na litakaswe. Ufalme wako na uje. Mapenzi yako na yatendeke duniani kama ilivyo mbinguni.' " **(Soma Mathayo 6:9-13.)** Kwa nini Yesu alitufundisha tusali kuhusu mambo hayo matatu?—Soma Maelezo ya Ziada 20.

3 Tumejifunza kwamba jina la Mungu ni Yehova. Pia tumejua kusudi la Mungu kwa wanadamu na dunia. Lakini Yesu alimaanisha nini aliposema: "Ufalme wako na uje"? Tutajifunza kuhusu Ufalme wa Mungu, mambo utakayotimiza, na jinsi utakavyolitakasa jina la Mungu.

UFALME WA MUNGU NI NINI?

4 Yehova amesimamisha serikali mbinguni na amemchagua Yesu kuwa Mfalme. Biblia inaiita serikali hiyo Ufalme wa Mungu. Yesu ni "Mfalme wa wale wanaotawala wakiwa wafalme na Bwana wa wale wanaotawala wakiwa mabwana." (1 Timotheo 6:15) Yesu

1. Tutazungumzia sala gani maarufu?
2. Yesu alitufundisha tusali kuhusu mambo gani matatu?
3. Tunahitaji kujua mambo gani kuhusu Ufalme wa Mungu?
4. Ufalme wa Mungu ni nini, na Mfalme wake ni nani?

ana nguvu za kufanya mambo mengi mazuri kwa ajili ya wanadamu kuliko mtawala **yeyote** wa wanadamu.

5 Yesu alirudi mbinguni siku arobaini baada ya kufufuliwa. Alichaguliwa na Yehova awe Mfalme wa Ufalme huo. (Matendo 2:33) Serikali ya Mungu itatawala dunia kutoka mbinguni. (Ufunuo 11:15) Ndiyo sababu Biblia inauita Ufalme wa Mungu 'Ufalme wa mbinguni.'—2 Timotheo 4:18.

6 Biblia inasema kwamba Yesu ni mkuu kuliko mwanadamu yeyote kwa sababu ni "yeye peke yake asiyeweza kufa." (1 Timotheo 6:16) Watawala wote wa kibinadamu hufa lakini Yesu hatakufa milele. Mambo mazuri ambayo Yesu atatufanyia yatadumu milele.

7 Unabii wa Biblia unasema kwamba Yesu atakuwa mfalme mwenye huruma na haki. Unabii huo unasema: "Roho ya Yehova itatua juu yake, roho ya hekima na ya uelewaji, roho ya shauri na ya nguvu, roho ya ujuzi na ya kumwogopa Yehova; naye atakuwa na shangwe katika kumwogopa Yehova. Na hatahukumu kulingana na sura inayoonekana kwa macho yake tu, wala kukaripia kulingana tu na jambo lililosikiwa na masikio yake. Naye atawahukumu kwa uadilifu watu wa hali ya chini." (Isaya 11:2-4) Je hungependa mfalme kama huyo?

8 Mungu amewachagua baadhi ya wanadamu watawale pamoja na Yesu huko mbinguni. Kwa mfano, mtume Paulo alimwambia Timotheo hivi: "Tukiendelea kuvumilia, tutatawala pamoja pia tukiwa wafal-

---

5. Serikali ya Mungu itatawala kutoka wapi? Itatawala nini?
6, 7. Kwa nini Yesu ni mfalme bora kuliko wafalme wa kibinadamu?
8. Tunajuaje kwamba Yesu hatatawala peke yake?

me." (2 Timotheo 2:12) Ni watu wangapi watatawala pamoja na Yesu?

9 Kama tulivyojifunza katika sura ya 7, mtume Yohana alimwona Yesu katika maono akiwa Mfalme pamoja na 144,000. Hao 144,000 ni nani? Yohana anaeleza kwamba 'jina la Yesu na jina la Baba yake limeandikwa juu ya mapaji ya nyuso zao.' Na akaongezea: "Hao ndio wale wanaoendelea kumfuata Mwana-Kondoo [Yesu] popote anapoenda. Walinunuliwa kutoka kati ya wanadamu." **(Soma Ufunuo 14:1, 4.)** Hao 144,000 ni Wakristo waaminifu ambao Mungu amewachagua "watawale wakiwa wafalme juu ya dunia" pamoja na Yesu. Wakifa wanafufuliwa na kwenda kuishi mbinguni. (Ufunuo 5:10) Yehova amekuwa akichagua Wakristo waaminifu ili kukamilisha kikundi hicho cha wafalme 144,000 tangu nyakati za mitume.

10 Yehova anatupenda sana ndiyo sababu amewachagua wanadamu watawale pamoja na Yesu. Yesu atakuwa mtawala mzuri kwa sababu anatujua vizuri. Anajua hali ya wanadamu na mateso wanayokabili. Paulo alisema kwamba Yesu anajua hisia zetu, anaweza "kuusikitikia udhaifu wetu," na "amejaribiwa katika mambo yote kama sisi." (Waebrania 4:15; 5:8) Hata wale 144,000 wanajua hali za wanadamu. Walikabiliana na hali ya kutokamilika na magonjwa. Kwa hiyo tunaweza kuwa na uhakika kabisa kwamba Yesu

---

9. Ni watu wangapi watakaotawala pamoja na Yesu? Mungu alianza kuwachagua lini?

10. Kuchaguliwa kwa Yesu na wale 144,000 kutawala dunia kunathibitishaje kwamba Yehova anatupenda?

pamoja na hao 144,000 wataelewa vizuri hisia na mahitaji yetu na kuyatatua.

UFALME WA MUNGU UTATIMIZA NINI?

11 Yesu aliwafundisha wanafunzi wake wasali mapenzi ya Mungu yatendeke mbinguni. Kwa nini? Katika sura ya 3 tulijifunza kwamba Shetani Ibilisi alimwasi Yehova. Baada ya kuasi Yehova aliruhusu Shetani na malaika walioasi wabaki kwa muda mbinguni. Kwa hiyo wakati huo si malaika wote waliokuwa mbinguni walifanya mapenzi ya Mungu. Katika sura ya 10, tutajifunza mengi kuhusu Shetani na malaika zake.

12 Biblia inasema kwamba baada ya Yesu kuwekwa kuwa Mfalme wa Ufalme wa Mungu, angepigana vita na Shetani. **(Soma Ufunuo 12:7-10.)** Mstari wa 10 unaeleza matukio mawili muhimu. Ufalme wa Mungu ungeanza kutawala Yesu akiwa Mfalme wa Ufalme huo, kisha Shetani angetupwa duniani kutoka mbinguni. Kama tutakavyojifunza, mambo hayo yamekwisha tukia.

13 Biblia inaelezea jinsi malaika waaminifu walivyofurahi baada ya Shetani na malaika zake kufukuzwa mbinguni. Tunasoma hivi: "Furahini, enyi mbingu nanyi mnaokaa ndani yake!" (Ufunuo 12:12) Sasa, mbinguni kuna amani na umoja kwa sababu malaika wote wanafanya mapenzi ya Mungu.

---

11. Kwa nini Yesu aliwafundisha wanafunzi wake wasali mapenzi ya Mungu yatendeke mbinguni?
12. Ni matukio gani mawili muhimu yanayoelezwa katika Ufunuo 12:10?
13. Ni nini kilichotokea baada ya Shetani kufukuzwa mbinguni?

14 Lakini hali duniani ni tofauti sana. Kuna mambo mengi mabaya "kwa sababu Ibilisi ameshuka" akiwa na "hasira kali, akijua kwamba ana kipindi kifupi cha wakati." (Ufunuo 12:12) Shetani ana hasira kali. Alifukuzwa mbinguni na anajua kwamba hivi karibuni ataharibiwa. Anafanya kila awezalo kusababisha matatizo, maumivu, na mateso ya kila aina.

15 Hata hivyo, kusudi la Mungu kwa dunia halijabadilika. Anapenda wanadamu waaminifu waishi milele katika dunia paradiso. (Zaburi 37:29) Ufalme wa Mungu utatimiza kusudi hilo jinsi gani?

16 Unabii wa Danieli 2:44 unasema: "Na katika siku za wafalme hao, Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaharibiwa kamwe. Na ufalme huo hautapewa watu wengine wowote. Utazivunja na kuzikomesha falme hizi zote, nao utasimama mpaka wakati usio na kipimo." Unabii huo unatufundisha nini kuhusu Ufalme wa Mungu?

17 Kwanza, unabii huo unaeleza kwamba Ufalme wa Mungu ungeanza kutawala "katika siku za wafalme hao." Jambo hilo linamaanisha kwamba serikali nyingine zingekuwa zikitawala wakati ambapo Ufalme wa Mungu ungeanza kutawala. Pili, unabii huo unaeleza kwamba Ufalme wa Mungu utadumu milele na hakuna serikali nyingine itakayochukua mahali pake. Tatu, kutakuwa na vita kati ya Ufalme wa Mungu na serikali za wanadamu. Ufalme wa Mungu

---

14. Hali zimekuwaje duniani baada ya Shetani kufukuzwa mbinguni?
15. Mungu ana kusudi gani kwa dunia?
16, 17. Andiko la Danieli 2:44 linatueleza nini kuhusu Ufalme wa Mungu?

utashinda na kuwa serikali pekee inayotawala dunia yote. Mwishowe wanadamu watakuwa na serikali bora ambayo hawajawahi kuwa nayo kamwe.

18 Ufalme wa Mungu utaziondoa jinsi gani serikali za wanadamu? Kabla ya vita vya mwisho, vinavyoitwa Har–Magedoni, mashetani watawapotosha "wafalme wa dunia nzima inayokaliwa, ili kuwakusanya pamoja kwa vita vya ile siku kuu ya Mungu Mweza-Yote." Serikali za wanadamu zitapigana na Ufalme wa Mungu.—Ufunuo 16:14, 16; Soma Maelezo ya Ziada 10.

19 Kwa nini tunahitaji Ufalme wa Mungu? Kuna sababu tatu. Kwanza, tunakuwa wagonjwa na kufa kwa sababu sisi ni wenye dhambi. Hata hivyo, Biblia inasema kwamba chini ya utawala wa Mungu, tutaishi milele. Andiko la Yohana 3:16 linasema: "Mungu aliupenda ulimwengu sana hivi kwamba akamtoa Mwana wake mzaliwa-pekee, ili kila mtu anayemwamini asiangamizwe bali awe na uzima wa milele."

20 Sababu ya pili ni kwamba tumezungukwa na watu waovu. Watu wengi si waaminifu, ni waongo, na wana maadili mabaya. Hatuwezi kuwaondoa, lakini Mungu atawaondoa. Watu wote wanaofanya mambo maovu wataangamizwa wakati wa Har–Magedoni. **(Soma Zaburi 37:10.)** Sababu ya tatu ni kwamba serikali za wanadamu ni dhaifu, katili, na zimejaa ufisadi. Serikali hizo haziwasaidii watu wamtii Mungu. Biblia inasema kwamba "mwanadamu amemtawala mwanadamu kwa kumuumiza."—Mhubiri 8:9.

---

18. Vita vya mwisho kati ya Ufalme wa Mungu na serikali za wanadamu inaitwaje?

19, 20. Kwa nini tunahitaji Ufalme wa Mungu utawale dunia?



Tangu Shetani na malaika zake wafukuzwe mbinguni, kumekuwa na mateso mengi duniani. Mateso hayo yatakoma hivi karibuni

21 Baada ya Har–Magedoni, Ufalme wa Mungu utahakikisha kwamba mapenzi ya Mungu yanatendeka duniani. Kwa mfano, Ufalme huo utamwangamiza Shetani na malaika zake. (Ufunuo 20:1-3) Hatimaye, hakutakuwa na magonjwa wala kifo. Fidia itawawezesha watu wote waaminifu kuishi milele katika Paradiso. (Ufunuo 22:1-3) Ufalme huo utalitakasa jina la Mungu. Hilo linamaanisha nini? Wanadamu wote watalitukuza jina la Yehova wakati ambapo Ufalme wa Mungu utaitawala dunia.—Soma Maelezo ya Ziada 21.

YESU ALIWEKWA KUWA MFALME LINI?

22 Yesu aliwafundisha wanafunzi wake wasali hivi: “Ufalme wako na uje.” Hivyo, ni wazi kwamba serikali ya Mungu ingeanza kutawala baadaye. Kwanza, Yehova angesimamisha serikali yake na kumweka Yesu kuwa Mfalme. Je, Yesu aliwekwa kuwa Mfalme mara tu aliporudi mbinguni? Hapana, alipaswa kusubi-

21. Ufalme utatimiza mapenzi ya Mungu duniani jinsi gani?
22. Tunajuaje kwamba Yesu hakuwekwa kuwa Mfalme alipokuwa duniani au mara tu alipofufuliwa?




Ufalme wa Mungu utahakikisha kwamba mapenzi ya Mungu yanatendeka duniani

ri. Muda mfupi baada ya kufufuliwa, Petro na Paulo walieleza jambo hilo waliponukuu unabii kumhusu Yesu ulio katika Zaburi 110:1. Katika unabii huo Yehova anasema: “Keti kwenye mkono wangu wa kuume, mpaka niwaweke adui zako kuwa kiti cha miguu yako.” (Matendo 2:32-35; Waebrania 10:12, 13) Yesu angewekwa na Yehova kuwa Mfalme lini?

23 Kwa miaka mingi, kikundi cha Wakristo waaminifu walijua kwamba mwaka wa 1914 ungekuwa mwaka muhimu katika utimizo wa unabii wa Biblia. Matukio ya ulimwengu tangu mwaka wa 1914 yanathibitisha kwamba walikuwa sahihi. Yesu alianza kutawala mwaka huo. (Zaburi 110:2) Baada tu ya Yesu kuanza kutawala, Shetani alitupwa duniani, na kwa sasa “ana kipindi kifupi cha wakati.” (Ufunuo 12:12) Katika sura inayofuata, tutaona uthibitisho zaidi unaoonyesha kwamba tunaishi katika kipindi hicho cha wakati. Pia, tutajifunza kwamba hivi karibuni Ufalme wa Mungu utafanya mapenzi ya Mungu yatendeke duniani.—Soma Maelezo ya Ziada 22.

23. (a) Yesu alianza kutawala lini akiwa Mfalme wa serikali ya Mungu? (b) Tutajifunza nini katika sura inayofuata?



UKWELI WA 1 UFALME WA MUNGU NI SERIKALI HALISI

"Ufalme wako na uje. Mapenzi yako na yatendeke duniani kama ilivyo mbinguni."—Mathayo 6:9-13

Ufalme wa Mungu nini?

Ufunuo 11:15
Ufalme au serikali ya Mungu, utaitawala duniani kutoka mbinguni.

1 Timotheo 6:15
Yesu ndiye Mfalme wa Ufalme wa Mungu.

Ufunuo 14:1, 4
Watu 144,000 watatawala na Yesu wakiwa mbinguni.

Waebrania 4:15; 5:8
Yesu na wale 144,000 wanaelewa hisia zetu na matatizo tunayokabili.

UKWELI WA 2 YESU ATAKUWA MTAWALA BORA

"Atawahukumu kwa uadilifu watu wa hali ya chini [au maskini]."—Isaya 11:4

Kwa nini Yesu anastahili kuwa Mfalme wa Ufalme wa Mungu?

1 Timotheo 6:16
Watawala wa wanadamu hufa, lakini Yesu hatakufa kamwe. Mambo yote mazuri ambayo Yesu atafanya kwa ajili Yetu yatadumu milele.

Isaya 11:2-4
Yesu anaweza kufanya mambo mazuri zaidi ya wanadamu. Ana nguvu kuliko watawala wote wa wanadamu hata wakiungana. Yeye ni mwenye haki na huruma.

UKWELI WA 3 UFALME WA MUNGU UTAHAKIKISHA KWAMBA MAPENZI YA MUNGU YANATENDEKA

"Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaharibiwa kamwe."—Danieli 2:44

Ni mambo gani ambayo tayari Ufalme wa Mungu umefanya?
Utafanya nini wakati ujao?

Ufunuo 12:7-12
Yesu alipowekwa rasmi kuwa Mfalme mbinguni mwaka wa 1914, alimtupa Shetani duniani. Hiyo ndiyo sababu kuna matatizo, maumivu na mateso mengi duniani.

Mhubiri 8:9;
Ufunuo 16:16
Katika vita vya Har–Magedoni, Ufalme wa Mungu utaziharibu serikali zote za wanadamu zilizojaa ukatili na ufisadi.

Zaburi 37:10
Watu wanaotenda maovu wataharibiwa.

Ufunuo 22:1-3
Ufalme wa Mungu utakapoitawala dunia, hakuna atakayekuwa mgonjwa au kufa na wanadamu wote watalisifu jina la Mungu.

JE MWISHO WA DUNIA UKO KARIBU?

JE UMEWAHI kusikiliza taarifa ya habari na ukajiuliza hivi, 'Kwa nini mambo yanazidi kuwa mabaya?' Dunia imejaa majanga na ukatili unaofanya baadhi ya watu waamini kwamba lazima mwisho wa dunia uwe karibu sana. Je, kweli mwisho uko karibu? Je, kuna njia yoyote ya kujua jambo hilo? Bila shaka. Wanadamu hawawezi kutabiri mambo ya wakati ujao. Ni Yehova Mungu pekee anayeweza kutabiri. Katika Biblia, anatueleza kuhusu wakati ujao wa dunia na wanadamu. —Isaya 46:10; Yakobo 4:14.

2 Mwisho wa dunia unaotajwa katika Biblia, unamaanisha mwisho wa uovu wala si kuharibiwa kwa sayari yetu dunia. Yesu aliwafundisha watu kwamba Ufalme wa Mungu utaitawala dunia. (Luka 4:43) Wanafunzi wa Yesu walitamani kujua ni lini Ufalme wa Mungu ungekuja, nao walimuuliza Yesu hivi: "Mambo haya yatakuwa wakati gani, na ni nini itakayokuwa ishara ya kuwapo kwako na ya umalizio wa mfumo wa mambo?" (Mathayo 24:3) Yesu hakutaja siku hususa, lakini aliwaeleza mambo ambayo yangetukia kabla ya mwisho wa dunia. Mambo ambayo Yesu alitabiri yanatukia katika siku zetu.

3 Katika sura hii tutachunguza mambo yanayothibitisha kwamba tunaishi katika siku za mwisho. Kwanza, tunahitaji kujifunza kuhusu vita iliyotokea mbingu-

1. Ni nani anayeweza kutabiri mambo ya wakati ujao?
2, 3. Wanafunzi wa Yesu walitamani kujua nini, na Yesu aliwaambia nini?

ni, ambayo imesababisha mambo yawe mabaya duniani.

VITA MBINGUNI

4 Katika sura ya 8 tulijifunza kwamba Yesu aliwekwa rasmi kuwa Mfalme mbinguni mwaka 1914. (Danieli 7:13, 14) Kitabu cha Ufunuo kinasimulia mambo yaliyotokea: "Vita vikatokea ghafula mbinguni: Mikaeli [Yesu] na malaika zake wakapigana na yule joka mkubwa [Shetani], naye joka mkubwa na malaika zake wakapigana."* Shetani na malaika zake walishindwa nao wakatupwa duniani. Hebu wazia jinsi malaika walivyoshangilia! Lakini namna gani kuhusu wanadamu duniani? Biblia inasema kwamba hicho kingekuwa kipindi cha taabu kwa wanadamu. Kwa nini? Kwa sababu Ibilisi ana hasira kali, "akijua kwamba ana kipindi kifupi cha wakati."—Ufunuo 12:7, 9, 12.

5 Ibilisi amesababisha matatizo mengi duniani. Ana hasira kali kwa sababu ana kipindi kifupi cha wakati kabla Mungu hajamwangamiza. Acheni sasa tuchunguze mambo ambayo Yesu alisema yangetukia katika siku za mwisho.—Soma Maelezo ya Ziada 24.

SIKU ZA MWISHO

6 Vita. Yesu alisema: "Taifa litasimama kupigana na taifa na ufalme kupigana na ufalme." (Mathayo 24:7)

* Mikaeli ni jina lingine la Yesu. Kwa maelezo zaidi, soma Maelezo ya Ziada 23.

4, 5. (a) Ni jambo gani lililotukia mbinguni baada ya Yesu kuwa Mfalme? (b) Kulingana na Ufunuo 12:12, ni jambo gani lingetukia baada ya Shetani kutupwa duniani?

6, 7. Vita na njaa vimesababisha nini ulimwenguni?

Katika siku zetu watu wengi wamekufa vitani kuliko wakati mwingine wowote katika historia. Ripoti moja ya shirika la Worldwatch inasema kwamba watu zaidi ya milioni mia moja wameuawa vitani tangu mwaka wa 1914. Idadi ya watu waliouawa vitani kwa miaka mia moja tangu mwaka wa 1900 hadi 2000 ni mara tatu zaidi ya idadi ya watu waliouawa kabla ya mwaka wa 1900. Hebu wazia uchungu na mateso ambayo watu wengi wamepata kutokana na vita!

7 Njaa. Yesu alisema: "Kutakuwa na upungufu wa chakula." (Mathayo 24:7) Ingawa mazao ya chakula yanakuzwa kwa wingi kuliko zamani, watu wengi hawapati chakula cha kutosha. Kwa nini? Kwa sababu hawana pesa za kutosha kununua chakula au mashamba ya kukuza chakula. Zaidi ya watu bilioni moja ulimwenguni ni maskini hohehahe. Shirika la afya ulimwenguni linasema kwamba mamilioni ya watoto hufa kila mwaka kwa sababu ya utapiamlo.





8 Matetemeko ya Nchi. Yesu alitabiri hivi: “kutakuwa na matetemeko makubwa ya nchi.” (Luka 21:11) Matetemeko makubwa ya ardhi hutokea kila mwaka. Tangu mwaka 1900, zaidi ya watu milioni mbili wamekufa kwa sababu ya matetemeko. Ingawa teknolojia imesaidia kugundua matetemeko kabla ya kutokea, bado matetemeko yameua watu wengi.

9 Magonjwa. Yesu alitabiri kwamba kungekuwa na “tauni.” Magonjwa hatari yanaenea kwa haraka na kuua watu wengi. (Luka 21:11) Ingawa madaktari wamejifunza kutibu magonjwa mengi, bado kuna baadhi ya magonjwa ambayo hayatibiki. Ripoti moja inasema kwamba kila mwaka watu wengi wanakufa kutokana na magonjwa kama vile kifua kikuu, malaria, na kipindupindu. Zaidi ya hayo, madaktari wamegundua magonjwa mapya zaidi ya 30 na baadhi ya magonjwa hayo hayana tiba.

8, 9. Ni mambo gani yanayoonyesha kwamba unabii wa Yesu kuhusu matetemeko na magonjwa unatimia?

WATU WA SIKU ZA MWISHO

10 Andiko la 2 Timotheo 3:1-5 linasema hivi: "Katika siku za mwisho kutakuwa na nyakati za hatari zilizo ngumu kushughulika nazo." Mtume Paulo alieleza jinsi ambavyo watu wengi wangejiendesha katika siku za mwisho. Alisema watu wangekuwa

- wenye kujipenda wenyewe
- wenye kupenda pesa
- wasiotii wazazi
- wasio washikamanifu
- wasio na upendo wa asili
- wasiojizuia
- wakali
- wanaopenda raha badala ya kumpenda Mungu
- wakiwa na namna ya ujitoaji-kimungu lakini wakizikana nguvu zake



11 Je, hivyo ndivyo watu walivyo katika eneo unaloishi? Hali iko hivyo ulimwenguni pote. Lakini, hivi karibuni Mungu atawaondoa watu hao. Anaahidi hivi: "Wakati waovu wanapochi-

---

10. Unabii wa 2 Timotheo 3:1-5 unatimiaje leo?
11. Kulingana na Zaburi 92:7, ni jambo gani litakalowapata watu waovu?

puka kama majani, na wote wanaotenda mambo yenye kuumiza wanapochanuka, ni ili wao wapate kuangamizwa [au,kuharibiwa] milele."—Zaburi 92:7.

HABARI NJEMA KATIKA SIKU ZA MWISHO

12 Biblia ilitabiri kwamba katika siku za mwisho, ulimwengu mzima ungejaa maumivu na mateso. Lakini pia inasema kuhusu mambo mazuri ambayo yangetukia.

13 Uelewaji wa Biblia. Nabii Danieli alitabiri kuhusu siku za mwisho. Aliandika hivi: "Ujuzi wa kweli utakuwa mwingi." (Danieli 12:4) Mungu angewasaidia watu wake waielewe Biblia vizuri zaidi kuliko ilivyokuwa zamani. Yehova amefanya hivyo hasa tangu mwaka 1914. Kwa mfano, ametufundisha jina lake, kusudi lake kwa dunia, ukweli kuhusu fidia, hali ya wafu, na tumaini la ufufuo. Tumejifunza kwamba ni Ufalme wa Mungu pekee unaoweza kusuluhisha matatizo yetu. Pia, tumejifunza jinsi ya kuwa na furaha na tunavyoweza kumpendeza Mungu katika maisha yetu. Hata hivyo, watumishi wa Mungu wanatumia jinsi gani mambo wanayojifunza? Unabii mwingine utatusaidia kupata jibu.—Soma Maelezo ya Ziada 21 na 25.

14 Kazi ya kuhubiri ulimwenguni pote. Alipokuwa akizungumzia siku za mwisho, Yesu alisema hivi: "Habari njema ya Ufalme itahubiriwa katika dunia yote." (Mathayo 24:3, 14) Habari njema ya Ufalme inahubiriwa katika lugha zaidi ya 700 katika nchi zaidi ya 230. Naam, ulimwenguni pote, Mashahidi wa Yehova

---

12, 13. Yehova ametufundisha mambo gani katika siku za mwisho?
14. Habari njema ya Ufalme inahubiriwa katika nchi na lugha ngapi, na ni nani wanaoihubiri?

kutoka "mataifa yote na makabila" wanawasaidia watu kuuelewa Ufalme wa Mungu na mambo utakayofanya kwa ajili ya wanadamu. (Ufunuo 7:9) Wanafanya kazi hiyo bila malipo. Ingawa wanapingwa na kuteswa na watu wengi, hakuna kitu kitakachozuia kazi ya kuhubiri kama Yesu alivyotabiri.—Luka 21:17.

UTAFANYA NINI?

15 Je, unaamini kwamba tunaishi katika siku za mwisho? Unabii mwingi unaohusu siku za mwisho umetimia. Hivi karibuni Yehova atasimamisha kazi ya kuhubiri, na "mwisho" utakuja. (Mathayo 24:14) Mwisho ni nini? Mwisho unamaanisha vita vya Har–Magedoni, Mungu atakapowaangamiza watu waovu. Yehova atamtumia Yesu na malaika zake wenye nguvu kuwaangamiza watu wote wasiomtii Yeye na Mwana wake. (2 Wathesalonike 1:6-9) Hatimaye, Shetani na mashetani wake hatawadanganya tena wanadamu. Wale wote wanaomtii Mungu na kuukubali Ufalme wake wataona utimizo wa unabii wote uliotolewa na Mungu.—Ufunuo 20:1-3; 21:3-5.

16 Hivi karibuni, Ulimwengu huu unaotawaliwa na Shetani utaharibiwa. Kwa hiyo, ni muhimu ujiulize hivi, 'Ninahitaji kufanya nini?' Yehova anataka uendelee kujifunza Biblia. Usipuuze kujifunza Biblia. (Yohana 17:3) Kila juma, Mashahidi wa Yehova huhudhuria mikutano inayowasaidia watu kuielewa Biblia. Jitahidi kuhudhuria mikutano hiyo. **(Soma Waebrania 10:24, 25.)** Unapojua kwamba unahitaji kufanya mabadiliko,

---

15. (a) Je, unaamini kwamba tunaishi katika siku za mwisho, kwa nini? (b) Ni nini kitakachowapata wale wasiomtii Mungu? (c) Wale wanaomtii Mungu wataona nini?
16. Kwa kuwa mwisho upo karibu, unahitaji kufanya nini?

"Habari njema ya ufalme itahubiriwa katika dunia yote inayokaliwa."
—Mathayo 24:14



usisite kuyafanya. Unapofanya hivyo uhusiano wako na Yehova unaimarika.—Yakobo 4:8.

17 Mtume Paulo alieleza kwamba uharibifu wa waovu utakuja bila kutarajiwa "kama mwizi usiku." (1 Wathesalonike 5:2) Yesu alitabiri kuwa watu wengi wangepuuza uthibitisho wa kwamba tunaishi katika siku za mwisho. Alisema hivi: "Kama vile siku za Noa zilivyokuwa, ndivyo kuwapo kwa Mwana wa binadamu [au, siku za mwisho] kutakavyokuwa. Kwa maana kama vile walivyokuwa katika siku hizo kabla ya gharika, wakila na kunywa, wanaume wakioa na wanawake wakiolewa, mpaka siku ambayo Noa aliingia ndani ya safina; nao hawakujali mpaka gharika ikaja na kuwafagilia mbali wote, ndivyo kuwapo kwa Mwana wa binadamu kutakavyokuwa."—Mathayo 24:37-39.

18 Yesu alionya kwamba hatupaswi kukengeushwa "na kula kupita kiasi na kunywa sana na mahangaiko ya maisha." Alisema kwamba mwisho utakuja ghafla, "kama mtego." Pia, alisema siku hiyo "itakuja juu ya wale wote wanaokaa juu ya uso wa dunia yote." Halafu akaendelea kusema hivi: "Basi, endeleeni kukesha wakati wote mkiomba dua [au, mkisali kwa unyofu] ili mpate kufanikiwa kuponyoka mambo yote hayo yaliyokusudiwa kutukia, na kusimama mbele ya Mwana wa binadamu." (Luka 21:34-36) Kwa nini inafaa kutii onyo la Yesu? Kwa sababu ulimwengu mwovu wa Shetani utaharibiwa hivi karibuni. Ni wale tu walio na kibali cha Yehova na Yesu watakaookolewa na kuishi milele katika ulimwengu mpya.—Yohana 3:16; 2 Petro 3:13.

17. Kwa nini watu wengi watashtuka mwisho utakapokuja?
18. Yesu alitoa onyo gani kwetu?

UKWELI WA 1 YEHOVA AMETUJULISHA KUHUSU WAKATI UJAO

"Anayetangaza tangu mwanzo ule mwisho, na kutoka zamani za kale mambo ambayo hayajafanywa."—Isaya 46:10

Tunajua nini kuhusu siku za mwisho?

Danieli 7:13, 14
Yesu aliwekwa rasmi kuwa mbinguni mwaka wa 1914.

Mathayo 24:3-14
Yesu alitabiri wakati ambapo hali zingekuwa ngumu.

Ufunuo 12:7-9, 12
Muda mfupi baada ya Yesu kuwekwa rasmi kuwa Mfalme, alimtupa Shetani duniani.
Shetani ana hasira kali kwa sababu anajua ana "kipindi kifupi cha wakati" kabla Mungu hajamwangamiza.

UKWELI WA 2 TUNAISHI KATIKA SIKU ZA MWISHO

"Ni nini itakayokuwa ishara ya . . . umalizio wa mfumo wa mambo?"—Mathayo 24:3

Je, umejionea utimizo wa unabii wa Biblia?

Mathayo 24:7; Luka 21:11
Zaidi ya wakati mwingine wowote, tumeshuhudia vita, njaa, matetemeko na magonjwa.

2 Timotheo 3:1-5
Mtume Paulo alisema kuhusu tabia za watu wa siku za mwisho.

Danieli 12:4
Mungu anawasaidia watu wake kuilewa Biblia zaidi kuliko wakati mwingine wowote.

Mathayo 24:14
Habari njema ya Ufalme itahubiriwa duniani kote.

UKWELI WA 3 CHUKUA HATUA SASA ILI KUMPENDEZA YEHOVA

"Siku ya Yehova inakuja sawasawa kabisa kama mwizi usiku."—1 Wathesalonike 5:2

Kwa kuwa mwisho uko karibu sana, unapaswa kufanya nini?

Yohana 17:3
Jifunze Biblia kwa bidii.

Waebrania 10:24, 25
Jifunze mengi zaidi kwa kuhudhuria mikutano ya Mashahidi wa Yehova.

Yakobo 4:8
Fanya marekebisho yanayohitajika katika maisha yako ili umkaribie Mungu zaidi.

Luka 21:34-36
Epuka mahangaiko, na utumie maisha yako kumwabudu Yehova.

UKWELI KUHUSU MALAIKA

YEHOVA anataka tuijue familia yake. Malaika ni sehemu ya familia yake. Katika Biblia huitwa "wana wa Mungu." (Ayubu 38:7) Malaika hufanya kazi gani? Waliwasaidia watu jinsi gani wakati uliopita? Je, wanaweza kutusaidia?—Soma Maelezo ya Ziada 8.

2 Malaika walitoka wapi? Andiko la Wakolosai 1:16 linasema kwamba baada ya Yehova kumuumba Yesu, ndipo "vitu vingine vyote viliumbwa mbinguni na duniani." Malaika pia waliumbwa. Ni malaika wangapi waliumbwa? Biblia inasema kwamba ni mamilioni ya malaika.—Zaburi 103:20; Ufunuo 5:11.

3 Pia, Biblia inafundisha kwamba Yehova aliwaumba malaika kabla ya kuumba dunia. Malaika walihisije dunia ilipoumbwa? Kitabu cha Biblia cha Ayubu kinasema kwamba walishangilia. Walikuwa familia iliyomtumikia Yehova kwa umoja.—Ayubu 38:4-7.

MALAIKA HUWASAIDIA WATU WA MUNGU

4 Sikuzote malaika hupendezwa na wanadamu na kusudi la Yehova kwa dunia. (Methali 8:30, 31; 1 Petro 1:11, 12) Ni wazi kwamba walihuzunika sana Adamu na Hawa walipomwasi Mungu. Wanahuzunika hata zaidi wanapowaona wanadamu wengi wakikataa kumtii Mungu. Hata hivyo, malaika hushangilia mtu

1. Kwa nini tujifunze kuhusu malaika?
2. Malaika walitoka wapi? Mungu aliumba malaika wangapi?
3. Andiko la Ayubu 38:4-7 linasema nini kuhusu malaika?
4. Tunajua jinsi gani kwamba malaika hupendezwa na wanadamu?

mmoja anapotubu na kumrudia Mungu. (Luka 15:10) Malaika wanapendezwa sana na wale wanaomtumikia Mungu. Yehova huwatumia malaika kuwasaidia na kuwalinda watumishi wake duniani. (Waebrania 1: 7, 14) Acheni tuchunguze baadhi ya mifano.

5 Yehova aliwatuma malaika wawili wamsaidie Loti na familia yake kuokoka uharibifu wa majiji ya So-

5. Malaika waliwasaidiaje watumishi wa Mungu nyakati za kale?

"Mungu wangu mwenyewe alimtuma malaika wake na kufunga vinywa vya simba."
—Danieli 6:22.



doma na Gomora. (Mwanzo 19:15, 16) Miaka mingi baadaye, nabii Danieli alitupwa katika shimo la simba, lakini hawakumshambulia kwa sababu "Mungu alimtuma malaika wake na kufunga vinywa vya simba." (Danieli 6:22) Baadaye, mtume Petro alipokuwa gerezani, Yehova alimtuma malaika ili kumweka huru. (Matendo 12:6-11) Pia, malaika walimsaidia Yesu alipokuwa duniani. Kwa mfano, baada ya kubatizwa, "malaika walikuwa wakimhudumia." (Marko 1: 13) Muda mfupi kabla ya Yesu kuuawa, malaika 'alimtia nguvu.'—Luka 22:43.

6 Leo, malaika hawawatokei wanadamu. Hata hivyo, bado Mungu anawatumia malaika kuwasaidia watumishi wake. Biblia inasema hivi: "Malaika wa Yehova anapiga kambi pande zote kuwazunguka wanaomwogopa, na yeye huwaokoa." (Zaburi 34:7) Kwa nini tunahitaji ulinzi? Kwa sababu tuna maadui wenye nguvu ambao wanataka kutushambulia. Maadui hao ni nani? Walitoka wapi? Wanataka kutuumiza jinsi gani? Ili kujibu maswali hayo, acheni tuchunguze mambo yaliyotokia muda mfupi baada ya Adamu na Hawa kuumbwa.

ADUI ZETU WASIOONEKANA

7 Katika sura ya 3 tulijifunza kwamba malaika mmoja alimwasi Mungu na alitaka kuwatawala wengine. Biblia humwita Shetani Ibilisi. (Ufunuo 12:9) Pia, Shetani alitaka wengine wamwasi Mungu. Alifaulu kumdanganya Hawa, na tangu wakati

6. (a) Tunajua jinsi gani kwamba malaika huwasaidia watu leo? (b) Tutachunguza maswali gani?
7. Shetani amefaulu kufanya nini?

huo amewadanganya wanadamu wengi. Hata hivyo, wanadamu wachache kama vile Abeli, Enoko na Noa, walibaki waaminifu kwa Yehova.—Waebrania 11:4, 5, 7.

8 Wakati wa Noa, baadhi ya malaika waliasi na kuacha makao yao mbinguni ili waishi duniani kama wanadamu. Kwa nini? Biblia inasema kwamba walitaka kuoa. **(Soma Mwanzo 6:2.)** Lakini lilikuwa kosa kwa malaika kufanya hivyo. (Yuda 6) Wakati huo, wanadamu wengi wakawa na maadili mabaya na jeuri kama malaika hao waovu. Ndipo Yehova akaamua kuwaharibu wanadamu wote waovu kwa gharika. Hata hivyo, aliwaokoa watumishi wake waaminifu. (Mwanzo 7:17, 23) Malaika waovu walirudi mbinguni ili wasiharibiwe. Biblia huwaita roho waovu. Walichagua kumuunga mkono Shetani, naye akawa mtawala wao. —Mathayo 9:34.

9 Kwa sababu waliasi, Yehova hakuwakubali tena katika familia yake. (2 Petro 2:4) Roho waovu hawawezi kujibadilisha na kuwa wanadamu tena, lakini bado 'wanaipotosha dunia nzima inayokaliwa.' (Ufunuo 12:9; 1 Yohana 5:19) Hebu tuchunguze jinsi ambavyo roho waovu huwadanganya au kuwapotosha watu wengi leo.**—Soma 2 Wakorintho 2:11.**

JINSI ROHO WAOVU WANAVYOPOTOSHA

10 Roho waovu hutumia njia nyingi kuwapotosha watu. Watu huwasiliana na roho waovu moja kwa


8. (a) Baadhi ya malaika walibadilika jinsi gani na kuwa roho waovu? (b) Roho waovu walifanya nini ili kuokoka Gharika?
9. (a) Ni nini kilichowapata roho waovu waliporudi mbinguni? (b) Tutajifunza nini katika sehemu inayofuata?
10. Roho waovu huwapotosha watu jinsi gani?

moja au kwa kupitia mtu mwingine, kama vile waganga wa kienyeji. Zoea hilo huitwa uwasiliani roho au pepo. Hata hivyo, Biblia inatuonya tuepuke kabisa jambo lolote linalohusiana na roho waovu. (Wagalatia 5:19-21) Kwa nini? Kama vile mwindaji hutumia mtego kuwanasa wanyama, roho waovu hutumia ujanja kuwanasa na kuwaongoza wanadamu.—Soma Maelezo ya Ziada 26.

11 Mbinu moja wanayotumia ni uaguzi. Uaguzi ni kutumia uchawi ili kutafuta habari za wakati ujao au jambo lisilojulikana. Huenda mtu akafanya uaguzi kwa kutazama nyota, kutafuta ishara za bahati, kusoma kadi za karata, kutazama mpira wa kioo, au kwa kusoma viganja vya mkono. Watu wengi hufikiri kwamba uaguzi hauna madhara yoyote, hata hivyo, ni hatari sana. Kwa mfano, Biblia inasema kwamba waaguzi hushirikiana na roho waovu. Katika Matendo 16:16-18 tunasoma kuhusu "roho mwovu wa uaguzi" aliyemwezesha kijakazi kufanya "ufundi wa kubashiri." Baada ya mtume Paulo kumtoa roho huyo mwovu, kijakazi huyo alipoteza uwezo wa kubashiri.

12 Roho waovu hutumia mbinu nyingine kuwanasa watu. Wanajaribu kuwadanganya watu waamini kwamba wafu wako hai, nao wanaweza kuwasiliana nasi au kutuumiza. Kwa mfano, huenda mtu aliyefiwa na rafiki au mtu wa ukoo akamwendea mchawi ambaye hudai ana uwezo wa kuwasiliana na wafu. Huenda akamweleza jambo fulani kuhusu mtu aliyekufa na hata kuiga sauti yake. (1 Samweli 28:3-19)

11. Uaguzi ni nini, na kwa nini tunapaswa kuepuka?
12. (a) Kwa nini ni hatari kuwasiliana na wafu? (b) Kwa nini watumishi wa Mungu hawashiriki desturi za kuwasiliana na wafu?



JINSI YA KUMPINGA SHETANI NA ROHO WAOVU

- Haribu vitu vyote vinavyohusiana na roho waovu au uchawi.
- Jifunze Biblia.
- Sali kwa Yehova Mungu.

Pia, desturi nyingi za mazishi zinaonyesha kwamba watu wanaamini kuwa wafu huendelea kuishi mahali fulani. Desturi hizo ni pamoja na sherehe za mazishi, siku za maombezi ya wafu, dhabihu kwa ajili ya wafu, siku za kuwatakasa wajane au sherehe za kukesha. Wakristo wanapokataa kushiriki desturi hizo, huenda watu wa familia au jamii ikawashutumu, kuwadhihaki, au kukataa kushirikiana nao katika shughuli nyingine. Wakristo wanajua kwamba wafu hawaendelei kuishi. Haiwezekani kuwasiliana na wafu, wala hawawezi kutuumiza. (Zaburi 115:17) Uwe mwangalifu sana. Usijaribu kamwe kuwasiliana na wafu, wala kushiriki katika desturi zinazohusiana na roho waovu.—**Soma Kumbukumbu la Torati 18:10, 11**; Isaya 8:19.

13 Roho waovu huwatisha na kuwapotosha watu. Shetani na roho wake waovu wanajua kwamba wana "kipindi kifupi cha wakati" kabla ya kuangamizwa, hivyo wana hasira nyingi na jeuri kuliko wakati mwingine wowote. (Ufunuo 12:12, 17) Hata hivyo, watu wengi ambao waliwaogopa roho waovu, hawawaogopi tena. Ni nini kimewasaidia kushinda woga huo?

WAPINGE ROHO WAOVU

14 Biblia hutueleza jinsi ya kuwapinga roho waovu. Kwa mfano, baadhi ya watu katika jiji la Efeso walikuwa wakiwasiliana na roho waovu kabla ya kujifunza ukweli. Ni nini kilichowasaidia kuacha

13. Watu wengi ambao waliwaogopa roho waovu wamefaulu kufanya nini?

14. Kama Wakristo wa karne ya kwanza, tunaweza kuwapinga jinsi gani roho waovu?

zoea hilo? Biblia inasema hivi: "Hesabu kubwa ya wale waliozoea kufanya ufundi wa uchawi wakaleta pamoja vitabu vyao wakaviteketeza mbele ya kila mtu." (Matendo 19:19) Kwa sababu walitaka kuwa Wakristo waliteketeza vitabu vyote vilivyohusiana na uchawi. Sisi pia tunahitaji kufanya kama wao. Ni lazima mtu anayetaka kumtumikia Yehova, aharibu vitu vyote vinavyohusiana na roho waovu. Vitu hivyo ni pamoja na vitabu, magazeti, kutazama nyota, sinema, muziki, na michezo inayohusisha kuwasiliana na roho waovu, au nguvu za uchawi. Pia, hirizi zinazovaliwa ili kujilinda na roho waovu.—1 Wakorintho 10:21.

15 Miaka kadhaa baada ya Wakristo huko Efeso kuharibu vitabu vyao vya uchawi, Mtume Paulo aliandika kwamba **bado** walihitaji kuendelea "kushindana mweleka" na kupambana na "majeshi ya roho waovu." (Waefeso 6:12) Ingawa walichoma vitabu vyao, bado roho waovu walijaribu kuwadhuru. Kwa hiyo, walihitaji kufanya nini? Paulo aliwaambia: "Zaidi ya mambo yote, ichukueni ngao kubwa ya imani, ambayo kwa kuitumia mtaweza kuizima mishale yote inayowaka moto ya yule mwovu." (Waefeso 6:16) Kama vile ngao humkinga askari vitani, imani yetu itatulinda. Tukimtumaini kabisa Yehova, atatulinda na tutamshinda Shetani na roho waovu.—Mathayo 17:20.

16 Tunaweza kuimarisha imani yetu kwa Yehova jinsi gani? Tunapaswa kusoma Biblia kila siku na ku-

15. Ni jambo gani lingine tunalohitaji kufanya ili kumpinga Shetani na roho waovu?
16. Tunaweza kuimarisha imani yetu katika Yehova jinsi gani?

mtegemea ili atulinde. Tukimtumaini Yehova, Shetani na roho wake waovu hawataweza kutudhuru.—1 Yohana 5:5.

17 Wakristo huko Efeso walihitaji kufanya jambo gani lingine? Waliishi katika jiji ambalo lilijaa mazoea ya kuwasiliana na roho waovu. Kwa hiyo Paulo aliwaambia hivi: "Endelezeni sala kila wakati." (Waefeso 6:18) Walihitaji kumwomba Yehova awalinde nyakati zote. Namna gani sisi? Tunaishi katika ulimwengu uliojaa mazoea ya kuwasiliana na roho waovu. Kwa hiyo, tunahitaji kumwomba Yehova atulinde, na tusali kwa kutumia jina lake. **(Soma Methali 18:10.)** Tukiendelea kumwomba Yehova atukomboe kutokana na Shetani, atajibu sala zetu.—Zaburi 145:19; Mathayo 6:13.

18 Tukiharibu kila kitu kinachohusiana na roho waovu na kumtegemea Yehova atulinde, tunaweza kumpinga Shetani na roho waovu. Hatupaswi kuwaogopa. **(Soma Yakobo 4:7, 8.)** Yehova ana nguvu kuliko roho waovu. Aliwaadhibu katika siku za Noa, na atawaangamiza wakati ujao. (Yuda 6) Kumbuka kwamba hatupigani vita hivyo peke yetu, Yehova hutumia malaika wake ili kutulinda. (2 Wafalme 6:15-17) Tuwe na uhakika kwamba tunaweza kushinda vita dhidi ya Shetani na roho waovu kwa sababu Yehova atatusaidia.—1 Petro 5:6, 7; 2 Petro 2:9.

19 Hata hivyo, kwa nini Mungu hajamwagamiza Shetani na roho waovu ambao wanasababisha mateso? Sura inayofuata itajibu swali hilo?

---

17. Tunahitaji kufanya jambo gani jingine ili kujilinda na roho waovu?
18, 19. (a) Tunaweza kushinda vita dhidi ya Shetani na roho waovu jinsi gani? (b) Sura inayofuata itajibu swali gani?

UKWELI WA 1 MALAIKA NI SEHEMU YA FAMILIA YA MUNGU

"Mbarikini Yehova, enyi malaika zake, mlio na uwezo katika nguvu."—Zaburi 103:20

Tunajua nini kuwahusu malaika?

Ayubu 38:4-7
Yehova aliwaumba malaika kabla hajaiumba dunia.

Ufunuo 5:11
Kuna mamilioni ya malaika.

1 Petro 1:11, 12
Sikuzote malaika wamependezwa na kutimizwa kwa kusudi la Yehova kwa dunia.

Luka 15:10
Malaika wanapendezwa na wale wote wanaomtumikia Mungu.

UKWELI WA 2 MALAIKA HUWASAIDIA WATUMISHI WA MUNGU

"Malaika wa Yehova anapiga kambi pande zote kuwazunguka wanaomwogopa, na yeye huwaokoa." —Zaburi 34:7

Tunajua jinsi gani kwamba malaika huwasaidia watu?

Mwanzo 19:15, 16; Danieli 6:22; Luka 22:43; Matendo 12:6-11
Malaika walimsaidia Loti, Danieli, Yesu, na Petro.

Waebrania 1:7, 14
Leo, Yehova huwatumia malaika kuwasaidia na kuwalinda watumishi wake.

UKWELI WA 3 MALAIKA WAOVU WANATAKA KUTUDHURU

"Shetani asitushinde akili, kwa maana sisi hatukosi kuzijua mbinu zake."—2 Wakorintho 2:11

Roho waovu ni nani, na kwa nini wao ni hatari?

Ufunuo 12:9
Shetani ni malaika aliyemwasi Yehova.

Mwanzo 6:2
Katika siku za Noa, baadhi ya malaika waliasi na kuja duniani.

Mathayo 9:34
Malaika hao walijiunga na uasi wa Shetani nao wakawa roho waovu.

Kumbukumbu la Torati 18: 10, 11
Roho waovu wanataka kuwadanganya na kuwadhuru watu kwa njia mbalimbali.

UKWELI WA 4 UNAWEZA KUMPINGA SHETANI NA ROHO WAOVU

"Mpingeni Ibilisi, naye atawakimbia ninyi."—Yakobo 4:7

Unaweza kupata jinsi gani msaada wa Yehova wa kumpinga Shetani na roho waovu?

Matendo 19:19
Haribu vitu vyote ambavyo hufanya kuwasiliana na pepo kuonekane kuwa hakuna madhara au ni jambo la kusisimua tu.

Waefeso 6:16, 18
Imarisha imani yako kwa kujifunza Biblia, na usali upate ulinzi wa Mungu.

Methali 18:10
Tumia jina la Yehova.

KWA NINI KUNA MATESO MENGI ULIMWENGUNI?

KIJIJI kinakumbwa na tsunami. Mhalifu anafyatua risasi kanisani, anajeruhi na kuua watu wengi sana. Mama anakufa kwa kansa na kuwaacha watoto watano wakiwa mayatima.

2 Majanga kama hayo yanapotokea, watu wengi hujiuliza, "Kwa nini?" Watu wengi wanajiuliza kwa nini ulimwengu umejaa chuki na mateso. Je, umewahi kujiuliza hivyo?

3 Katika Biblia, tunajifunza kuhusu wanaume waaminifu ambao walimwuliza Mungu maswali kama hayo. Kwa mfano, nabii Habakuki alimwuliza Yehova hivi: "Kwa nini unanionyesha jambo lenye kudhuru, nawe unaendelea kutazama taabu tupu? Na kwa nini kuna uporaji na jeuri mbele yangu, kwa nini kugombana hutokea, kwa nini mzozo huendelezwa?"—Habakuki 1:3.

4 Katika andiko la Habakuki 2:2, 3, tunasoma jinsi Mungu alivyomjibu Habakuki na ahadi yake ya kurekebisha hali. Yehova anawapenda sana watu. Biblia inasema hivi: "Anawajali ninyi." (1 Petro 5:7) Kwa kweli, Mungu anachukia kuona watu wakiteseka. (Isaya 55:8, 9) Hivyo basi, acheni tuzungumzie swali hili: Kwa nini ulimwengu umejaa mateso?

1, 2. Watu wengi wanajiuliza swali gani?
3, 4. (a) Habakuki aliuliza maswali gani? b) Yehova alimjibu jinsi gani?

KWA NINI KUNA MATESO MENGI SANA?

5 Mara nyingi viongozi na walimu wa dini hufundisha kwamba watu wanapoteseka ni mapenzi ya Mungu. Wengine wanasema kwamba mambo yote mabaya yanayowapata watu yamepangwa na Mungu na hatuwezi kuelewa sababu. Wengine wanasema kwamba watu, hata watoto wadogo wanakufa ili wakaishi na Mungu mbinguni. Hata hivyo, mafundisho hayo si ya kweli. Yehova hasababishi mambo mabaya yatukie. Biblia inasema: "Hasha, Mungu wa kweli asitende kwa uovu, Na Mweza-Yote kutenda isivyo haki!"—Ayubu 34:10.

6 Watu wengi wanamlaumu Mungu kwa sababu ya mateso yaliyojaa ulimwenguni. Wanafikiri kwamba Mungu ndiye anayetawala ulimwengu huu. Lakini kama tulivyojifunza katika sura ya 3, mtawala halisi wa ulimwengu huu ni Shetani Ibilisi.

7 Biblia inasema kwamba "ulimwengu mzima unakaa katika nguvu za yule mwovu." (1 Yohana 5: 19) Mtawala wa ulimwengu huu, Shetani, ni mkatili. 'Anaipotosha dunia nzima inayokaliwa.' (Ufunuo 12:9) Watu wengi wanamwiga. Hiyo ni sababu moja inayofanya ulimwengu ujae uwongo, chuki na jeuri.

8 Kuna sababu nyingine zinazofanya ulimwengu ujae mateso. Baada ya Adamu na Hawa kuasi, wazao wao walirithi dhambi hiyo. Hivyo, kwa sababu ya dhambi, wanadamu wanawaumiza wanadamu wenzao.

---

5. Walimu wengi wa dini wanafundisha nini kuhusu mateso? Biblia inafundisha nini?

6. Kwa nini watu wengi wanamlaumu Mungu kwa mateso yaliyo ulimwenguni?

7, 8. Kwa nini ulimwengu umejaa mateso?

Wanafikiria faida zao wenyewe tu. Wanapigana, wanaenda vitani, na kuwanyanyasa wengine. (Mhubiri 4:1; 8:9) Nyakati nyingine watu wanateseka kwa sababu ya "wakati na tukio lisilotazamiwa." (Mhubiri 9: 11) Wanapokuwa mahali na wakati usiofaa, aksidenti na mambo mengine mabaya yanaweza kutukia.

9 Kamwe Yehova hasababishi mateso. Hatupaswi kumlaumu kwa sababu ya vita, jeuri na ukandamizaji. Mungu hasababishi majanga kama vile matetemeko, vimbunga na mafuriko. Lakini huenda ukajiuliza, 'Ikiwa Yehova ndiye mwenye nguvu zaidi katika ulimwengu wote mzima, kwa nini hazuii mambo mabaya yatukie?' Tunajua kwamba Mungu anatujali sana, kwa hiyo lazima awe na sababu nzuri ya kuacha mateso yaendelee.—1 Yohana 4:8.

KWA NINI MUNGU AMEACHA MATESO YAENDELEE?

10 Katika bustani ya Edeni, Ibilisi aliwadanganya Adamu na Hawa. Shetani alimshtaki Mungu kuwa ni mtawala mbaya. Alidai kwamba Mungu alikuwa anawanyima Adamu na Hawa mambo mazuri. Alitaka waamini kwamba yeye [Shetani] angekuwa mtawala mzuri kuliko Yehova na kwamba hawakuhitaji utawala wa Mungu.—Mwanzo 3:2-5; soma Maelezo ya Ziada 27.

11 Adamu na Hawa walikataa kumtii Yehova na wakamwasi. Walifikiri walikuwa na haki ya kujiamulia mema na mabaya. Yehova angethibitisha jinsi gani

9. Kwa nini tuna uhakika kwamba Yehova ana sababu nzuri ya kuacha mateso?
10. Shetani alimpinga Yehova jinsi gani?
11. Tunahitaji jibu la swali gani?

kwamba waasi hao wamekosea na kwamba yeye ndiye anayejua yanayotufaa?

12 Yehova hakuwaharibu Adamu na Hawa mara moja. Badala yake, aliwaruhusu wazae watoto. Kisha, Yehova akafanya iwezekane kwa watoto wa Adamu na Hawa kuchagua yule atakayekuwa mtawala wao. Kusudi la Yehova lilikuwa kuijaza dunia watu wakamilifu, na hilo lingetimia licha ya upinzani wa Shetani. —Mwanzo 1:28; Isaya 55:10, 11.

13 Shetani alimpinga Yehova mbele ya mamilioni ya malaika. (Ayubu 38:7; Danieli 7:10) Hivyo, Yehova alimpa Shetani muda ili kuthibitisha mashtaka yake. Pia aliwapa wanadamu wakati wa kuanzisha serikali zao chini ya utawala wa Shetani na kuona kama zingeweza kufanikiwa bila msaada wa Mungu.

14 Kwa miaka mingi, wanadamu wamejaribu kujitawala lakini wameshindwa. Shetani amethibitika kuwa mwongo. Wanadamu **wanahitaji** msaada wa Mungu. Nabii Yeremia alikuwa sahihi alipoandika hivi: "Ninajua vema, Ee Yehova, kwamba njia ya mtu wa udongo haimo katika uwezo wake. Mwanadamu anayetembea hana uwezo wa kuongoza hatua yake."—Yeremia 10:23.

KWA NINI YEHOVA AMESUBIRI KWA MUDA MREFU?

15 Kwa nini Yehova ameruhusu mateso yaendelee

12, 13. (a) Kwa nini Yehova hakuwaharibu waasi hao mara tu baada ya kuasi? (b) Kwa nini Yehova ameruhusu Shetani atawale ulimwengu huu na wanadamu wajitawale?

14. Utawala wa wanadamu umethibitisha nini?

15, 16. (a) Kwa nini Yehova ameruhusu mateso yaendelee kwa muda mrefu? (b) Kwa nini hajazuia matatizo yanayosababishwa na Shetani?

kwa muda mrefu? Kwa nini hazuii mambo mabaya yasitokee? Ilihitaji muda mrefu kuthibitisha kwamba utawala wa Shetani umeshindwa. Wanadamu wamejaribu mifumo mbalimbali ya serikali bila mafanikio. Hata ingawa wamefanya maendeleo katika sayansi na teknolojia, kuna ukosefu wa haki, umaskini, jeuri, na vita kuliko wakati mwingine wowote. Wanadamu hawawezi kujiongoza kwa mafanikio bila Mungu.

16 Hata hivyo, Yehova hajaondoa matatizo yaliyosababishwa na Shetani. Ikiwa angefanya hivyo angekuwa anaunga mkono utawala wa Shetani, na hawezi kamwe kufanya hivyo. Pia, wanadamu wangeamini kwamba wanaweza kujitawala wenyewe kwa mafanikio, jambo ambalo si kweli na Yehova hawezi kuunga mkono jambo hilo. Yeye hasemi uwongo.—Waebrania 6:18.

17 Je, Yehova anaweza kuondoa madhara yote ambayo yamesababishwa na uasi wa Shetani na wanadamu? Ndiyo. Kwa Mungu mambo yote yanawezekana. Yehova anajua wakati ambao atajibu mashtaka yote ya Shetani. Kisha, ataifanya dunia kuwa paradiso, kama alivyokusudia. Wote walio katika "makaburi ya ukumbusho" watafufuliwa. (Yohana 5:28, 29) Watu hawataugua wala kufa tena. Yesu ataondoa madhara yote yaliyosababishwa na Shetani. Yehova atamtumia Yesu 'kuvunja kazi za Ibilisi.' (1 Yohana 3:8) Tunashukuru sana kwamba Yehova amekuwa na subira hivi kwamba tumepata fursa ya kumjua na tunaweza kua-

17, 18. Yehova atafanya nini kuhusu madhara yote ambayo yamesababishwa na Shetani?

mua awe Mtawala wetu. **(Soma 2 Petro 3:9, 10.)** Hata tunapoteseka, anatusaidia kuendelea kuvumilia.—Yohana 4:23; **soma 1 Wakorintho 10:13.**

18 Yehova hatulazimishi tumchague awe Mtawala wetu. Ametupatia uhuru wa kuchagua. Acheni tuchunguze jinsi tunavyoweza kutumia uhuru huo.

UTATUMIAJE UHURU WA KUCHAGUA?

19 Uhuru wa kuchagua ambao tumepewa na Yehova unatufanya tuwe tofauti na wanyama. Wanyama wanaongozwa na silika, lakini sisi tunaweza kuamua jinsi tutakavyoishi na ikiwa tutamtumikia Yehova. (Methali 30:24) Sisi si kama mashine ambazo zinaongozwa na mtu mwingine. Tuna uhuru wa kuchagua marafiki, jinsi tutakavyoishi, na mambo tutakayofanya maishani. Yehova anapenda tufurahie maisha.

20 Yehova anataka tumpende. (Mathayo 22:37, 38) Yeye ni kama baba anayefurahia kusikia mtoto wake anapomwambia "Nakupenda" kutoka moyoni bila kulazimishwa. Yehova ametupatia uhuru wa kuchagua kumtumikia au kutomtumikia. Shetani, Adamu, na Hawa walichagua kutomtumikia Yehova. **Wewe** utatumiaje uhuru wa kuchagua?

21 Chagua kumtumikia Yehova. Kuna mamilioni ya watu ambao wameamua kumpendeza Mungu na kumkataa Shetani. (Methali 27:11) Unaweza kufanya nini sasa ili ustahili kuingia katika ulimwengu mpya ambao hautakuwa na mateso? Sura inayofuata itajibu swali hilo.

---

19. Yehova ametupatia nini? Kwa nini tunapaswa kumshukuru?
20, 21. Unaweza kufanya uamuzi gani sasa?

UKWELI WA 1 YEHOVA HASABISHI MATESO

"Hasha, Mungu wa kweli asitende kwa uovu, na Mweza-Yote kutenda isivyo haki!"—Ayubu 34:10

Kwa nini ulimwengu umejaa mateso?

1 Yohana 5:19
Shetani Ibilisi ndiye mtawala wa ulimwengu huu.

Mhubiri 8:9
Wanadamu wamewasababishia wengine mateso.

Mhubiri 9:11
Wakati mwingine watu huteseka kwa sababu ya kuwa mahali na wakati usiofaa.

1 **Petro 5:7**
Yehova anawapenda sana watu. Anaumia kuona wakiteseka.

UKWELI WA 2 SHETANI ALITILIA SHAKA HAKI YA YEHOVA YA KUTAWALA

"Mungu anajua kwamba . . . macho yenu yatafunguliwa, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya."—Mwanzo 3:5

Kwa nini Yehova hakupuuza dai la Shetani?

Mwanzo 3:2-5
Shetani alidai kwamba Mungu ni mtawala mbaya. Shetani alitaka wanadamu waamini kwamba wana haki ya kujiamulia mema na mabaya.

Ayubu 38:7
Mamilioni ya malaika walishuhudia Shetani akimpinga Yehova.

UKWELI WA 3 DAI LA SHETANI HALIJAFAULU

"Mwanadamu anayetembea hana uwezo wa kuongoza hatua yake."—Yeremia 10:23

Kwa nini wanadamu wameteseka kwa muda mrefu?

Isaya 55:9
Wanadamu wamejaribu aina mbalimbali za serikali, hata hivyo, hawawezi kufaulu kujitawala bila mwongozo wa Mungu.

2 Petro 3:9, 10
Yehova ni mwenye subira na ameruhusu muda upite ili tumjue na tumkubali kuwa Mtawala wetu.

1 Yohana 3:8
Yehova atamtumia Yesu kuondoa madhara yote yaliyosababishwa na Shetani.

UKWELI WA 4 TUMIA UHURU WAKO WA KUCHAGUA KUMTUKIA YEHOVA

"Uwe na hekima, mwanangu, . . . ili nipate kumjibu anayenidhihaki."—Methali 27:11

Kwa nini Yehova hatulazimishi tumtumikie?

Methali 30:24
Wanyama wanaongozwa na silika, lakini Yehova ametupatia uhuru wa kuchagua. Tunaweza kuamua kumtumikia au kutomtumikia.

Mathayo 22:37, 38
Yehova anataka tumtumikie kwa sababu tunampenda.

JINSI UNAVYOWEZA KUWA RAFIKI YA MUNGU

UNGEPENDA kuwa na rafiki wa aina gani? Bila shaka ni yule unayempenda na aliye tayari kushirikiana nawe. Mwenye fadhili na sifa nyingine bora unazopenda.

2 Yehova Mungu amewachagua baadhi ya wanadamu wawe rafiki zake. Kwa mfano, Abrahamu alikuwa rafiki wa Yehova. (Isaya 41:8; Yakobo 2:23) Yehova alimpenda pia Daudi. Alisema kwamba Daudi alikuwa 'mtu anayekubalika moyoni mwake.' (Matendo 13:22) Nabii Danieli alikuwa "mwenye kutamanika sana" na Yehova. —Danieli 9:23.

3 Kwa nini Abrahamu, Daudi, na Danieli walikuwa rafiki za Yehova? Yehova alimwambia Abrahamu hivi: "Umeisikiliza sauti yangu." (Mwanzo 22:18) Yehova ni rafiki ya wale wote wanaomtii kwa unyenyekevu. Hata watu wa taifa zima wanaweza kuwa rafiki za Yehova. Yehova aliliambia taifa la Israeli hivi: "Tiini sauti yangu, nami nitakuwa Mungu wenu, nanyi mtakuwa watu wangu." (Yeremia 7:23) Hivyo, unahitaji kumtii Yehova ikiwa unataka kuwa rafiki yake.

YEHOVA ANAWALINDA RAFIKI ZAKE

4 Biblia inasema kwamba Yehova anatafuta nafasi "ili aonyeshe nguvu zake kwa ajili ya wale ambao moyo wao ni mkamilifu kumwelekea yeye." (2 Mambo ya Nyakati

1, 2. Taja baadhi ya watu waliokuwa rafiki za Yehova.
3. Kwa nini Abrahamu, Daudi, na Danieli walikuwa rafiki za Yehova?
4, 5. Yehova anawalinda jinsi gani rafiki zake?

16:9) Katika Zaburi 32:8, Yehova anawaahidi rafiki zake hivi: "Nitakufanya uwe na ufahamu na kukufundisha katika njia unayopaswa kuiendea. Nitakupa shauri jicho langu likiwa linakutazama."

5 Adui mwenye nguvu anataka kutuzuia tusiwe rafiki za Mungu. Hata hivyo, Yehova anataka kutulinda dhidi ya adui huyo. **(Soma Zaburi 55:22.)** Tunamtumikia Yehova kwa moyo wote, kwa sababu ni rafiki yetu. Tunashikamana naye hata tukikabili hali ngumu. Nasi tuna uhakika kama wa mtunga zaburi, ambaye aliandika hivi kuhusu Yehova: "Kwa sababu yuko upande wa mkono wangu wa kuume, sitatikiswa." (Zaburi 16:8; 63:8) Shetani hutuzuia jinsi gani tusiwe rafiki za Mungu?

MADAI YA SHETANI

6 Katika sura ya 11 tulijifunza kwamba Shetani alidai kuwa Yehova ni mwongo na hatendi haki kwa sababu aliwanyima Adamu na Hawa uhuru wa kujiamulia mema na mabaya. Kitabu cha Ayubu kinatuambia kwamba Shetani anawashutumu pia watu wote wanaotaka kuwa rafiki za Mungu. Anadai kwamba wanamtumikia Mungu kwa kuwa amewabariki, na si kwa sababu wanampenda. Pia, Shetani anadai kuwa anaweza kumgeuza **mtu yeyote** aache kumtumikia Mungu. Acheni tuchunguze mambo tunayojifunza kutoka kwa Ayubu na jinsi Yehova alivyomlinda.

7 Ayubu alikuwa nani? Alikuwa mtu mwaminifu aliyeishi miaka 3,600 iliyopita. Yehova alisema hakuna mwanadamu yeyote duniani aliyekuwa kama Ayubu. Ayubu alimheshimu sana Mungu, na alichukia mambo

---

6. Shetani anadai nini kuhusu wanadamu?

7, 8. (a) Yehova alimwonaje Ayubu? (b) Shetani alidai nini kumhusu Ayubu?

mabaya. (Ayubu 1:8) Naam, Ayubu alikuwa rafiki ya Yehova.

8 Shetani alidai kwamba Ayubu alimtumikia Mungu kwa sababu ya ubinafsi. Shetani alimwambia Yehova hivi: "Je, wewe hukuweka ukuta [au, wigo] kumzunguka yeye na kuzunguka nyumba yake na kuzunguka kila kitu alicho nacho pande zote? Umeibariki kazi ya mikono yake, na mifugo yake imeenea kotekote duniani. Lakini, ili kuwe na badiliko, tafadhali nyoosha mkono wako, uguse kila kitu alicho nacho, uone kama hatakulaani wewe mbele za uso wako."—Ayubu 1:10, 11.

9 Shetani alidai kwamba Ayubu alimtumikia Yehova kwa sababu Mungu alimbariki. Shetani alidai kwamba angeweza kumgeuza Ayubu aache kumtumikia. Yehova alijua kwamba madai hayo yalikuwa ya uwongo, lakini alimruhusu Shetani amjaribu Ayubu ili athibitishe madai yake.

SHETANI AMSHAMBULIA AYUBU

10 Kwanza, Shetani alisababisha mifugo yote ya Ayubu iibiwe au kuuawa. Halafu, aliwaua watumishi wengi wa Ayubu. Ayubu alipoteza kila kitu. Mwishowe, Shetani aliwaua watoto kumi wa Ayubu kwa kimbunga. Hata hivyo, Ayubu aliendelea kushikamana na Yehova. "Katika hayo yote Ayubu hakutenda dhambi, wala kumhesabia Mungu jambo lolote lisilofaa."—Ayubu 1:12-19, 22.

11 Shetani hakukata tamaa. Alimwambia Mungu hivi: "Uguse kufikia mfupa wake na nyama yake, uone kama hatakulaani wewe mbele za uso wako." Hivyo, Sheta-

---

9. Yehova alimruhusu Shetani afanye nini?
10. Shetani alimshambulia Ayubu jinsi gani, na Ayubu alitendaje?
11. (a) Ni mambo gani mengine ambayo Shetani alimsababishia Ayubu? (b) Ayubu alitendaje?

ni alimshambulia Ayubu kwa ugonjwa wenye maumivu makali. (Ayubu 2:5, 7) Lakini Ayubu aliendelea kushikamana na Yehova. Alisema hivi: "Mpaka nitakapokata pumzi, sitajiondolea utimilifu wangu!"—Ayubu 27:5.

12 Ayubu hakujua chochote kuhusu madai ya Shetani au sababu za kuteseka. Alifikiri kwamba Yehova ndiye aliyesababisha matatizo aliyokabili. (Ayubu 6:4; 16:11-14) Licha ya hali hizo, Ayubu aliendelea kuwa mshikamanifu kwa Yehova. Bila shaka, Shetani alipata jibu la madai yake. Ayubu hakuwa mbinafsi. Alikuwa rafiki ya Yehova kwa sababu alimpenda. Madai ya Shetani yalithibitika kuwa ni ya uwongo!


13 Ingawa Ayubu hakujua mambo yaliyotokia mbinguni, alikuwa mshikamanifu kwa Mungu na kuthibitisha kwamba Shetani ni mwovu. Yehova alimbariki Ayubu kwa ushikamanifu wake.—Ayubu 42:12-17.

JINSI UNAVYOHUSIKA

14 Unaweza kujifunza mambo muhimu kutokana na majaribu yaliyompata Ayubu. Shetani anadai kwamba tunamtumikia Yehova kwa sababu ametubariki. Katika Ayubu 2:4, Shetani alidai kwamba: "Kila kitu alicho nacho **mtu** atakitoa kwa ajili ya nafsi yake." Kwa hiyo, Shetani anawashutumu watumishi **wote** wa Yehova kwamba ni wenye ubinafsi. Miaka mingi baada ya Ayubu kufa, Shetani aliendelea kumdhihaki Yehova na kuwashutumu watumishi wake. Kwa mfano, andiko la Methali 27:11, linasema hivi: "Uwe na hekima, mwanangu, na kuufanya moyo wangu ushangilie, ili nipate kumjibu anayenidhihaki."

---

12. Ayubu alithibitishaje kwamba Shetani ni mwongo?
13. Ayubu alipata matokeo gani kwa sababu ya ushikamanifu wake?
14, 15. Shetani anadai nini kuhusu watumishi wa Yehova?



Yehova alimbariki
Ayubu kwa sababu
ya ushikamanifu wake

15 Unaweza kuchagua kumtii Yehova na kuwa rafiki yake ili kuthibitisha kwamba Shetani ni mwongo. Kuchagua kuwa rafiki ya Mungu ni uamuzi bora sana hata kama utahitaji kufanya mabadiliko makubwa maishani mwako! Uamuzi huo ni jambo zito. Shetani anadai kwamba ukikabili matatizo, **huwezi** kuwa mshikamanifu kwa Mungu. Anajaribu kutupotosha tuache kushikamana na Mungu. Anatumia mbinu gani?

16 Shetani anatumia mbinu mbalimbali ili kutuzuia tusiwe rafiki za Mungu. Anatushambulia "kama simba anayenguruma, akitafuta kummeza mtu." (1 Petro 5:8) Usishangae marafiki zako, watu wa familia, au wengine wanapokuzuia kujifunza Biblia na kufanya mambo mazuri. Huenda ukahisi kana kwamba unashambuliwa.* (Yohana 15:19, 20) Pia, Shetani anaweza kujifanya "malaika wa nuru." Hivyo, anaweza kutupotosha tusimtii Yehova. (2 Wakorintho 11:14) Mbinu nyingine ambayo Shetani anatumia kutuzuia kumtumikia Yehova ni kutufanya tuhisi hatustahili kumtumikia Mungu.—Methali 24:10.

TII AMRI ZA YEHOVA

17 Tunapomtii Yehova, tunathibitisha kwamba Shetani ni mwongo. Ni nini kitakachotusaidia kuwa watiifu? Biblia inasema hivi: "Lazima umpende Yehova Mungu

* Hilo halimaanishi kwamba Shetani anawatuma watu wajaribu kukuzuia kujifunza Biblia. Hata hivyo, Shetani ni "mungu wa mfumo huu wa mambo," na "ulimwengu mzima unakaa katika nguvu [zake]." Hivyo, haishangazi kuona baadhi ya watu wakijaribu kutuzuia kumtumikia Yehova.—2 Wakorintho 4:4; 1 Yohana 5:19.

16. (a) Ni mbinu gani ambazo Shetani anatumia ili kuwazuia watu kumtumikia Yehova? (b) Huenda Shetani akatumia mbinu gani ili kukuzuia kumtumikia Yehova?
17. Kwa nini tunamtii Yehova?

wako kwa moyo wako wote na kwa nafsi yako yote na kwa nguvu zako zote." (Kumbukumbu la Torati 6:5) Tunamtii Yehova kwa sababu tunampenda. Upendo wetu kwa Yehova unapoongezeka, utatuchochea kufanya jambo lolote analoagiza. Mtume Yohana aliandika hivi: "Kumpenda Mungu humaanisha hivi, kwamba tuzishike amri zake; na bado amri zake si mzigo mzito."—1 Yohana 5:3.

18 Ni baadhi ya mambo gani yanayomchukiza Yehova? Kuna mifano kadhaa katika sanduku "Chukia mambo yanayomchukiza Yehova." Huenda mwanzoni ukahisi kwamba baadhi ya mambo hayo si mabaya sana. Lakini unaposoma mistari hiyo ya Biblia na kuitafakari, utaelewa faida za kutii amri za Yehova. Pia, utagundua

18, 19. (a) Ni baadhi ya mambo gani ambayo yanamchukiza Yehova? (b) Tunajua jinsi gani kwamba Yehova hawezi kutuagiza tufanye jambo lolote linalopita uwezo wetu?

CHUKIA MAMBO YANAYOMCHUKIZA YEHOVA

- **Mauaji**
  Kutoka 20:13; 21:22, 23
- **Mwenendo mpotovu kingono**
  Walawi 20:10, 13, 15, 16; Waroma 1:24, 26, 27, 32; 1 Wakorintho 6:9, 10
- **Ushirikina**
  Kumbukumbu la Torati 18:9-13; 1 Wakorintho 10:21, 22; Wagalatia 5:20, 21
- **Ibada ya sanamu**
  1 Wakorintho 10:14
- **Ulevi**
  1 Wakorintho 5:11
- **Wizi**
  Walawi 6:2, 4; Waefeso 4:28
- **Uwongo**
  Methali 6:16, 19; Wakolosai 3:9; Ufunuo 22:15

kwamba unahitaji kufanya mabadiliko fulani maishani mwako. Huenda ikawa vigumu kubadilika, hata hivyo ukifanya mabadiliko, utapata amani na furaha kwa sababu ya ushikamanifu wako kwa Mungu. (Isaya 48: 17, 18) Je, inawezekana kufanya mabadiliko?

19 Yehova hawezi kutuagiza tufanye jambo lolote linalopita uwezo wetu. (Kumbukumbu la Torati 30:11-14) Akiwa Rafiki yetu wa karibu, anatujua vizuri kuliko tunavyojijua. Anajua uwezo na udhaifu wetu. (Zaburi 103:14) Mtume Paulo alitutia moyo hivi: "Mungu ni mwaminifu, naye hatawaacha ninyi mjaribiwe kupita mnavyoweza kuhimili, bali pamoja na hilo jaribu ataifanya pia njia ya kutokea kusudi mweze kulivumilia." (1 Wakorintho 10:13) Tuna uhakika kwamba Yehova atatupatia nguvu za kufanya mambo yanayofaa. Atakupatia "nguvu zinazopita zile za kawaida" ili uvumilie hali ngumu. (2 Wakorintho 4:7) Mtume Paulo,

- **Pupa**
  1 Wakorintho 5:11
- **Jeuri**
  Zaburi 11:5; Methali 22:24, 25; Malaki 2:16; Wagalatia 5:20, 21
- **Matusi na porojo**
  Walawi 19:16; Waefeso 5:4; Wakolosai 3:8
- **Matumizi mabaya ya damu**
  Mwanzo 9:4; Matendo 15:20, 28, 29
- **Kukataa kuitunza familia**
  1 Timotheo 5:8
- **Kushiriki katika vita au siasa**
  Isaya 2:4; Yohana 6:15; 17:16
- **Kuvuta sigara na kutumia dawa za kulevya**
  Marko 15:23; 2 Wakorintho 7:1

aliyepata msaada wa Mungu alipokabili hali ngumu, alisema hivi: "Kwa mambo yote nina nguvu kupitia yeye anayenipa nguvu."—Wafilipi 4:13.

JIFUNZE KUPENDA MAMBO YANAYOMPENDEZA MUNGU

20 Tukitaka kuwa rafiki za Yehova, tunapaswa kufanya mambo mengi zaidi ya kuchukia tu mambo mabaya. (Waroma 12:9) Rafiki za Yehova wanapenda mambo yanayompendeza. Mambo hayo yanatajwa katika **Zaburi 15:1-5. (Soma.)** Rafiki za Yehova wanaiga sifa zake, kama vile "upendo, shangwe, amani, ustahimilivu, fadhili, wema, imani, upole, kujizuia."—Wagalatia 5: 22, 23.

21 Unaweza kuiga jinsi gani sifa hizo za Mungu? Unaweza kujua mambo yanayompendeza Yehova kwa kusoma na kujifunza Biblia kila siku. (Isaya 30:20, 21) Unapofanya hivyo, upendo wako kwa Yehova utaongezeka, nawe utachochewa kumtii zaidi.

22 Kufanya mabadiliko maishani ni sawa na kubadili nguo chafu na kuvaa nguo safi. Biblia inasema kwamba unahitaji "kuvua utu wa zamani" na kuvaa "utu mpya." (Wakolosai 3:9, 10) Ingawa si rahisi, tukifanya mabadiliko na kumtii Yehova, anaahidi kutupatia "thawabu kubwa." (Zaburi 19:11) Naam, chagua kumtii Yehova, na kuthibitisha kwamba Shetani ni mwongo. Mtumikie Yehova kwa moyo wote na si kwa sababu ya baraka za wakati ujao. Hatimaye utakuwa rafiki wa karibu wa Mungu!

---

20. Unapaswa kuiga sifa gani za Mungu, na kwa nini?
21. Unaweza kujifunza jinsi gani sifa zinazompendeza Mungu?
22. Ukimtii Yehova utapata baraka gani?

UKWELI WA 1 RAFIKI ZA YEHOVA HUMTII

"Tiini sauti yangu, nami nitakuwa Mungu wenu, nanyi mtakuwa watu wangu."—Yeremia 7:23

Je inawezekana kuwa rafiki ya Mungu?

Mwanzo 22:18; Yakobo 2:23
Abrahamu alikuwa rafiki ya Yehova kwa kuwa alimwamini na kumtii Mungu.

2 Mambo ya Nyakati 16:9
Yehova atawasaidia wale wanaomtii.

Zaburi 25:14; 32:8
Yehova huwapa uelewaji rafiki zake.

Zaburi 55:22
Yehova huwategemeza rafiki zake.

UKWELI WA 2 AYUBU ALIKUWA RAFIKI YA MUNGU NAYE ALIENDELEA KUWA MWAMINIFU

"Katika hayo yote Ayubu hakutenda dhambi, wala kumhesabia Mungu jambo lolote lisilofaa."—Ayubu 1:22

Shetani alimshambulia Ayubu jinsi gani, naye Ayubu alitendaje?

Ayubu 1:10, 11
Shetani alidai kwamba Ayubu alimtumikia Mungu kwa sababu za kichoyo na si kwa sababu alimpenda.

Ayubu 1:12-19; 2:7
Yehova alimruhusu Shetani kuharibu mali zote za Ayubu, na Shetani alimpiga Ayubu kwa ugonjwa mbaya sana.

Ayubu 27:5
Ingawa Ayubu hakujua chanzo cha mateso yake makali, aliendelea kuwa mwaminifu.

UKWELI WA 3 SHETANI ANATAKA KUHARIBU UHUSIANO WAKO NA YEHOVA

"Kila kitu alicho nacho mtu atakitoa kwa ajili ya nafsi yake."—Ayubu 2:4

Shetani anatumia mbinu gani kuharibu uhusiano wetu na Yehova?

2 Wakorintho 11:14
Shetani hutushawishi tusimtii Yehova.

Methali 24:10
Shetani anataka tuhisi kwamba hatustahili kumtumikia Yehova.

1 Petro 5:8
Shetani hututesa.

Methali 27:11
Amua kumtii Yehova ili uwe rafiki yake mwaminifu. Hilo litathibitisha kwamba Shetani ni mwongo.

UKWELI WA 4 TUNAMTII YEHOVA KWA SABABU TUNAMPENDA

"Kwa maana kumpenda Mungu humaanisha hivi, kwamba tuzishike amri zake."—1 Yohana 5:3

Unaweza kuwa rafiki ya Yehova jinsi gani?

Kumbukumbu la Torati 6:5
Mpende Mungu. Hilo litakusaidia umtii.

Isaya 48:17, 18
Mtii Yehova, nawe utafaidika milele.

Kumbukumbu la Torati 30: 11-14
Uwe na imani kwamba Yehova hadai mambo yanayozidi uwezo wako.

Wafilipi 4:13
Fanya yaliyo mema, na Yehova atakutegemeza.

HESHIMU ZAWADI YA UHAI

YEHOVA ni "Mungu aliye hai." (Yeremia 10:10) Ni Muumba wetu, naye ametupatia uhai. Biblia inasema: "Uliumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako navyo vikaumbwa." (Ufunuo 4:11) Ndiyo, Yehova anataka tuishi. Uhai ni zawadi kutoka kwa Yehova.**—Soma Zaburi 36:9.**

2 Yehova hutuandalia mahitaji kama vile chakula na maji ili tuishi. (Matendo 17:28) Zaidi ya hayo, anataka tufurahie maisha. (Matendo 14:15-17) Ili tufaulu maishani ni lazima tutii amri za Mungu.—Isaya 48:17, 18.

MUNGU ANA MAONI GANI KUHUSU UHAI?

3 Biblia hutufundisha kwamba Yehova huthamini uhai wetu na uhai wa wengine. Kwa mfano, Kaini mwana wa Adamu na Hawa alipomkasirikia ndugu yake Abeli, Yehova alimwonya adhibiti hasira yake. Lakini Kaini hakumsikiliza, alikasirika sana na mwishowe "akamshambulia Abeli ndugu yake, na kumuua." (Mwanzo 4:3-8) Yehova alimwadhibu Kaini kwa sababu ya kumuua Abeli. (Mwanzo 4:9-11) Hivyo, ni hatari kusitawisha hasira na chuki kwa sababu huenda zikatufanya tutende kwa jeuri au ukatili. Watu wenye jeuri hawatapata uzima wa milele. **(Soma 1 Yohana 3:15.)** Ili tumpendeze Mungu, ni lazima tuwapende wengine. —1 Yohana 3:11, 12.

---

1. Ni nani aliyetupatia uhai?
2. Tunahitaji kufanya nini ili tufaulu maishani?
3. Yehova alifanya nini Kaini alipomuua Abeli?

UHAI NI WENYE THAMANI



- Hatutoi mimba



- Hatuvuti sigara au kutafuna mirungi (miraa) au kutumia dawa za kulevya



- Hatuwachukii wanadamu wenzetu

4 Miaka mingi baadaye, Yehova alionyesha anathamini uhai alipompa Musa Amri kumi. Amri moja ilisema hivi: "Usiue." (Kumbukumbu la Torati 5:17) Ikiwa mtu angemuua mwenzake kwa kukusudia, yeye pia alipaswa kuuawa.

5 Mungu ana maoni gani kuhusu kutoa mimba? Yehova anathamini hata uhai wa mtoto ambaye hajazaliwa. Katika sheria ambayo Yehova aliwapa Waisraeli, Yehova aliwaambia kwamba mtu yeyote ambaye angemwumiza mwanamke mwenye mimba na kusababisha kifo cha mtoto ambaye hajazaliwa, mtu huyo angeuawa. **(Soma Kutoka 21:22, 23;** Zaburi 127:3.) Hilo linatufundisha kwamba ni kosa kutoa mimba.—Soma Maelezo ya Ziada 28.

6 Tunaweza kuonyesha jinsi gani kwamba tuna maoni kama ya Yehova kuhusu uhai wetu na wa wengine? Tukiepuka kufanya jambo lolote linaloweza kuhatarisha uhai wetu au wa wengine. Kwa hivyo tutaepuka kuvuta sigara, kutafuna mirungi (miraa) au kutumia dawa za kulevya kwa sababu zitatudhuru na zinaweza kusababisha kifo.

7 Mungu ndiye aliyetupatia uhai na mwili wetu, nasi tunapaswa kuishi kulingana na kusudi lake. Kwa hiyo, tunapaswa kuutunza mwili wetu. Tusipofanya hivyo, hatutakuwa safi machoni pa Mungu. (Waroma 6:19; 12:1; 2 Wakorintho 7:1) Yehova hawezi kukubali ibada yetu ikiwa hatuthamini uhai ambao ametupatia. Ingawa si rahisi kuacha mazoea hayo mabaya, tukijitahidi

---

4. Sheria ambayo Mungu aliwapa Waisraeli inatufundisha nini kuhusu zawadi ya uhai?
5. Mungu ana maoni gani kuhusu kutoa mimba?
6, 7. Tunaweza kuonyesha jinsi gani kwamba tuna maoni kama ya Yehova kuhusu uhai?

Yehova atatusaidia kuacha mazoea hayo kwa sababu tunauthamini uhai.

8 Tumejifunza kwamba uhai ni zawadi yenye thamani. Yehova ana uhakika kwamba tutajitahidi kuutunza uhai wetu na wa wengine. Tutaendesha kwa uangalifu magari, pikipiki na vyombo vingine vya usafiri. Tutaepuka michezo hatari au yenye jeuri. (Zaburi 11:5) Pia, tunajitahidi kudumisha usalama nyumbani. Yehova aliwaamuru Waisraeli hivi: "Ikiwa utajenga nyumba mpya, pia utafanya ukuta wa ukingoni kwa ajili ya dari lako, ili usiletee nyumba yako hatia ya damu kwa sababu mtu anaweza kuanguka kutoka hapo."—Kumbukumbu la Torati 22:8.

9 Yehova anajali pia jinsi tunavyowatendea wanyama. Ameturuhusu kuchinja wanyama kwa ajili ya chakula na mavazi au kuua mnyama ikiwa anahatarisha uhai wetu. (Mwanzo 3:21; 9:3; Kutoka 21:28) Hata hivyo, hatupaswi kuwatesa wanyama au kuwaua ili kujifurahisha tu.—Methali 12:10.

HESHIMU UTAKATIFU WA DAMU

10 Damu ni takatifu machoni pa Yehova kwa sababu inawakilisha uhai. Baada ya Kaini kumuua Abeli, Yehova alimwambia hivi: "Damu ya ndugu yako inanililia kutoka katika udongo." (Mwanzo 4:10) Damu ya Abeli iliwakilisha uhai wake, na Yehova alimwadhibu Kaini kwa kumuua Abeli. Baada ya Gharika ya siku za Noa, Yehova alionyesha tena kwamba bado damu inawakilisha uhai. Yehova alimruhusu Noa na familia yake kuchinja wanyama kwa ajili ya chakula. Alise-

8. Tutafanya nini ili tusihatarishe uhai wetu na wa wengine?
9. Tunapaswa kuwatendea wanyama jinsi gani?
10. Tunajua jinsi gani kwamba damu huwakilisha uhai?

ma hivi: "Kila mnyama anayetembea ambaye yuko hai anaweza kuwa chakula chenu. Kama nilivyowapa mimea ya majani, nawapeni hao wote." Hata hivyo, Yehova aliwakataza jambo moja: "Isipokuwa tu nyama pamoja na nafsi yake—damu yake—msile."—Mwanzo 1: 29; 9:3, 4.

11 Miaka 800 hivi baada ya Yehova kumwambia Noa asile damu, aliwaamuru watu wake hivi: "Na mtu yeyote kati ya wana wa Israeli au mkaaji mgeni yeyote anayekaa akiwa mgeni katikati yenu ambaye katika kuwinda anamkamata mnyama-mwitu au ndege anayeweza kuliwa, basi ataimwaga damu yake na kuifunika kwa mavumbi." Kisha akaongeza hivi: "Hamtakula damu." (Mambo ya Walawi 17:13, 14) Yehova bado alitaka watu wake waione damu kuwa takatifu. Waliruhusiwa kula nyama lakini si damu. Walipomchinja mnyama kwa ajili ya chakula, walipaswa kumwaga damu yake.

12 Miaka michache baada ya Yesu kufa, mitume na wazee wa kutaniko la Kikristo huko Yerusalemu walikutana ili waamue amri walizopewa Waisraeli ambazo bado Wakristo walihitaji kushika. **(Soma Matendo 15:28, 29;** 21:25.) Yehova aliwasaidia waelewe kwamba bado damu ilikuwa yenye thamani kwake, nao walipaswa kuiheshimu. Wakristo wa mapema hawakula au kunywa damu wala kula nyama ya mnyama aliyenyongwa au kibudu. Lilikuwa kosa kula au kunywa damu kama tu kuabudu sanamu au kufanya uasherati. Tangu wakati huo na kuendelea, Wakristo wa kweli hukataa kula au kunywa damu. Namna gani leo? Yehova bado anataka tuiheshimu damu kwa sababu ni takatifu.

---

11. Mungu aliwapa Waisraeli sheria gani kuhusu damu?
12. Wakristo wana maoni gani kuhusu damu?

13 Je, hilo linamaanisha kwamba Wakristo wanapaswa kukataa kutiwa damu mishipani? Ndiyo. Yehova ametuamuru tusile au kunywa damu. Ikiwa daktari angekwambia usinywe pombe, je, ungejitia pombe hiyo mishipani? Bila shaka hapana! Vivyo hivyo, amri ya kutokula au kunywa damu inamaanisha kwamba hatutakubali kutiwa mishipani.—Soma Maelezo ya Ziada 29.

14 Namna gani ikiwa daktari atasema kwamba tutakufa tusipotiwa damu mishipani? Ni lazima kila mtu afanye uamuzi wake mwenyewe inapohusu kutii sheria ya Mungu kuhusu damu. Wakristo huheshimu sana uhai ambao ni zawadi kutoka kwa Mungu, nasi hutafuta matibabu mengine yasiyohusisha damu; hata hivyo, hatutakubali kutiwa damu mishipani.

15 Kwa kuwa uhai ni wenye thamani machoni pa Mungu, sisi hujitahidi kudumisha afya lakini hatutakubali kutiwa damu mishipani ili kuendeleza uhai. Ni muhimu sana kumtii Yehova badala ya kutafuta njia nyingine zinazopingana na amri yake ili tu kuokoa uhai wetu. Yesu alisema: "Yeyote yule anayetaka kuiokoa nafsi yake ataipoteza; lakini yeyote yule anayeipoteza nafsi yake kwa ajili yangu ataipata." (Mathayo 16:25) Tunataka kumtii Yehova kwa sababu tunampenda. Naye anajua mambo yanayotufaa na kama Yehova, tunauthamini uhai na kuuona kuwa mtakatifu. —Waebrania 11:6.

16 Watumishi waaminifu wa Mungu wameazimia kutii amri ya Mungu kuhusu damu. Hawali au kunywa

---

13. Kwa nini Wakristo hukataa kutiwa damu mishipani?
14, 15. Kwa nini ni muhimu kwa Wakristo kuheshimu uhai na kumtii Yehova?
16. Watumishi wa Mungu wana uhakika kuhusu jambo gani?

damu, na pia hawakubali kuitumia kwa ajili ya matibabu.* Hata hivyo, wao hukubali matibabu ya aina nyingine ili kuokoa uhai. Wana uhakika kwamba Muumba wa uhai anajua mambo yenye faida kwao. Je, unaamini hivyo?

MATUMIZI PEKEE YA DAMU AMBAYO YEHOVA ALIKUBALI

17 Yehova aliwaambia hivi Waisraeli katika sheria aliyompa Musa: "Nafsi ya mwili iko katika damu, nami mwenyewe nimeiweka juu ya madhabahu ili ninyi mfanye upatanisho [ili kupata msamaha] kwa ajili ya nafsi zenu, kwa sababu damu ndiyo hufanya upatanisho." (Mambo ya Walawi 17:11) Waisraeli walipofanya dhambi, wangemwomba Yehova msamaha kwa kutoa dhabihu ya mnyama na kumwomba kuhani amwage kiasi fulani cha damu kwenye madhabahu hekaluni. Yehova alikubali Waisraeli watumie damu kwa ajili ya dhabihu pekee.

18 Yesu alipokuja duniani, alibadili sheria ya kutoa dhabihu za wanyama kwa kutoa uhai au damu yake, ili tupate msamaha wa dhambi zetu. (Mathayo 20:28; Waebrania 10:1) Uhai wa Yesu ulikuwa wenye thamani kubwa ndiyo sababu baada ya kufufuliwa na kurudi mbinguni, Yehova angewapa wanadamu wote fursa ya kuishi milele.—Yohana 3:16; Waebrania 9:11, 12; 1 Petro 1:18, 19.

---

* Ili kupata habari zaidi kuhusu kutiwa damu mishipani soma kitabu "*Jitunzeni Katika Upendo wa Mungu,*" ukurasa wa 77-79, kilichochapishwa na Mashahidi wa Yehova.

---

17. Katika taifa la Israeli, Yehova alikubali damu itumiwe kwa kusudi gani pekee?
18. Dhabihu ya Yesu hutuwezesha kupata nini?



Unaweza kuonyesha jinsi gani kwamba unaheshimu uhai na damu?

19 Tunamshukuru Yehova kwa sababu ya zawadi bora ya uhai. Tunataka kuwajulisha wengine kwamba wakimwamini Yesu, wanaweza kuishi milele. Tunawapenda, nasi tutafanya yote tuwezayo ili kuwafundisha jinsi wanavyoweza kupata uhai. (Ezekieli 3:17-21) Kisha, kama mtume Paulo, tutasema hivi: "Mimi ni safi kutokana na damu ya watu wote, kwa maana sikuepuka kuwaambia ninyi mashauri yote ya Mungu." (Matendo 20:26, 27) Naam, sisi huonyesha kwamba tunaheshimu uhai kwa kuwaeleza wengine kumhusu Yehova na jinsi anavyouona uhai kuwa ni wenye thamani.

19. Ni lazima tufanye nini ili tuwe "safi kutokana na damu ya watu wote"?

UKWELI WA 1 HESHIMU ZAWADI YA UHAI

"Kwa maana kwako wewe iko chemchemi ya uzima."—Zaburi 36:9

Tunaonyesha jinsi gani kwamba tunaheshimu uhai?

Matendo 17:28; Ufunuo 4:11
Uhai ni zawadi kutoka kwa Yehova, na tunapaswa kuuheshimu.

Kutoka 21:22, 23; Kumbukumbu la Torati 5:17
Ni kosa kuua na kutoa mimba.

1 Yohana 3:11, 12, 15
Ni dhambi kuwachukia wengine.

2 Wakorintho 7:1
Epuka tabia mbaya, kama vile kuvuta sigara na dawa kulevya.

Zaburi 11:5
Epuka michezo na burudani zenye jeuri.

UKWELI WA 2 UHAI NA DAMU

"Kwa maana nafsi ya kila namna ya mwili ni damu yake kwa nafsi iliyo ndani yake."—Mambo ya Walawi 17:14

Mungu anauonaje uhai na damu?

Mwanzo 4:10; Kumbukumbu la Torati 12:23
Damu inawakilisha uhai.

Mwanzo 9:3, 4
Tunaweza kula nyama lakini si damu.

Matendo 15:28, 29; 21:25
Amri ya Mungu ya kujiepusha na damu inahusu pia kutoitumia kwa matibabu.

Waebrania 11:6
Uhusiano wetu na Yehova ndilo jambo muhimu sana maishani mwetu.

UKWELI WA 3 MATUMIZI YA DAMU AMBAYO YEHOVA ALIRUHUSU

"Damu ya Yesu . . . hutusafisha kutoka katika dhambi yote."—1 Yohana 1:7

Dhabihu ya Yesu inafanya jambo gani liwezekane kwa ajili yetu?

Mambo ya Walawi 17:11
Nyakati za Biblia, Waisraeli walipotenda dhambi wangeomba msamaha wa Yehova kwa kutoa dhabihu ya mnyama na kumwomba kuhani amwage damu ya mnyama huyo kwenye madhabahu.

Mathayo 20:28; Waebrania 9:11-14
Yesu alipokuja duniani, alibadilisha sheria ya kutoa dhabihu za wanyama, kwa kutoa uhai wake au damu kwa ajili ya msamaha wa dhambi zetu.

Yohana 3:16
Uhai wa Yesu ulikuwa na thamani sana hivi kwamba baada ya Yehova kumfufua Yesu kwenda mbinguni, Yehova aliwapa wanadamu wote wanaomwamini Yesu fursa ya kuishi milele.

JINSI FAMILIA YAKO INAVYOWEZA KUWA NA FURAHA

YEHOVA Mungu alianzisha ndoa ya kwanza. Biblia inasema kwamba alimuumba mwanamke wa kwanza na "kumleta kwa huyo mwanamume." Adamu alifurahi sana, naye akasema hivi: "Mwishowe huyu ni mfupa wa mifupa yangu na nyama ya nyama yangu." (Mwanzo 2:22, 23) Jambo hilo linaonyesha kwamba Yehova anataka wale waliofunga ndoa wawe na furaha.

2 Kwa kusikitisha, familia nyingi leo hazina furaha. Hata hivyo, Biblia ina kanuni zinazoweza kumsaidia kila mtu katika familia atimize majukumu yake na kufurahia kuwa pamoja.—Luka 11:28.

MUNGU ANATARAJIA WAUME WAFANYE NINI?

3 Biblia inasema kwamba mume mzuri anapaswa kumpenda na kumheshimu mke wake. Tafadhali, **soma Waefeso 5:25-29.** Sikuzote mume anamtendea mke wake kwa upendo. Pia anamlinda, anamtunza, na hatafanya jambo lolote lenye kumuumiza.

4 Mume anapaswa kufanya nini mke wake akikosea? Biblia inawashauri waume hivi: "**Endeleeni** kuwapenda wake zenu nanyi msiwakasirikie kwa uchungu." (Wakolosai 3:19) Waume, kumbukeni kwamba ninyi pia hufanya makosa. Ikiwa unataka Mungu

1, 2. Yehova anataka familia ziwe na hali gani?
3, 4. (a) Mume anapaswa kumtendea mke wake jinsi gani? (b) Kwa nini ni muhimu kwa mume na mke kusameheana kwa hiari?

akusamehe, unapaswa kumsamehe mke wako. (Mathayo 6:12, 14, 15) Mume na mke wataifurahia sana ndoa ikiwa wanasameheana kwa hiari.

5 Yehova anatazamia mume amheshimu mke wake. Mume anapaswa kuzingatia mahitaji ya mke wake. Hilo ni jambo zito sana. Ikiwa mume anamtendea vibaya mke wake, Yehova hatasikiliza sala zake. (1 Petro 3:7) Yehova anawathamini watu wote wanaompenda. Hawaoni wanaume kuwa ni bora kuliko wanawake.

6 Yesu alisema kwamba mume na mke "si wawili tena, bali **mwili mmoja.**" (Mathayo 19:6) Wanapaswa kuwa waaminifu kwa mmoja na mwenzake. (Methali 5:15-21; Waebrania 13:4) Mume na mke wanapaswa kutimiziana mahitaji yao ya ngono. (1 Wakorintho 7: 3-5) Mume anapaswa kukumbuka kwamba "hakuna mtu anayeuchukia **mwili wake kwa vyovyote, bali huulisha na kuutunza kwa upendo.**" Hivyo, anapaswa kumpenda na kumtunza mke wake. Zaidi ya yote, mke anahitaji mume wake ampende na kumtendea kwa fadhili.—Waefeso 5:29.

MUNGU ANATARAJIA WAKE WAFANYE NINI?

7 Kila familia inahitaji kuwa na kichwa anayeiongoza ili mambo yafanyike kwa mpango. Biblia inasema hivi katika 1 Wakorintho 11:3: "Kichwa cha kila mwanamume ni Kristo, nacho kichwa cha mwanamke ni mwanamume, nacho kichwa cha Kristo ni Mungu."

---

5. Kwa nini mume anapaswa kumheshimu mke wake?
6. Ni nini maana ya mume na mke kuwa "mwili mmoja"?
7. Kwa nini familia inahitaji kuwa na kichwa?



Kwa nini Sara ni mfano mzuri kwa wanawake?

8 Hata waume hukosea. Lakini ikiwa mke anaunga mkono maamuzi ya mume wake na kushirikiana naye kwa hiari, familia nzima inanufaika. (1 Petro 3:1-6) Biblia inasema: "Mke anapaswa kumheshimu sana mume wake." (Waefeso 5:33) Namna gani ikiwa mume si mwamini? Bado mke ana wajibu wa kumheshimu. Biblia inasema hivi: "Ninyi wake, jitiisheni kwa waume zenu wenyewe, ili, ikiwa wowote si watiifu kwa lile neno, wavutwe bila neno kupitia mwenendo wa wake zao, kwa sababu wamekwisha kushuhudia kwa macho mwenendo wenu ulio safi kiadili pamoja na **heshima kubwa.**" (1 Petro 3:1, 2) Mfano mzuri wa mke unaweza kumsaidia mume wake akubali na kuheshimu imani ya mke wake.

9 Mke anaweza kufanya nini ikiwa hakubaliani na wazo fulani la mume wake? Anaweza kueleza maoni yake kwa heshima. Kwa mfano, wakati fulani

---

8. Mke anaweza kuonyesha heshima kwa mume wake jinsi gani?
9. (a) Mke anapaswa kufanya nini ikiwa hakubaliani na wazo fulani la mume wake? (b) Wake wanashauriwa nini katika andiko la Tito 2: 4, 5?

Abrahamu hakupendezwa na maoni ya Sara, lakini Yehova alimwambia hivi: "Sikiliza sauti yake." (Mwanzo 21:9-12) Mke anapaswa kuunga mkono maamuzi yote ya mume wake ikiwa hayavunji kanuni za Biblia. (Matendo 5:29; Waefeso 5:24) Mke bora anatunza familia yake. **(Soma Tito 2:4, 5.)** Mume na watoto wanapoona akifanya kazi kwa bidii, watampenda na kumheshimu sana.—Methali 31:10, 28.

10 Nyakati fulani kuna hali zinazoweza kufanya wenzi wa ndoa watengane au kutalikiana. Hata hivyo, Biblia inasema kwamba "mke hapaswi kuondoka kwa mume wake" na "mume hapaswi kumwacha mke wake." (1 Wakorintho 7:10, 11) Huenda kutokana na matatizo fulani mazito wenzi wa ndoa wakaamua kutengana, hata hivyo huo ni uamuzi mzito. Namna gani kuhusu talaka? Biblia inasema kwamba sababu pekee inayoweza kufanya mume au mke watalikiane ni uasherati.—Mathayo 19:9.

MUNGU ANATARAJIA WAZAZI WAFANYE NINI?

11 Wazazi, tumieni wakati mwingi iwezekanavyo pamoja na watoto wenu. Watoto wanawahitaji ninyi wazazi zaidi ya kitu kingine chochote, wanahitaji muwafundishe kumhusu Yehova.—Kumbukumbu la Torati 6:4-9.

12 Ulimwengu wa Shetani umekuwa mwovu sana, pia kuna baadhi ya watu ambao wanataka kuwadhuru watoto wetu, kwa kuwatendea vibaya kingono. Ni vigumu kwa baadhi ya wazazi kuwafundisha watoto

10. Biblia inasema nini kuhusu kutengana na talaka?
11. Watoto wanahitaji nini kutoka kwa wazazi?
12. Wazazi wanapaswa kufanya nini ili kuwalinda watoto wao?

wao kuhusu ngono. Hata hivyo, wazazi wanapaswa kuwaonya watoto wao kuhusu watu hao wabaya na kuwafundisha jinsi ya kuwaepuka. Wazazi, mnapaswa kuwalinda watoto wenu.*—1 Petro 5:8.

13 Wazazi wana wajibu wa kuwafundisha watoto wao tabia nzuri. Unaweza kuwafundisha watoto wako tabia nzuri jinsi gani? Watoto wako wanahitaji nidhamu, lakini nidhamu haipaswi kutolewa kwa ukatili.

* Unaweza kupata habari zaidi kuhusu jinsi ya kuwalinda watoto wako katika kitabu *Jifunze kutoka kwa Mwalimu Mkuu,* sura ya 32, kilichochapishwa na Mashahidi wa Yehova.

13. Wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao jinsi gani?

Yesu ni mfano mzuri kwa kila mshiriki wa familia



(Yeremia 30:11) Kwa hiyo, usimwadhibu mtoto wako unapokuwa na hasira. Usitumie maneno makali kama "upanga unaochoma" ambayo yatawaumiza. (Methali 12:18) Wafundishe watoto wako umuhimu wa kutii.—Waefeso 6:4; Waebrania 12:9-11; soma Maelezo ya Ziada 30.

MUNGU ANATARAJIA WATOTO WAFANYE NINI?

14 Yesu alimtii Baba yake sikuzote, hata ilipokuwa vigumu kufanya hivyo. (Luka 22:42; Yohana 8:28, 29) Yehova anatarajia watoto wawatii wazazi wao.—Waefeso 6:1-3.

15 Watoto, hata mkihisi kwamba ni vigumu kuwatii wazazi wenu, kumbukeni kwamba mkiwa watiifu, mtamfurahisha Yehova na wazazi wenu.*—Methali 1:8; 6:20; 23:22-25.

16 Ibilisi anaweza kuwatumia rafiki zako na vijana wengine ili wakushawishi ufanye mambo mabaya. Anajua kwamba itakuwa vigumu kwako kuwapinga. Kwa mfano, Dina binti ya Yakobo alikuwa na marafiki ambao hawakumpenda Yehova. Urafiki huo ulisababisha matatizo mengi sana kwake na kwa familia yake. (Mwanzo 34:1, 2) Ikiwa rafiki zako hawampendi Yehova, wanaweza kukushawishi ufanye mambo yanayomchukiza, hivyo kukuumiza wewe, familia yako, na Mungu. (Methali 17:21, 25) Kwa kweli, ni muhimu

* Mtoto anaweza kukataa ikiwa mzazi anataka avunje sheria za Mungu.—Matendo 5:29.

14, 15. Kwa nini watoto wanapaswa kuwatii wazazi wao?
16. (a) Shetani anatumia njia gani kuwashawishi vijana wafanye mambo mabaya? (b) Kwa nini ni muhimu kuchagua marafiki wanaompenda Yehova?

kutafuta marafiki wanaompenda Yehova.—1 Wakorintho 15:33.

FAMILIA YAKO INAWEZA KUWA NA FURAHA

17 Washiriki wa familia wanapofuata mwongozo wa Mungu, wanaepuka matatizo mengi. Hivyo, ikiwa wewe ni mume mpende mke wako. Mke, unapaswa kumheshimu na kumtii mume wako, pia unapaswa kuiga mfano wa mke anayetajwa katika Methali 31:10-31. Ikiwa wewe ni mzazi, wafundishe watoto wako kumpenda Mungu. (Methali 22:6) Ikiwa wewe ni baba, ongoza familia yako "kwa njia nzuri." (1 Timotheo 3:4, 5; 5:8) Nanyi watoto, watiini wazazi wenu. (Wakolosai 3:20) Kumbuka kwamba kila mtu katika familia anaweza kukosea, hivyo uwe mnyenyekevu na kuwaomba wengine msamaha. Naam, Biblia ina mwongozo wa Yehova kwa ajili ya kila mtu katika familia.

17. Kila mmoja katika familia ana wajibu gani?



Ni nini kitakachowasaidia vijana kumtii Mungu wanaposhawishiwa kufanya mambo mabaya?

UKWELI WA 1 YEHOVA ALIANZISHA FAMILIA

"Kwa sababu hiyo nampigia Baba magoti, ambaye kila familia mbinguni na duniani hupata jina kutokana naye."—Waefeso 3:14, 15

Jinsi familia yako inavyoweza kuwa na furaha.

Mwanzo 1:26-28
Yehova alianzisha familia ya kwanza.

Waefeso 5:1, 2
Ufunguo wa kuwa na maisha ya familia yenye furaha ni kumwiga Yehova na Yesu.

UKWELI WA 2 JINSI YA KUWA MUME AU MKE BORA

"Kila mtu mmoja-mmoja kati yenu na ampende hivyo mke wake . . . Mke anapaswa kumheshimu sana mume wake."—Waefeso 5:33

Mume na mke wanapaswa kutendeana jinsi gani?

Waefeso 5:22-29
Mume ni kichwa cha familia. Anapaswa kumpenda mke wake naye mke anapaswa kuunga mkono maamuzi ya mume wake.

Wakolosai 3:19; 1 Petro 3:4
Wanapaswa kutendeana kwa fadhili na ufikirio.

1 Petro 3:1, 2, 7
Mume na mke wanapaswa kuheshimiana.

1 Timotheo 5:8; Tito 2:4, 5
Mume anapaswa kuiandalia familia yake. Mke anapaswa kuitunza nyumba yake kwa njia inayofaa.

UKWELI WA 3 JINSI YA KUWA MZAZI BORA

"Msiwe mkiwakasirisha watoto wenu, bali endeleeni kuwalea katika nidhamu na mwongozo wa akilini wa Yehova."—Waefeso 6:4

Wazazi wana wajibu gani?

Kumbukumbu la Torati 6:4-9; Methali 22:6
Tenga wakati wa kuwafundisha watoto wako kumhusu Yehova. Anza wakiwa wachanga na uwasaidie kuwa rafiki za Yehova.

1 Petro 5:8
Wafundishe watoto wako jinsi wanavyoweza kuepuka kutendewa vibaya kingono na hatari zingine.

Yeremia 30:11; Waebrania 12:9-11
Unapaswa kuwatia nidhamu watoto wako, lakini si kwa hasira au kwa ukatili.

UKWELI WA 4 MUNGU ANATAZAMIA WATOTO WAFANYE NINI?

"Enyi watoto, watiini wazazi wenu."—Waefeso 6:1

Watoto, kwa nini mnapaswa kuwatii wazazi wenu?

Methali 23:22-25; Wakolosai 3:20
Unapotii utamfurahisha Yehova na wazazi wako.

1 Wakorintho 15:33
Uwe rafiki wa wale wanaompenda Yehova. Hivyo, itakuwa rahisi kwako kutenda yaliyo mema.

JINSI YA KUMWABUDU MUNGU KWA NJIA INAYOFAA

DINI nyingi zinadai kwamba zinafundisha ukweli kumhusu Mungu. Hata hivyo, si kweli, kwa sababu dini hizo zinafundisha mambo tofauti kabisa kuhusu Mungu na jinsi tunavyopaswa kumwabudu. Tunaweza kujua jinsi gani njia inayofaa ya kumwabudu Mungu? Yehova pekee ndiye anayeweza kutufundisha jinsi tunavyopaswa kumwabudu.

2 Yehova ametupatia Biblia ili tujifunze jinsi ya kumwabudu kwa njia inayofaa. Kwa hiyo, jifunze Biblia, unapofanya hivyo Yehova atakusaidia ufaidike na mafundisho yake kwa sababu anakupenda sana.—Isaya 48:17.

3 Baadhi ya watu husema kwamba Mungu hukubali dini zote, hata hivyo Yesu hakutufundisha hivyo. Alisema hivi: "Si kila mtu anayeniambia, 'Bwana, Bwana,' atakayeingia katika ufalme wa mbinguni, bali yule anayefanya mapenzi ya Baba yangu." Kwa hiyo, ni muhimu sana tujifunze na kuyafanya mapenzi ya Mungu. Hilo ni jambo zito kwani Yesu aliwalinganisha watu wasiomtii Mungu kuwa sawa na wahalifu "wenye matendo ya uasi-sheria."—Mathayo 7:21-23.

4 Yesu alisema kwamba tukitaka kufanya mapenzi ya

---

1. Ni nani anayepaswa kutufundisha jinsi ya kumwabudu Mungu?
2. Unaweza kujifunza jinsi gani kumwabudu Mungu kwa njia inayofaa?
3. Mungu anataka tufanye nini?
4. Yesu alisema nini kuhusu kufanya mapenzi ya Mungu?

Mungu, tutakabili upinzani. Alisema hivi: "Ingieni kupitia lango jembamba; kwa sababu barabara inayoongoza kwenye uharibifu ni pana na kubwa, na wengi ndio wanaoipitia; lakini lango ni jembamba na barabara inayoongoza kwenye uzima ina nafasi ndogo, na wachache ndio wanaoipata." (Mathayo 7:13, 14) Barabara nyembamba, au njia inayofaa ya kumwabudu Mungu, inaongoza kwenye uzima wa milele. Barabara pana au njia isiyofaa ya kumwabudu Mungu inaongoza kwenye uharibifu. Hata hivyo, Yehova hataki mtu yeyote aangamizwe. Anampa kila mtu fursa ya kujifunza kumhusu yeye.—2 Petro 3:9.

JINSI YA KUMWABUDU MUNGU KWA NJIA INAYOFAA

5 Yesu alisema kwamba inawezekana kuwatambua wale wanaomwabudu Mungu kwa njia inayofaa. Tunaweza kufanya hivyo kwa kuchunguza yale wanayoamini na kutenda. Alisema hivi: "Kwa matunda yao mtawatambua." Kisha akaongeza: "Kila mti mzuri huzaa matunda mazuri." (Mathayo 7:16, 17) Hilo halimaanishi kwamba wale wanaomwabudu Mungu ni wakamilifu. Hata hivyo, watumishi wa Mungu wanajitahidi kufanya yaliyo sawa. Sasa tutachunguza mambo yatakayotusaidia kuwatambua wale wanaomwabudu Mungu kwa njia inayofaa.

6 **Ibada yetu inapaswa kutegemea Biblia.** Biblia inasema: "Andiko lote limeongozwa na roho ya Mungu nalo ni lenye faida kwa kufundisha, kwa kukaripia, kwa kunyoosha mambo, kwa kutia nidhamu

---

5. Unaweza kuwatambua jinsi gani wale wanaomwabudu Mungu kwa njia inayofaa?

6, 7. Kwa nini ibada ya kweli inategemea Biblia? Mfano wa Yesu unatufundisha nini?

katika uadilifu, ili mtu wa Mungu awe na uwezo kamili, akiwa na vifaa kamili kwa ajili ya kila kazi njema." (2 Timotheo 3:16, 17) Mtume Paulo aliwaandikia Wakristo hivi: "Mlipolipokea neno la Mungu, ambalo mlilisikia kutoka kwetu, mlilikubali, si kama neno la wanadamu, bali, kama vile lilivyo kwa kweli, kama neno la Mungu." (1 Wathesalonike 2:13) Ibada ya kweli inategemea Biblia neno la Mungu. Haitegemei mawazo ya wanadamu, utamaduni, au jambo lingine lolote.

7 Mambo yote ambayo Yesu alifundisha yalitegemea Neno la Mungu. **(Soma Yohana 17:17.)** Mara nyingi alinukuu Maandiko. (Mathayo 4:4, 7, 10) Waabudu wa kweli wa Mungu wanafuata mfano wa Yesu na kila jambo wanalofundisha linategemea Biblia.

8 Tunapaswa kumwabudu Yehova Pekee. Zaburi 83:18 husema hivi: "Wewe, ambaye jina lako ni Yehova, Wewe peke yako ndiye Uliye Juu Zaidi, juu ya dunia yote." Yesu alitaka watu wamjue Mungu wa kweli, naye aliwafundisha jina la Mungu. **(Soma Yohana 17:6.)** Yesu alisema: "Yehova Mungu wako ndiye unayepaswa kumwabudu, na yeye peke yake ndiye unayepaswa kumtolea utumishi mtakatifu." (Mathayo 4:10) Hivyo, tukiwa watumishi wa Mungu tunafuata mfano wa Yesu. Tunamwabudu Yehova peke yake, tunatumia jina lake, na tunawafundisha wengine jina la Mungu na yale atakayotufanyia wakati ujao.

9 Tunapaswa Kuwapenda watu. Yesu aliwafundisha wanafunzi wake wapendane. **(Soma Yohana 13:35.)** Tunapendana licha ya kwamba tunatofautiana uta-

---

8. Yesu alitufundisha nini kuhusu kumwabudu Yehova?

9, 10. Tunaweza kuonyesha jinsi gani kwamba tunawapenda wengine?

maduni au kipato. Upendo unapaswa kutuunganisha kuwa ndugu na dada. (Wakolosai 3:14) Kwa sababu hiyo hatushiriki vita wala kuua watu. Biblia inasema: "Watoto wa Mungu na watoto wa Ibilisi ni wazi kwa jambo hili: Kila mtu ambaye haendelei kufanya uadilifu hatokani na Mungu, wala yeye ambaye hampendi ndugu yake." Pia inaongezea hivi: "Tunapaswa kupendana; si kama Kaini, aliyetokana na yule mwovu akamuua ndugu yake."—1 Yohana 3:10-12; 4:20, 21.

10 Tunatumia wakati, nguvu, na mali zetu ili kusaidiana na kutiana moyo. (Waebrania 10:24, 25) 'Tunawatendea wote mema.'—Wagalatia 6:10.

11 Tunapaswa kumtii Yesu kwa kuwa yeye ndiye njia inayotuongoza kwa Mungu. Biblia inasema: "Hakuna wokovu katika mwingine yeyote, kwa maana hakuna jina lingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu ambalo kupitia hilo lazima sisi tupate kuokolewa." (Matendo 4:12) Katika sura ya 5 ya kitabu hiki, tulijifunza kwamba Yehova alimtuma Yesu aje atoe uhai wake ukiwa fidia kwa ajili ya wanadamu watiifu. (Mathayo 20:28) Yehova amemchagua Yesu atawale akiwa Mfalme wa dunia. Ndiyo sababu Biblia hutuambia kwamba ni lazima tumtii Yesu ikiwa tunataka kuishi milele. **—Soma Yohana 3:36.**

12 Hatupaswi kujihusisha na siasa. Yesu hakujihusisha na siasa. Kesi yake ilipokuwa ikisikilizwa, alimwambia Pilato, mtawala wa Roma hivi: "Ufalme wangu si sehemu ya ulimwengu huu." **(Soma Yohana 18:36.)** Kama Yesu, tunashikamana na Ufalme wa Mungu,

---

11. Kwa nini tunaamini kwamba Yesu ndiye njia inayotuongoza kwa Mungu?
12. Kwa nini hatujihusishi na siasa?

hivyo hatujihusishi na siasa. Hata hivyo, Biblia inatuamuru tutii "mamlaka zilizo kubwa," yaani, serikali. (Waroma 13:1) Tunatii sheria za nchi. Hata hivyo, sheria za wanadamu zinapopingana na sheria za Mungu, tunaiga mfano wa mitume, ambao walisema hivi: "Lazima tumtii Mungu kuwa mtawala kuliko wanadamu." —Matendo 5:29; Marko 12:17.

13 Tunaamini kwamba Ufalme wa Mungu ndio suluhisho la pekee kwa matatizo ya ulimwengu. Yesu alisema kwamba, "habari njema ya ufalme" itahubiriwa katika dunia yote. **(Soma Mathayo 24:14.)** Hakuna serikali ya wanadamu inayoweza kufanya mambo ambayo Ufalme wa Mungu utafanya. (Zaburi 146:3) Yesu alitufundisha tusali kuhusu Ufalme wa Mungu aliposema hivi: "Ufalme wako na uje. Mapenzi yako na yatendeke duniani kama ilivyo mbinguni." (Mathayo 6: 10) Biblia inatueleza kwamba Ufalme wa Mungu utaziharibu serikali zote za wanadamu, "nao utasimama mpaka wakati usio na kipimo."—Danieli 2:44.

14 Baada ya kujifunza mambo hayo, jiulize: 'Ni nani ambao mafundisho yao hutegemea Biblia? Ni nani wanaowafundisha wengine jina la Mungu? Ni nani ambao wana upendo wa kweli na wanaamini kwamba Mungu alimtuma Yesu ili atukomboe? Ni nani ambao hawajihusishi na siasa? Ni nani wanaohubiri kwamba Ufalme wa Mungu pekee ndio unaoweza kuondoa matatizo yetu?' Ni Mashahidi wa Yehova pekee.—Isaya 43:10-12.

UNAHITAJI KUFANYA NINI?

15 Haitoshi tu kuamini kwamba kuna Mungu. Hata

13. Tunahubiri ujumbe gani kuhusu Ufalme wa Mungu?
14. Ni nani wanaomwabudu Mungu kwa njia inayofaa?
15. Ni lazima tufanye nini ikiwa tunataka Mungu akubali ibada yetu?

WALE WANAOMWABUDU MUNGU

- mafundisho yao hutegemea Biblia
- wanamwabudu Yehova pekee, na kuwafundisha wengine jina lake
- wanapendana
- wanaamini kwamba Mungu alimtuma Yesu ili atukomboe
- hawajihusishi na siasa
- wanahubiri kwamba Ufalme wa Mungu ndio suluhisho pekee la matatizo yanayowakabili wanadamu



roho waovu wanaamini kwamba kuna Mungu, lakini hawamtii. (Yakobo 2:19) Ikiwa tunataka Mungu akubali ibada yetu, hatupaswi tu kuamini kwamba yupo, bali tunapaswa kufanya mapenzi yake.

16 Ili Mungu akubali ibada yetu, lazima tuache kushirikiana na dini za uwongo. Nabii Isaya aliandika hivi: "Tokeni katikati yake, jiwekeni safi." (Isaya 52:11; 2 Wakorintho 6:17) Hiyo ndiyo sababu tunahitaji kukataa kila kitu kinachohusiana na ibada ya uwongo.

17 Dini za uwongo ni zipi? Ni dini zote zinazofundisha kinyume na Neno Mungu. Biblia inaziita dini zote za uwongo "Babiloni Mkubwa." (Ufunuo 17:5) Kwa nini? Baada ya gharika ya siku za Noa, mafundisho mengi ya dini za uwongo yalianzia katika jiji la Babiloni. Mafundisho hayo ya uwongo yalienea katika dunia yote. Kwa mfano, watu wa Babiloni waliabudu kikundi cha miungu watatu. Leo, dini nyingi zinafundisha kwamba Mungu ni Utatu. Lakini Biblia inafundisha wazi kwamba kuna Mungu mmoja tu wa kweli, Yehova, na kwamba Yesu ni Mwana wake. (Yohana 17:3) Pia, Wababiloni waliamini kwamba kitu fulani huendelea kuishi baada ya mwili kufa na kwamba huteseka katika moto wa mateso. Fundisho hilo ni la uwongo.—Soma Maelezo ya Ziada 14, 17, na 18.

18 Mungu ametabiri kwamba hivi karibuni dini zote za uwongo zitaharibiwa. (Ufunuo 18:8) Je, unaelewa kwa nini ni muhimu utoke haraka katika dini za uwongo? Yehova Mungu anataka ufanye hivyo kabla haijawa kuchelewa mno.—Ufunuo 18:4.

---

16. Kwa nini tuache kushirikiana na dini za uwongo?

17, 18. "Babiloni Mkubwa" ni nini, na kwa nini ni muhimu utoke kwake?

19 Unapoamua kuacha dini za uwongo na kuanza kumtumikia Yehova, huenda baadhi ya rafiki au watu wa familia wasikubaliane na uamuzi wako na hata wanaweza kukupinga. Hata hivyo, Yehova hatakuacha. Utajiunga na familia kubwa yenye upendo wa kweli ya mamilioni ya watu ulimwenguni pote, pia utakuwa na tumaini la kuishi milele katika ulimwengu mpya wa Mungu. (Marko 10:28-30) Baadaye, huenda baadhi ya rafiki na watu wa familia ambao wanapinga uamuzi wako wa kumtumikia Yehova wakaamua kujifunza Biblia.

20 Hivi karibuni, Mungu atawaharibu watu waovu na Ufalme wake utatawala dunia. (2 Petro 3:9, 13) Huo utakuwa wakati mzuri sana! Sote tutamwabudu Yehova kwa njia anayokubali. Kwa hivyo, ni muhimu sana kwako kuamua sasa kumwabudu Mungu kwa njia inayofaa.

19. Yehova atafanya nini ukiamua kumtumikia?
20. Kwa nini ni muhimu kumwabudu Mungu kwa njia inayofaa?



Unapomtumikia Yehova pamoja na watu wake, utajiunga na familia ya ulimwenguni pote

UKWELI WA 1 JINSI YA KUITAMBUA IBADA YA KWELI

"Lango ni jembamba na barabara inayoongoza kwenye uzima ina nafasi ndogo, na wachache ndio wanaoipata."—Mathayo 7:14

Tunajua jinsi gani kwamba Mungu hakubali ibada zote?

Mathayo 7:21-23
Mungu hazikubali dini zote. Kwa kuwa sio dini zote zinazofanya mapenzi yake.

Mathayo 7:13, 14
Ibada ya kweli inaongoza kwenye uhai wa milele. Dini ya uwongo huongoza kwenye uharibifu wa milele.

Mathayo 7:16, 17
Unaweza kuitambua ibada ya kweli kwa matendo yake. Huhitaji kuchunguza dini zote; unachohitaji kufanya ni kujifunza yale ambayo Biblia inasema.

UKWELI WA 2 NJIA INAYOFAA YA KUMWABUDU MUNGU

---

1 Wathesalonike 2:13; 2 Timotheo 3:16, 17
Huamini na kufundisha yale ambayo Biblia husema.

Mathayo 4:10; Yohana 17:6
Humwabudu Yehova na kutumia jina lake.

Yohana 13:35
Wana upendo wa kweli.

Yohana 3:36; Matendo 4:12
Wanamtii Yesu. Wanaamini kwamba Mungu anamtumia Yesu ili kutuokoa.

Yohana 18:36; Matendo 5:29
Hawajihusishi na siasa.

Mathayo 24:14; 6:10
Wanawafundisha wengine kwamba Ufalme wa Mungu ndio suluhisho la matatizo yetu.

UKWELI WA 3

UNAPASWA KUISHI KULINGANA NA YALE UNAYOAMINI

Unapaswa kufanya nini ikiwa unataka Mungu aikubali ibada yako?

Yakobo 2:19
Haitoshi tu kumwamini Mungu. Unapaswa kufanya yale anayosema katika Biblia.

Isaya 52:11; Ufunuo 17:5
Dini ya uwongo, au "Babiloni Mkubwa," huwafundisha watu kinyume na Mungu anavyotaka wamwabudu. Mafundisho ya dini za uwongo hutia ndani Utatu, kutokufa kwa nafsi, na moto wa mateso.

Ufunuo 18:4, 8
Hivi karibuni Yehova ataziharibu dini zote za uwongo. Unapaswa kukataa kitu chochote kinachotokana na dini ya uwongo.

Marko 10:28-30
Huenda ukakabili upinzani hata hivyo, Yehova hatakuacha.

AMUA KUMWABUDU MUNGU

KUPITIA kujifunza Biblia, umetambua kwamba watu wengi wanaodai wanamwabudu Mungu hufundisha au kufanya mambo ambayo Mungu anachukia. (2 Wakorintho 6:17) Ndiyo sababu, Yehova anatuamuru tutoke katika dini za uwongo, yaani, "Babiloni Mkubwa." (Ufunuo 18:2, 4) Utafanya nini? Kila mtu anapaswa kufanya uamuzi na kujiuliza hivi, 'Je, nitamwabudu Mungu kulingana na mapenzi yake au nimwabudu jinsi nipendavyo?'

2 Umefanya vizuri ikiwa umeacha kushirikiana na dini ya uwongo. Hata hivyo, huenda ikawa vigumu kuacha baadhi ya mazoea na desturi fulani za dini za uwongo ambazo ulizoea. Hebu tuchunguze baadhi ya mazoea na desturi hizo na tuone umuhimu wa kuwa na maoni kama ya Yehova.

KUABUDU SANAMU NA MABABU

3 Kwa miaka mingi, baadhi ya watu wamekuwa na vihekalu katika nyumba zao au wametumia sanamu katika ibada. Ikiwa ulikuwa na mazoea hayo, huenda ukaona ni vigumu au ni kosa kumwabudu Mungu bila kutumia sanamu. Hata hivyo, kumbuka kwamba Yehova hutufundisha jinsi tunavyopaswa kumwabudu. Biblia inasema wazi kwamba Yehova hataki tutumie sana-

---

1, 2. Unapaswa kujiuliza swali gani, na kwa nini ni muhimu kufanya hivyo?

3. (a) Kwa nini huenda wengine wakaona ni vigumu kuacha kutumia sanamu katika ibada? (b) Biblia inasema nini kuhusu kutumia sanamu katika ibada?

mu katika ibada.—**Soma Kutoka 20:4, 5**; Zaburi 115: 4-8; Isaya 42:8; 1 Yohana 5:21.

4 Baadhi ya watu hutumia muda na nguvu nyingi ili kuwapendeza mababu zao waliokufa. Huenda hata wakawaabudu. Hata hivyo, tumejifunza kwamba wafu hawawezi kutusaidia au kutuumiza. Hawaendelei kuishi pahali pengine. Kwa kweli, ni hatari kujaribu kuwasiliana na wafu kwa sababu habari yoyote ambayo huenda tukafikiri inatoka kwa mpendwa wetu aliyekufa, inatoka kwa roho waovu. Ndiyo sababu, Yehova aliwaamuru Waisraeli wasiwasiliane na wafu au kujihusisha na ushirikina wa aina yoyote ile.—Kumbukumbu la Torati 18: 10-12; soma Maelezo ya Ziada 26 na 31.

5 Ni nini kitakachokusaidia kuacha kutumia sanamu katika ibada au kuabudu mababu waliokufa? Unapaswa kusoma Biblia na kutafakari kwa makini maoni ya Yehova kuhusu mambo hayo. Mambo hayo ni 'chukizo' kwake. (Kumbukumbu la Torati 27:15) Sali kwa Yehova kila siku ili akusaidie kuwa na maoni kama yake na umwabudu kwa njia inayofaa. (Isaya 55:9) Uwe na uhakika kwamba Yehova atakusaidia uache kabisa mazoea yote ya dini za uwongo.

JE, TUNAPASWA KUSHEREHEKEA KRISMASI?

6 Krismasi ni sikukuu maarufu sana ambayo husherehekewa duniani pote, na wengi huamini kwamba ni sherehe ya kukumbuka kuzaliwa kwa Yesu. Hata hivyo, Krismasi inatokana na ibada ya uwongo. Kitabu

4. (a) Kwa nini hatupaswi kuwaabudu mababu zetu waliokufa? (b) Kwa nini Yehova aliwakataza watu wake kuwasiliana na wafu?
5. Ni nini kitakachokusaidia kuacha kuabudu mababu waliokufa na kutumia sanamu katika ibada?
6. Kwa nini Desemba 25 ilichaguliwa kuwa siku ya kusherehekea kuzaliwa kwa Yesu?

kimoja cha ensaiklopedia kinasema kwamba Waroma wapagani walisherehekea kuzaliwa kwa jua Desemba 25. (Luka 2:8-12) Viongozi wa makanisa walitaka wapagani wengi wawe Wakristo, hivyo waliamua kusherehekea kuzaliwa kwa Yesu Desemba 25 ingawa Yesu hakuzaliwa tarehe hiyo. Wanafunzi wa Yesu hawakusherehekea Krismasi. Kitabu kimoja cha marejeo kinasema kwamba miaka 200 baada ya Yesu kuzaliwa, "hakuna mtu ambaye alijua siku hususa ambayo Yesu alizaliwa, na ni watu wachache tu ambao walitaka kujua." (*Sacred Origins of Profound Things*) Krismasi ilianza kusherehekewa miaka mingi baada ya Yesu kuishi duniani.

7 Watu wengi wanajua kwamba Krismasi na desturi zake kama vile sherehe za kupeana zawadi zilitokana na wapagani. Kwa mfano, wakati fulani nchini Uingereza na maeneo fulani ya Amerika, sikukuu ya Krismasi ilipigwa marufuku kwa sababu ya chanzo chake cha kipagani. Yeyote aliyesherehekea aliadhibiwa. Hata hivyo, baadaye watu walianza kusherehekea tena Krismasi. Kwa nini Wakristo wa kweli hawasherehekei Krismasi? Kwa sababu wanataka kumpendeza Mungu katika kila jambo wanalofanya.

JE, TUNAPASWA KUSHEREHEKEA SIKU ZA KUZALIWA?

8 Watu wengi pia husherehekea siku zao za kuzaliwa. Je, Wakristo wanapaswa kusherehekea siku za kuzaliwa? Sherehe pekee za kukumbuka siku za kuzaliwa zinazotajwa katika Biblia zilifanywa na watu ambao hawaku-

---

7. Kwa nini Wakristo wa kweli hawasherehekei Krismasi?

8, 9. Kwa nini Wakristo wa mapema hawakusherehekea siku za kuzaliwa?

mwabudu Yehova. (Mwanzo 40:20; Marko 6:21) Sherehe za siku za kuzaliwa zilifanywa ili kuheshimu miungu ya uwongo. Ndiyo sababu, Wakristo wa karne ya kwanza "waliona kusherehekea siku ya kuzaliwa kuwa ni desturi ya kipagani."—*The World Book Encyclopedia.*

9 Waroma na Wagiriki wa kale waliamini kwamba roho fulana ilikuwepo mtu alipozaliwa na ilimlinda maishani mwake. Kitabu *The Lore of Birthdays* kinasema hivi: "Roho hiyo ilikuwa na uhusiano wa kichawi na mungu ambaye siku yake ya kuzaliwa ililingana na siku ya kuzaliwa ya mtu huyo."

10 Je, unafikiri Yehova anakubali sikukuu ambazo zinahusiana na dini za uwongo? (Isaya 65:11, 12) Hapana. Hiyo ndiyo sababu hatusherehekei siku za kuzaliwa au sikukuu nyingine zinazohusiana na dini za uwongo.

JE, NI MUHIMU KUJUA CHANZO?

11 Ingawa baadhi ya watu wanajua kwamba Krismasi na sikukuu nyingine zilitokana na wapagani, bado wao huendelea kuzisherehekea. Wanafikiri kwamba sikukuu ni wakati mzuri wa kuwa pamoja na familia zao. Je, wewe una maoni hayo? Si vibaya kutenga wakati ili kuwa pamoja na familia yako. Yehova alianzisha familia, na angependa tuwe na uhusiano mzuri pamoja na familia. (Waefeso 3:14, 15) Hata hivyo, tunapaswa kuzingatia zaidi uhusiano wetu pamoja na Yehova kuliko kuwapendeza ndugu zetu kwa kusherehekea sikukuu zinazotokana na dini za uwongo. Ndiyo sababu mtume Paulo aliandika hivi: "Endeleeni kuhakikisha lile linalokubalika kwa Bwana."—Waefeso 5:10.

---

10. Kwa nini Wakristo hawapaswi kusherehekea siku za kuzaliwa?
11. Kwa nini baadhi ya watu husherehekea sikukuu? Unapaswa kuzingatia jambo gani?

12 Watu wengi hufikiri kwamba si muhimu kujua chanzo cha sikukuu, hata hivyo, hilo halipatani na maoni ya Yehova. Mungu hukataa sikukuu zinazotokana na dini za uwongo, zinazowatukuza wanadamu au nembo za taifa. Kwa mfano, Wamisri walikuwa na sherehe nyingi kwa ajili ya miungu yao ya uwongo. Baada ya Waisraeli kukombolewa kutoka Misri, waliiga sikukuu moja ya kipagani na kuiita "sherehe kwa ajili ya Yehova." Yehova aliwaadhibu kwa sababu ya kufanya hivyo. (Kutoka 32:2-10) Kama nabii Isaya alivyosema, hatupaswi 'kugusa kitu chochote kilicho najisi.'**—Soma Isaya 52:11.**

UWE MWENYE FADHILI UNAPOSHUGHILIKA NA WENGINE

13 Huenda ukajiuliza maswali mengi baada ya kuamua kuacha kusherehekea sikukuu fulani. Kwa mfano: Ninaweza kuwajibu jinsi gani wafanyakazi wenzangu wanaponiuliza kwa nini sisherehekei Krismasi pamoja nao? Ninaweza kufanya nini nikipewa zawadi ya Krismasi? Ninaweza kufanya nini ikiwa mwenzi wangu wa ndoa anataka tusherehekee sikukuu? Ninaweza kuwasaidia watoto wangu jinsi gani wasihisi vibaya kwa sababu hawasherehekei siku za kuzaliwa au sikukuu nyingine?

14 Ni muhimu kutumia hekima tunapoamua jinsi ya kushughulikia hali tofauti-tofauti tunazokabili. Kwa mfano, ikiwa mtu anakutakia heri ya sikukuu, hupaswi kumpuuza. Unaweza kusema, "Asante". Hata hivyo, ikiwa mtu angependa kujua zaidi kwa nini husherehekei sikukuu, usisite kumweleza. Pamoja na hayo, wakati wote

---

12. Kwa nini Yehova anazikataa sikukuu fulani?
13. Huenda ukajiuliza maswali gani baada ya kuamua kuacha kusherehekea sikukuu?
14, 15. Unaweza kufanya nini mtu fulani anapokutakia heri ya sikukuu au kukupatia zawadi?

uwe mwenye fadhili, busara na heshima. Biblia inasema hivi: "Maneno yenu na yawe yenye neema sikuzote, yenye kukolezwa chumvi, ili mjue jinsi mnavyopaswa kumjibu kila mtu." (Wakolosai 4:6) Huenda ikafaa kuwaeleza kwamba unapenda kushirikiana na wengine, hata kutoa na kupokea zawadi, lakini, ungependa kufanya hivyo wakati mwingine tofauti na wakati wa sikukuu.

15 Unaweza kufanya nini ikiwa mtu fulani anakupa zawadi? Biblia haina sheria kuhusu kila jambo, lakini inatuhimiza tudumishe dhamiri njema. (1 Timotheo 1: 18, 19) Huenda mtu anayekupa zawadi hajui kwamba wewe husherehekei sikukuu. Au huenda akasema hivi: "Ninajua kwamba husherehekei sikukuu, hata hivyo ningependa kukupatia zawadi." Ikitegemea hali, unaweza kuamua kukubali au kukataa zawadi hiyo. Lakini, jitahidi kudumisha dhamiri njema katika uamuzi unaofanya. Hatungependa kufanya jambo lolote lile ambalo litaharibu uhusiano wetu pamoja na Yehova.

WEWE NA FAMILIA YAKO

16 Unapaswa kufanya nini ikiwa watu wa familia yako wanataka kusherehekea sikukuu? Usiwakataze. Kumbuka kwamba wana haki ya kuamua mambo wanayotaka kufanya. Uwe mwenye fadhili na heshimu maoni yao kama vile ambavyo ungependa waheshimu maoni yako. **(Soma Mathayo 7:12.)** Hata hivyo, utafanya nini ikiwa watu wa familia wanataka ushirikiane nao wakati wa sikukuu? Kabla ya kuamua jambo la kufanya, sali kwa Yehova ili akusaidie kufanya uamuzi unaofaa. Fikiria hali hiyo, na ufanye utafiti. Kumbuka kwamba sikuzote, unataka kumpendeza Yehova.

16. Unapaswa kufanya nini ikiwa watu wa familia wanataka kusherehekea sikukuu?

17 Unaweza kufanya nini ili watoto wako wasihisi wamekosa kitu fulani kwa sababu ya kutosherehekea sikukuu? Mara kwa mara, pangeni kufanya mambo ambayo watafurahia. Pia, unaweza kuwafurahisha kwa kuwapatia zawadi. Mojawapo ya zawadi bora ambayo unaweza kuwapatia watoto wako ni kutenga wakati wa kuwa pamoja nao na kuwapenda.


SHIRIKIANA NA DINI YA KWELI

18 Ili tumpendeze Yehova, tunapaswa kuacha kushirikiana na dini za uwongo na kuepuka desturi na sikukuu za dini hizo. Pia, tunapaswa kushirikiana na dini ya kweli. Jinsi gani? Njia moja ni kwa kuhudhuria mikutano ya Kikristo kwa ukawaida. **(Soma Waebrania 10: 24, 25.)** Mikutano ni sehemu muhimu sana katika ibada ya kweli. (Zaburi 22:22; 122:1) Tunapokutana pamoja tunatiana moyo.—Waroma 1:12.

19 Njia nyingine ya kushirikiana na ibada ya kweli ni kuwaeleza wengine mambo ambayo umejifunza katika Biblia. Watu wengi wanahangaishwa na mambo mabaya yanayotendeka duniani. (Ezekieli 9:4) Huenda unawajua baadhi ya watu wanaohangaishwa na mambo hayo. Waeleze kuhusu tumaini zuri la wakati ujao. Kuhudhuria mikutano ya Kikristo na kuwaeleza wengine kweli za Biblia, kutakusaidia kushinda tamaa ya kushirikiana na dini ya uwongo pamoja na desturi zake. Uwe na uhakika kwamba utakuwa na furaha na Yehova atabariki jitihada zako za kumwabudu kwa njia inayofaa. —Malaki 3:10.

---

17. Unaweza kufanya nini ili kuwasaidia watoto wako wasihisi wamekosa kitu fulani kwa sababu ya kutosherehekea sikukuu?
18. Kwa nini tunapaswa kuhudhuria mikutano ya Kikristo?
19. Kwa nini ni muhimu kuwaeleza wengine kuhusu kweli za Biblia ambazo umejifunza?



Wale wanaomwabudu
Yehova wana furaha

UKWELI WA 1 EPUKA IBADA YA UWONGO

"Tokeni katikati yao, na mjitenge, . . . na mwache kugusa kitu kilicho najisi."—2 Wakorintho 6:17

Kwa nini ni kosa kuabudu mababu na sanamu?

Kutoka 20:4, 5; 1 Yohana 5:21
Yehova hataki tutumie sanamu katika ibada.

Kumbukumbu la Torati 18: 10-12
Wale wanaowasiliana na wafu, huwasiliana na roho waovu.

UKWELI WA 2 MUNGU HAKUBALI SHEREHE ZOTE

"Endeleeni kuhakikisha lile linalokubalika kwa Bwana."—Waefeso 5:10

Unahitaji kufanya nini ili kuamua ikiwa utashiriki katika sherehe fulani?

Ezekieli 44:23; 2 Wakorintho 6:14, 15
Chunguza ikiwa ina chanzo cha kipagani.

Kutoka 32:2-10
Hata kama wale wanaopanga sherehe wana nia nzuri, huenda sherehe hiyo isikubaliwe na Mungu.

Danieli 3:1-27
Epuka sherehe zinazowatukuza wanadamu, mashirika ya wanadamu, au nembo za taifa.

1 Timotheo 1:18, 19
Tumia busara, hata hivyo, dumisha dhamiri njema mbele za Yehova.

UKWELI WA 3

UWE MWENYE FADHILI UNAPOWAELEZA WENGINE IMANI YAKO

"Maneno yenu na yawe yenye neema sikuzote, yenye kukolezwa chumvi, ili mjue jinsi mnavyopaswa kumjibu kila mtu."—Wakolosai 4:6

Unaweza kuwaeleza wengine imani yako jinsi gani?

Mathayo 7:12
Heshimu maoni ya wengine kama vile ambavyo ungetaka waheshimu maoni yako.

2 Timotheo 2:24
Sikuzote uwe mwenye fadhili, na usigombane na wengine kwa sababu ya imani yako.

1 Petro 3:15
Tetea imani yako kwa upole na heshima.

Waebrania 10:24, 25
Katika mikutano ya Kikristo, utatiwa moyo na kusaidiwa kujua jinsi ya kutetea imani yako inapotiliwa shaka.

ZAWADI YA SALA

DUNIA ni ndogo sana inapolinganishwa na ulimwengu wote mzima. Hivyo, Yehova anapotazama dunia, watu katika mataifa yote huonekana kama tone dogo la maji katika ndoo. (Zaburi 115:15; Isaya 40:15) Hata hivyo, ingawa sisi tunaonekana kuwa wadogo sana tunapolinganishwa na ulimwengu wote mzima, andiko la Zaburi 145:18, 19 linasema hivi: "Yehova yuko karibu na wote wanaomwitia, wote wanaomwitia yeye katika ukweli. Atawatimizia wale wanaomwogopa tamaa yao, naye atakisikia kilio chao cha kuomba msaada, naye atawaokoa." Hiyo ni heshima kubwa sana! Yehova, Muumba mweza yote anataka tumkaribie, na anataka kusikiliza sala zetu. Naam, sala ni zawadi, ni zawadi ya pekee ambayo Yehova amempatia kila mmoja wetu.

2 Hata hivyo, Yehova atatusikiliza ikiwa tu tunasali kwa njia anayoikubali. Tunawezaje kusali kwa njia hiyo? Acheni tuone jinsi Biblia inavyosema kuhusu jambo hilo.

KWA NINI TUSALI KWA YEHOVA?

3 Yehova anataka usali au uwasiliane naye. Tunajuaje? Tafadhali **soma Wafilipi 4:6, 7.** Hebu wazia kuhusu mwaliko huo. Mtawala wa ulimwengu wote mzima anakujali sana hivi kwamba anakualika umweleze hisia na matatizo yako.

4 Sala hutusaidia kuwa na urafiki wa karibu pamoja

1, 2. Kwa nini unafikiri sala ni zawadi ya pekee sana, na kwa nini tunahitaji kujua yale ambayo Biblia inafundisha kuhusu sala?
3. Kwa nini tunapaswa kusali kwa Yehova?
4. Kusali kwa ukawaida kunaweza kuimarisha jinsi gani urafiki wako pamoja na Yehova?



"Mtengenezaji wa mbingu na dunia" yuko tayari kusikiliza sala zetu. —Zaburi 115:15

na Yehova. Marafiki wa kweli wanapozungumza kwa ukawaida kuhusu maoni, mahangaiko na hisia zao, urafiki wao unaimarika zaidi. Hivyo ndivyo ilivyo kuhusu uhusiano wetu pamoja na Yehova. Kupitia Biblia, anakujulisha maoni na hisia zake, na pia anakueleza yale atakayofanya wakati ujao. Unaweza kumweleza hisia zako za ndani kabisa kwa kusali kwa ukawaida. Unapofanya hivyo, urafiki wako pamoja na Yehova utaimarika zaidi.—Yakobo 4:8.

TUNAPASWA KUFANYA NINI ILI MUNGU ASIKILIZE SALA ZETU?

5 Je, Yehova husikiliza sala zote? Hapana. Wakati wa nabii Isaya, Yehova aliwaambia Waisraeli hivi: "Hata mjapotoa sala nyingi, mimi sisikilizi; mikono yenu imejaa umwagaji wa damu." (Isaya 1:15) Kwa hiyo, tusipokuwa waangalifu tunaweza kufanya mambo yanayotutenga na Yehova, hivyo kufanya asisikilize sala zetu.

5. Tunajuaje kwamba Yehova hasikilizi sala zote?

6 Ikiwa tunataka Yehova asikilize sala zetu, ni lazima tuwe na imani katika yeye. (Marko 11:24) Mtume Paulo alieleza hivi: "Bila imani haiwezekani kamwe kumpendeza vema, kwa maana yule anayemkaribia Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko na kwamba yeye huwa mthawabishaji wa wale wanaomtafuta kwa bidii." (Waebrania 11:6) Hata hivyo, haitoshi tu kusema kwamba tuna imani. Tunapaswa kuonyesha wazi imani yetu kwa kumtii Yehova kila siku.—**Soma Yakobo 2:26.**

7 Tunahitaji kuwa na heshima na unyenyekevu tunaposali kwa Yehova. Kwa nini? Ikiwa tungehitaji kuzungumza na mfalme au rais, tungefanya hivyo kwa heshima. Yehova ni Mungu Mweza yote, kwa hiyo tunahitaji kuwa na heshima na unyenyekevu mwingi zaidi tunapozungumza naye. (Mwanzo 17:1; Zaburi 138:6) Pia tunapaswa kuwa wanyofu na kusali kwa Yehova kutoka moyoni, na sio kusali kwa kurudia rudia maneno yaleyale tena na tena.—Mathayo 6:7, 8.

8 Mwishowe, tunaposali kuhusu jambo fulani, tunahitaji kufanya yote tunayoweza ili kutenda kulingana na sala zetu. Kwa mfano, ikiwa tumesali kwa Yehova atusaidie kupata riziki ya siku, ikiwa tuna uwezo wa kufanya kazi hatupaswi kuwa wavivu tukitarajia kwamba Yehova atatupatia kila kitu. Ni lazima tufanye kwa bidii kazi yoyote tunayoweza kufanya. (Mathayo 6:11; 2 Wathesalonike 3:10) Ikiwa tumesali kwa Yehova atu-

6. Kwa nini ni muhimu kuwa na imani? Unaweza kuonyesha jinsi gani kwamba una imani?

7. (a) Kwa nini tunapaswa kuwa na heshima na unyenyekevu tunaposali kwa Yehova? (b) Tunaweza kuonyesha jinsi gani kwamba sisi ni wanyofu tunaposali?

8. Tunaposali kuhusu jambo fulani, tunapaswa kufanya jambo gani lingine?

saidie kuacha kufanya jambo fulani baya, ni lazima tujitahidi kuepuka hali yoyote ile inayoweza kutuingiza kwenye kishawishi. (Wakolosai 3:5) Acheni sasa tuchunguze baadhi ya maswali ambayo watu hujiuliza kwa ukawaida kuhusu sala.

MASWALI YANAYOULIZWA KUHUSU SALA

9 Tunapaswa kusali kwa nani? Yesu aliwafundisha wafuasi wake kusali hivi: "Baba yetu uliye mbinguni." (Mathayo 6:9) Pia, alisema hivi: "Mimi ndiye njia na kweli na uzima. Hakuna anayekuja kwa Baba ila kupitia kwangu." (Yohana 14:6) Kwa hiyo, tunahitaji kusali **kwa** Yehova pekee **kupitia** kwa Yesu. Inamaanisha nini kusali kupitia kwa Yesu? Ili Yehova asikilize sala zetu, tunahitaji kuheshimu mgawo wa pekee ambao Yehova amempatia Yesu. Kama tulivyojifunza, Yesu alikuja duniani ili kutukomboa kutokana na dhambi na kifo. (Yohana 3:16; Waroma 5:12) Pia, Yehova amemweka Yesu kuwa Kuhani Mkuu na Hakimu.—Yohana 5:22; Waebrania 6:20.

10 Je, ni lazima tuwe katika hali fulani hususa? Hapana, Yehova hahitaji tupige magoti, tukae, au tusimame wakati tunaposali. Biblia inatufundisha kwamba tunaweza kuzungumza na Yehova tukiwa katika hali mbalimbali lakini kwa heshima. (1 Mambo ya Nyakati 17:16; Nehemia 8:6; Danieli 6:10; Marko 11:25) Jambo muhimu sana kwa Yehova si kukaa katika kikao fulani hususa bali ni kusali tukiwa na nia nzuri. Tunaweza kusali kwa sauti au kimyakimya mahali popote na wakati wowote iwe mchana au usiku. Tunaposali kwa Yehova,

---

9. Tunapaswa kusali kwa nani? Andiko la Yohana 14:6 linatufundisha nini kuhusu sala?

10. Je, ni lazima tuwe katika kikao fulani hususa tunaposali? Fafanua.

tunaweza kuwa na uhakika kwamba atatusikiliza hata ikiwa sala hiyo ni ya kimyakimya.—Nehemia 2:1-6.

[11] **Tunaweza kusali kuhusu nini?** Tunaweza kusali kuhusu jambo lolote kulingana na mapenzi ya Yehova. Biblia inasema hivi: "Hata tukiomba nini kulingana na mapenzi yake, yeye hutusikia." (1 Yohana 5:14) Je, tunaweza kusali kuhusu mambo ya kibinafsi? Ndiyo. Kusali kwa Yehova kunapaswa kuwa sawa na kuzungumza na rafiki wa karibu. Tunaweza kumweleza Yehova jambo lolote tunalofikiria au lililo moyoni mwetu. (Zaburi 62:8) Tunaweza kusali kwake ili atupe roho takatifu itusaidie kufanya yaliyo sawa. (Luka 11:13) Tunaweza kusali kwa Yehova atupe hekima ili tufanye maamuzi kwa njia nzuri, pia tunaweza kusali ili atupatie nguvu za kushinda hali ngumu. (Yakobo 1:5) Tunapaswa kumwomba Yehova atusamehe dhambi zetu. (Waefeso 1: 3, 7) Pia, tunapaswa kusali kwa ajili ya wengine, kutia ndani familia yetu na ndugu na dada kutanikoni.—Matendo 12:5; Wakolosai 4:12.


[12] **Tunapaswa kutanguliza mambo gani katika sala zetu?** Tunapaswa kumtanguliza Yehova na mapenzi yake. Tunaweza kumshukuru kutoka moyoni kwa mambo yote ambayo ametufanyia. (1 Mambo ya Nyakati 29:10-13) Tunajua jambo hilo kwa sababu Yesu alipokuwa duniani aliwafundisha wanafunzi wake jinsi ya kusali. **(Soma Mathayo 6:9-13.)** Alisema kwamba wanapaswa kusali kwanza kuhusu kutakaswa kwa jina la Mungu, yaani, waliheshimu na kuliona kuwa takatifu. Kisha Yesu alisema kwamba tunapaswa kusali Ufalme wa Mungu uje ili kufanya mapenzi ya Yehova hapa du-

11. Tunaweza kusali kwa Yehova kuhusu mambo gani?
12. Ni mambo gani muhimu tunayoweza kutaja katika sala zetu?

niani. Baada ya kusali kuhusu mambo hayo muhimu, Yesu alisema kwamba tunaweza kusali kuhusu mahitaji yetu. Tunaonyesha mambo yaliyo muhimu zaidi katika maisha yetu ikiwa tutamtanguliza Yehova na mapenzi yake katika sala zetu.

13 Sala zetu zinapaswa kuwa na urefu gani? Biblia haisemi kuhusu jambo hilo. Sala zetu zinaweza kuwa

13. Sala zetu zinapaswa kuwa na urefu gani?



Unaweza kusali wakati wowote



Yehova anaweza kujibu sala zetu kupitia msaada tunaopokea kutoka kwa Wakristo wenzetu

ndefu au fupi ikitegemea hali. Kwa mfano, kabla ya kula tunaweza kutoa sala fupi lakini tunaweza kutoa sala ndefu tunapomshukuru Yehova au tunapomweleza mahangaiko yetu. (1 Samweli 1:12, 15) Hatungependa kutoa sala ndefu ili tu kujionyesha, kama ambavyo baadhi ya watu walifanya katika siku za Yesu. (Luka 20: 46, 47) Yehova hapendezwi na sala kama hizo. Jambo muhimu kwa Yehova ni kusali kutoka moyoni.

14 Tunapaswa kusali mara ngapi? Yehova anatualika tuwasiliane naye kwa ukawaida. Biblia inasema kwamba tunapaswa "kusali sikuzote," 'kudumu katika sala' na 'kusali bila kuacha.' (Mathayo 26:41; Waroma 12:12; 1 Wathesalonike 5:17) Yehova yuko tayari kutusikiliza wakati wowote. Tunaweza kumshukuru kila siku kwa

14. Tunapaswa kusali mara ngapi, na jambo hilo linatufundisha nini kumhusu Yehova?

sababu ya upendo na ukarimu wake. Pia, tunaweza kumwomba atupe mwongozo, nguvu na faraja. Kwa kweli ikiwa tunaithamini sana zawadi hii ya sala, tutatumia kila fursa tunayopata ili kusali kwake.

15 Kwa nini tunapaswa kusema "amina" mwishoni mwa sala? Neno "amina" humaanisha "bila shaka" au "na iwe hivyo." Ni njia ya kuonyesha kwamba tunakubaliana na yale yaliyotajwa katika sala, na hilo linamaanisha kwamba sisi ni wanyofu. (Zaburi 41:13) Biblia inatufundisha kwamba ni vizuri pia kusema "amina," kimyakimya au kwa sauti, mwishoni mwa sala inayotolewa kwa ajili ya watu wote kuonyesha kwamba tunakubaliana na yale yaliyotajwa.—1 Mambo ya Nyakati 16:36; 1 Wakorintho 14:16.

JINSI MUNGU ANAVYOJIBU SALA ZETU

16 Je, kweli Yehova hujibu sala zetu? Ndiyo. Biblia inasema kwamba yeye ni "Msikiaji wa sala." (Zaburi 65:2) Yehova husikiliza na kujibu sala zinazotolewa kwa unyofu na mamilioni ya watu, naye hujibu kwa njia mbalimbali.

17 Yehova huwatumia malaika na watumishi wake walioko duniani ili kujibu sala zetu. (Waebrania 1: 13, 14) Kuna mifano mingi ya watu ambao walisali ili wapate msaada wa kuielewa Biblia na muda mfupi tu wakatembelewa na Shahidi wa Yehova. Biblia inaonyesha kwamba malaika wanashiriki kutangaza "habari njema"duniani kote. **(Soma Ufunuo 14:6.)** Pia, huenda tumewahi kusali kwa Yehova kuhusu tatizo fulani

---

15. Kwa nini tunapaswa kusema "amina" mwishoni mwa sala?
16. Je, kweli Yehova husikiliza sala zetu? Fafanua.
17. Yehova anawatumiaje malaika na watumishi wake walio duniani ili kujibu sala zetu?

hususa na kisha tukapokea msaada tuliohitaji kutoka kwa Wakristo wenzetu.—Methali 12:25; Yakobo 2:16.

18 Yehova hutumia roho yake takatifu ili kujibu sala zetu. Tunapoomba msaada wa kukabiliana na tatizo fulani, anaweza kutumia roho yake takatifu ili kutupa mwongozo na kutuimarisha. (2 Wakorintho 4:7) Pia, Yehova hutumia Biblia kujibu sala zetu na kutusaidia kufanya maamuzi kwa hekima. Tunaposoma Biblia, tunaweza kupata maandiko fulani yanayoweza kutusaidia. Yehova anaweza kumchochea mtu fulani kutoa maelezo yanayoweza kutusaidia katika mikutano au anaweza kumtumia mzee wa kutaniko atusomee jambo fulani lenye kutia moyo katika Biblia.—Wagalatia 6:1.

19 Nyakati fulani huenda tukajiuliza hivi: 'Kwa nini Yehova bado hajajibu sala zangu?' Kumbuka kwamba yeye anajua wakati na njia inayofaa ya kujibu sala zetu. Anajua kile tunachohitaji hasa. Hivyo, tunapoendelea kusali kuhusu jambo hilo tunaonyesha wazi kuwa tuna uhitaji na pia kwamba tuna imani kumwelekea. (Luka 11:5-10) Nyakati nyingine Yehova hujibu sala zetu kwa njia tusiyotarajia. Kwa mfano, tunaweza kusali kuhusu hali fulani ngumu tunayokabili, hata hivyo, badala ya kuondoa tatizo hilo, anaweza kutupatia nguvu za kuendelea kuvumilia.—**Soma Wafilipi 4:13.**

20 Kwa kweli ni heshima kubwa kuwasiliana na Yehova katika sala! Tunaweza kuwa na hakika kwamba atatusikiliza. (Zaburi 145:18) Kadiri tunavyosali mara nyingi kwa Yehova kutoka moyoni, ndivyo urafiki wetu pamoja naye utakavyoimarika.

---

18. Yehova anaitumiaje roho takatifu na Biblia ili kujibu sala zetu?
19. Kwa nini nyakati fulani huenda ikaonekana kwamba Yehova hajajibu sala zetu?
20. Kwa nini tunapaswa kusali kwa Yehova mara nyingi zaidi?

UKWELI WA 1 YEHOVA ANATAKA KUSIKILIZA SALA ZETU

"Yehova yuko karibu na wote wanaomwitia, Wote wanaomwitia yeye katika ukweli."—Zaburi 145:18

Tunapaswa kufanya nini ikiwa tunataka Yehova asikilize sala zetu?

Waebrania 11:6
Tunapaswa kuwa na imani.

Zaburi 138:6
Tunapaswa kuwa wanyenyekevu na wenye heshima.

Yakobo 2:26
Lazima mwenendo wetu upatane na sala zetu.

Mathayo 6:7, 8
Tunapaswa kuwa wanyofu. Hatupaswi kurudia maneno yaleyale katika sala zetu.

Isaya 1:15
Lazima tuishi kupatana na mapenzi ya Mungu.

UKWELI WA 2 MASWALI YANAYOULIZWA KUHUSU SALA

Tunapaswa kusali kwa nani?
Mathayo 6:9; Yohana 14:6

Je, ni lazima tuwe katika hali fulani hususa?
1 Mambo ya Nyakati 17:16; Nehemia 8:5, 6; Danieli 6:10; Marko 11:25

Je, Yehova husikia sala zetu za kimyakimya?
Nehemia 2:1-6

Sala zinapaswa kuwa na urefu gani?
1 Samweli 1:12, 15; Luka 20: 46, 47

Tunapaswa kusali mara ngapi?
Waroma 12:12; 1 Wathesalonike 5:17

Kwa nini tunapaswa kusema "amina" mwishoni mwa sala?
1 Mambo ya Nyakati 16:36; 1 Wakorintho 14:16

UKWELI WA 3 TUNAWEZA KUSALI KUHUSU NINI?

"Hata tukiomba nini kulingana na mapenzi yake, yeye hutusikia."—1 Yohana 5:14

Ni mambo gani ambayo tunaweza kutaja katika sala?

Mathayo 6:9, 10
Sali mapenzi ya Yehova yatendeke.

1 Mambo ya Nyakati 29:10-13
Sali kumshukuru Mungu.

Mathayo 6:11-13
Sali kuhusu mahitaji na mahangaiko yetu.

Luka 11:13
Sali ili kuomba roho takatifu.

Yakobo 1:5
Sali ili upate hekima na mwongozo ili ufanye maamuzi mazuri.

Wafilipi 4:13
Sali ili upate nguvu za kuvumilia.

Waefeso 1:3, 7
Sali ili upate msamaha wa dhambi.

Matendo 12:5
Sali kwa ajili ya wengine.

UKWELI WA 4 YEHOVA HUJIBU SALA ZETU

"Ee msikiaji wa sala, kwako wewe watu wote wenye mwili watakuja."—Zaburi 65:2

Yehova hujibu sala zetu jinsi gani?

Methali 12:25; Ufunuo 14:6
Yehova anaweza kutumia malaika au wanadamu kutusaidia.

2 Wakorintho 4:7
Roho takatifu hutupatia msaada tunaohitaji.

Wafilipi 4:6, 7, 13
Anatupatia amani na nguvu tunazohitaji ili kuvumilia.

Wagalatia 6:1; 2 Timotheo 3:16, 17
Anatupatia hekima kupitia Biblia na mikutano.

JE, NINAPASWA KUJIWEKA WAKFU KWA MUNGU NA KUBATIZWA?

UMEJIFUNZA kweli nyingi za Biblia katika kitabu hiki, kama vile ahadi ya Mungu ya uzima wa milele, hali ya wafu, na tumaini la ufufuo. (Mhubiri 9:5; Luka 23:43; Yohana 5:28, 29; Ufunuo 21:3, 4) Labda umeanza kuhudhuria mikutano ya Mashahidi wa Yehova na unaamini kwamba ibada yao ni ya kweli. (Yohana 13:35) Huenda umeanza kusitawisha urafiki wa karibu pamoja na Yehova, na umeamua kumtumikia.

1. Huenda ukajiuliza swali gani baada ya kujifunza kwa makini kitabu hiki?



Hivyo, huenda ukajiuliza, 'Ninapaswa kufanya nini ili kumtumikia Mungu?'

2 Hivyo ndivyo alivyohisi mwanaume Mwethiopia aliyeishi wakati wa Yesu. Muda fulani baada ya Yesu kufufuliwa, Filipo, mwanafunzi wa Yesu alimhubiria mwanaume huyo. Filipo alimhakikishia mwanaume huyo kuwa Yesu alikuwa Masihi. Mwanaume Mwethiopia alichochewa sana na mambo aliyojifunza, hivi kwamba akauliza "Tazama! Maji; ni nini kinachonizuia nisibatizwe?"—Matendo 8:26-36.

3 Biblia inafundisha wazi kwamba ili umtumikie Yehova unapaswa kubatizwa. Yesu aliwaamuru wafuasi wake 'wafanye wanafunzi kutoka kwa watu wa mataifa yote na **kuwabatiza.**' (Mathayo 28:19) Yesu alituwekea kielelezo alipobatizwa. Yesu hakunyunyiziwa maji kichwani bali alizamishwa kabisa ndani ya maji. (Mathayo 3:16) Leo pia, Mkristo anapobatizwa, ni lazima azamishwe kabisa ndani ya maji.

4 Unapobatizwa, unawaonyesha wengine kwamba unataka kuwa rafiki ya Mungu na ungependa kumtumikia. (Zaburi 40:7, 8) Hivyo, huenda ukajiuliza, 'Ninapaswa kufanya nini ili nibatizwe?'

UJUZI NA IMANI

5 Kabla ya kubatizwa, ni lazima **umjue** Yehova na Yesu. Umeanza kupata ujuzi huo kwa kujifunza Biblia.

---

2. Ni nini kilichomchochea mwanaume Mwethiopia atake kubatizwa?
3. (a) Yesu aliwaamuru wanafunzi wake wafanye nini? (b) Mtu anapaswa kubatizwa jinsi gani?
4. Unapobatizwa unawaonyesha nini wengine?
5. (a) Kabla ya kubatizwa unapaswa kufanya nini? (b) Kwa nini ni muhimu kuhudhuria kwa ukawaida mikutano ya Kikristo?

(Soma Yohana 17:3.) Ujuzi pekee hautoshi. Biblia inasema kwamba ni lazima 'tujazwe ujuzi sahihi' kuhusu mapenzi ya Yehova. (Wakolosai 1:9) Mikutano ya Mashahidi wa Yehova itakusaidia kuwa na uhusiano wa karibu na Yehova. Hiyo ni sababu moja muhimu ya kuhudhuria mikutano kwa kawaida.—Waebrania 10: 24, 25.

6 Ni kweli kwamba Yehova hatazamii ujue kila kitu katika Biblia ili ubatizwe. Yehova hakutazamia Mwethiopia ajue kila kitu ili abatizwe. (Matendo 8: 30, 31) Tutaendelea kujifunza kumhusu Yehova milele. (Mhubiri 3:11) Hata hivyo, ili ubatizwe unapaswa kujua na kukubali mafundisho ya msingi ya Biblia. —Waebrania 5:12.

7 Biblia inasema: "Bila imani haiwezekani kamwe kumpendeza Mungu." (Waebrania 11:6) Hivyo, ili ubatizwe unapaswa kuwa na imani. Biblia inasema kwamba watu fulani katika jiji la kale la Korintho walisikia mafundisho ya wafuasi wa Yesu, nao 'wakaamini na kubatizwa.' (Matendo 18:8) Vivyo hivyo, kujifunza Biblia kumekusaidia **kuamini** ahadi za Mungu na nguvu ya dhabihu ya Yesu inayoweza kutuokoa kutokana na dhambi na kifo.—Yoshua 23:14; Matendo 4: 12; 2 Timotheo 3:16, 17.

ZUNGUMZA NA WENGINE KUHUSU KWELI ZA BIBLIA

8 Kadiri unavyojifunza Biblia na kuona faida zake maishani ndivyo imani yako itazidi kuimarika.

---

6. Unapaswa kuwa na ujuzi wa Biblia kadiri gani ili ubatizwe?
7. Kujifunza Biblia kumekusaidia jinsi gani?
8. Ni nini kitakuchochea kuwaeleza wengine kuhusu mambo ambayo umejifunza?

Utachochewa **kuwaeleza wengine mambo unayojifunza**. (Yeremia 20:9; 2 Wakorintho 4:13) Hata hivyo, utawahubiria nani?

9 Unaweza kuzungumza na watu wa familia, marafiki, majirani, au wafanyakazi wenzako mambo unayojifunza. Hata hivyo, uwe mwenye fadhili na upendo unapozungumza nao. Baadaye, unaweza kuanza kuhubiri na kutaniko. Ukihisi kwamba ungependa kuanza kuhubiri na kutaniko, mjulishe anayekufundisha Biblia. Ikiwa anayekufundisha Biblia anaona kwamba unastahili na unaishi kulingana na viwango vya Biblia, mipango itafanywa ili wewe na mwalimu wako mzungumze pamoja na wazee wawili wa kutaniko.

10 Ni mambo gani yatakayozungumziwa katika mkutano huo? Wazee watazungumza na wewe ili kujua kama unaelewa na kuamini mafundisho ya msingi ya Biblia, unaishi kulingana na kanuni za Biblia, na kama kweli unataka kuwa Shahidi wa Yehova. Kumbuka kwamba wazee wanalichunga kutaniko lote, kutia ndani wewe, hivyo usiogope kuzungumza nao. (Matendo 20:28; 1 Petro 5:2, 3) Baada ya mkutano huo, wazee watakujulisha ikiwa unastahili kuanza kuhubiri na kutaniko.

11 Huenda wazee wakakushauri ufanye mabadiliko fulani kabla ya kuanza kuhubiri na kutaniko. Kwa nini ni muhimu kufanya mabadiliko hayo? Kwa sababu tunapozungumza na wengine kumhusu Mungu, tu-

---

9, 10. (a) Unaweza kuanza kuwahubiria nani mambo ambayo umejifunza? (b) Unapaswa kufanya nini ikiwa unataka kuhubiri na kutaniko?

11. Kwa nini ni muhimu kufanya mabadiliko kabla ya kuanza kuhubiri na kutaniko?

namwakilisha Yehova nasi tunapaswa kuishi kwa njia inayomheshimu.—1 Wakorintho 6:9, 10; Wagalatia 5: 19-21.

TUBU NA UGEUKE

12 Kuna jambo lingine ambalo unapaswa kufanya kabla ya kubatizwa. Mtume Petro alisema hivi: "Kwa hiyo, **tubuni** na mgeuke ili dhambi zenu zipate kufutwa." (Matendo 3:19) Kutubu kunamaanisha nini? Kunamaanisha kusikitikia na kujutia makosa ambayo umefanya. Kwa mfano, ikiwa ulikuwa mwasherati, unapaswa kutubu. Hata ikiwa ulijitahidi kuishi maisha safi, unapaswa kutubu kwa sababu sote ni watenda dhambi na hivyo tunapaswa kumwomba Mungu msamaha.—Waroma 3:23; 5:12.

13 Je, inatosha tu kusikitikia na kujutia dhambi ambazo umefanya? La. Mtume Petro alisema kwamba unapaswa **'kugeuka.'** Hilo linamaanisha kwamba unapaswa kuacha kabisa mwenendo mbaya wa zamani na kuanza kufanya yaliyo mema. Kwa mfano, wazia kwamba unasafiri kwenda eneo fulani kwa mara ya kwanza. Baada ya muda, unatambua kwamba unaelekea upande usiofaa. Utafanya nini? Bila shaka, utapunguza mwendo, utasimama na kugeuka, kisha ufuate njia inayofaa. Vivyo hivyo, unapoendelea kujifunza Biblia, utatambua kwamba kuna mazoea au tabia ambazo unapaswa kuacha. Uwe tayari 'kugeuka,' yaani kufanya mabadiliko yanayofaa, na kuanza kutenda mema.

---

12. Kwa nini sote tunapaswa kutubu?
13. 'Kugeuka' kunamaanisha nini?

JIWEKE WAKFU

14 **Kujiweka wakfu** kwa Yehova ni hatua nyingine muhimu unayopaswa kuchukua kabla ya kubatizwa. Unapojiweka wakfu kwa Yehova katika sala, unamwahidi kwamba utamwabudu yeye peke yake na kutanguliza mapenzi yake maishani.—Kumbukumbu la Torati 6:15.

15 Unapomwahidi Yehova kwamba utamtumikia ni sawa na kumwahidi mtu unayempenda kwamba mtaishi pamoja katika maisha yenu yote. Wazia kwamba mwanamume na mwanamke wanaanzisha urafiki. Kadiri mwanamume anavyomjua mwanamke huyo vizuri atampenda na atataka kumwoa. Ingawa huo ni uamuzi mzito, mwanamume huyo yuko tayari kukubali wajibu huo kwa sababu anampenda.

16 Kadiri unavyojifunza kumhusu Yehova, utampenda na utataka kumtumikia. Hilo litakuchochea kusali na kumwahidi kumtumikia. Biblia inasema kwamba yeyote anayetaka kumfuata Yesu lazima "ajikane mwenyewe." (Marko 8:34) Inamaanisha nini? Inamaanisha kwamba kumtii Yehova litakuwa jambo kuu katika maisha yako. Kutanguliza mapenzi ya Yehova kutakuwa muhimu kuliko malengo na mambo tunayopenda.—**Soma 1 Petro 4:2.**

USIOGOPE KUSHINDWA

17 Baadhi ya watu hawataki kujiweka wakfu kwa Yehova kwa sababu wanaogopa kwamba watashindwa

---

14. Unajiweka wakfu kwa Yehova jinsi gani?
15, 16. Ni nini kinachomchochea mtu kujiweka wakfu kwa Mungu?
17. Kwa nini baadhi ya watu wanaogopa kujiweka wakfu kwa Yehova?

kuendelea kumtumikia. Huenda wanaogopa kwamba watamkosea, au wanafikiri kwamba wasipojiweka wakfu, hawatawajibika mbele za Yehova.

18 Upendo wako kwa Yehova utakusaidia kushinda hofu ya kumkosea. Kwa kuwa unampenda, utajitahidi kutimiza ahadi yako. (Mhubiri 5:4; Wakolosai 1:10) Haitakuwa vigumu kwako kufanya mapenzi ya Yehova. Mtume Yohana aliandika hivi: "Kwa maana kumpenda Mungu humaanisha hivi, kwamba tuzishike amri zake; na bado amri zake si mzigo mzito."—1 Yohana 5:3.

19 Si lazima uwe mkamilifu ili ujiweke wakfu kwa Yehova. Hatazamii tufanye mambo yanayozidi uwezo wetu. (Zaburi 103:14) Atakusaidia kufanya mema. (Isaya 41:10) Mtegemee Yehova kwa moyo wako wote, "naye atanyoosha mapito yako."—Methali 3:5, 6.

TANGAZO LA HADHARANI LA WOKOVU

20 Je, unafikiri uko tayari kujiweka wakfu kwa Yehova? Ukijiweka wakfu utakuwa tayari kwa hatua nyingine. Hatua hiyo ni **kubatizwa.**

21 Mjulishe mratibu wa baraza la wazee wa kutaniko lako kwamba umejiweka wakfu kwa Yehova na ungependa kubatizwa. Kisha, atapanga baadhi ya wazee wapitie mafundisho ya msingi ya Biblia pamoja nawe. Wakiona unastahili,

18. Ni nini kitakachokusaidia kushinda hofu ya kumkosea Yehova?
19. Kwa nini hupaswi kuogopa kujiweka wakfu kwa Yehova?
20. Unapaswa kuchukua hatua gani nyingine baada ya kujiweka wakfu?
21, 22. Unatoa jinsi gani "tangazo la hadharani" la imani yako?



Kabla ya kubatizwa,
ni lazima ujifunze Biblia

Imani inapaswa
kukuchochea
kuwaambia wengine
mambo unayoamini



watakujulisha kwamba utabatizwa katika kusanyiko linalofuata la Mashahidi wa Yehova. Kusanyikoni, hotuba inayoeleza maana ya ubatizo itatolewa. Kisha, msemaji wa hotuba hiyo atawaomba walio tayari kwa ubatizo wajibu maswali mawili rahisi. Kwa kujibu maswali hayo, utafanya “tangazo la hadharani” la imani yako.—Waroma 10:10.

22 Kisha utabatizwa. Utazamishwa kabisa ndani ya maji. Kwa kubatizwa, utawaonyesha watazamaji kwamba umejiweka wakfu kwa Yehova na sasa wewe ni Shahidi wa Yehova.

Je, umemwahidi Yehova kwamba utamtumikia?

Unapobatizwa, unaonyesha kwamba unataka kufanya mapenzi ya Mungu



MAANA YA UBATIZO WAKO

23 Yesu alisema kwamba wanafunzi wake wangebatizwa "katika jina la Baba na la Mwana na la roho takatifu." **(Soma Mathayo 28:19.)** Inamaanisha nini? Inamaanisha kutambua mamlaka ya Yehova na fungu la Yesu katika kutimizwa kwa kusudi la Mungu, na jinsi Mungu anavyotumia roho takatifu kutimiza mapenzi yake.—Zaburi 83:18; Mathayo 28:18; Wagalatia 5:22, 23; 2 Petro 1:21.

24 Ubatizo unawakilisha jambo muhimu sana. Kuzamishwa katika maji, kunamaanisha kwamba umekufa au umeacha maisha yako ya zamani. Unapoinuka kutoka katika maji, utaanza maisha mapya yaani kufanya mapenzi ya Mungu. Inamaanisha kwamba kuanzia sasa na kuendelea utamtumikia Yehova. Kumbuka kwamba hujajiweka wakfu kwa mwanadamu, shirika au kazi fulani. Umejiweka wakfu kwa Yehova.

25 Wakfu wako utakusaidia kuimarisha urafiki pamoja na Mungu. (Zaburi 25:14) Hilo halimaanishi kwamba mtu ataokolewa kwa sababu tu amebatizwa. Mtume Paulo aliandika hivi: "Endeleeni kuufanyia kazi wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka." (Wafilipi 2:12) Ubatizo ni mwanzo tu. Hata hivyo, unawezaje kukaa karibu na Yehova? Sura ya mwisho ya kitabu hiki itajibu swali hilo.

---

23. Inamaanisha nini kubatizwa "katika jina la Baba na la Mwana na la roho takatifu"?

24, 25. (a) Ubatizo unamaanisha nini? (b) Tutazungumzia nini katika sura ya mwisho ya kitabu hiki?

UKWELI WA 1 JE, NINAPASWA KUBATIZWA?

"Tazama! Maji; ni nini kinachonizuia nisibatizwe?"
—Matendo 8:36

Kwa nini ni lazima ubatizwe na unapaswa kufanya nini ili ustahili?
Ubatizo unaonyesha kwamba umeacha mwenendo wako wa zamani na umeanza kuishi maisha mapya ya kufanya mapenzi ya Mungu.

Mathayo 28:19, 20
Unapaswa kubatizwa ili kumtumikia Yehova.

Zaburi 40:8
Ubatizo unawaonyesha wengine kwamba unataka kumtumikia Mungu.

Mathayo 3:16
Lazima uzamishwe kabisa katika maji kama Yesu alivyofanya.

UKWELI WA 2 YEHOVA HATAZAMII KAMWE TUFANYE MAMBO YANAYOZIDI UWEZO WETU

"Kumpenda Mungu humaanisha hivi, kwamba tuzishike amri zake; na bado amri zake si mzigo mzito."—1 Yohana 5:3

Kwa nini hupaswi kuogopa kujiweka wakfu kwa Yehova?

Zaburi 103:14; Isaya 41:10
Si lazima uwe mkamilifu ili ujiweke wakfu kwa Yehova. Atakusaidia kufanya yaliyo sawa.

Wakolosai 1:10
Upendo wako kwa Yehova utakusaidia kukabili woga wa kushindwa kumpendeza.

UKWELI WA 3 HATUA ZINAZOONGOZA KWENYE UBATIZO

"Ee Mungu wangu, nimependezwa na kufanya mapenzi yako, na sheria yako imo ndani yangu."—Zaburi 40:8

Unapaswa kufanya nini ili kujiweka wakfu kwa Yehova?

Yohana 17:3
JIFUNZE NENO LA MUNGU
Jifunze kumhusu Yehova na Yesu Kristo. Kadiri unavyojifunza mengi zaidi kuwahusu, ndivyo utakavyowapenda zaidi.

Waebrania 11:6
IMARISHA IMANI YAKO
Tumaini kabisa ahadi za Mungu na nguvu ya dhabihu ya Yesu ya kutukomboa kutoka katika dhambi na kifo.

Matendo 3:19
KUTUBU
Kunamaanisha kusikitika na kujutia makosa ambayo umefanya.

KUGEUKA
Kunamaanisha kuacha mwenendo mbaya wa zamani na kuanza kufanya yaliyo mema.

1 Petro 4:2
KUJIWEKA WAKFU
Unajiweka wakfu kwa Yehova unapomwahidi katika sala kwamba utamwabudu yeye pekee na kutanguliza mapezi yake maishani.

KAA KARIBU NA YEHOVA

WAZIA kwamba unatembea wakati wa dhoruba kali. Mawingu yanazidi kutanda, radi zinapiga, na ngurumo zinasikika. Kisha mvua kubwa inaanza kunyesha. Unatafuta mahali pa kujificha. Bila shaka, utafurahi sana unapopata mahali salama!

2 Tunaishi kipindi kinachofanana na hali hiyo. Hali za ulimwengu zinazidi kuwa mbaya. Huenda ukajiuliza, 'Ninaweza kupata wapi kimbilio?' Mwandikaji wa zaburi aliandika hivi: "Nitamwambia Yehova: 'Wewe ni kimbilio langu na ngome yangu, Mungu wangu, ambaye nitamtegemea.'" (Zaburi 91:2) Yehova anaweza kutupatia kitulizo cha matatizo yetu ya sasa, na pia tumaini zuri la wakati ujao.

3 Yehova anaweza kutulinda jinsi gani? Anaweza kutusaidia kukabiliana na matatizo yetu, na ana nguvu kuliko yeyote anayetaka kutudhuru. Hata ikiwa tutapatwa na jambo fulani baya kwa sasa, tuna uhakika kwamba Yehova atarekebisha hali hiyo wakati ujao. Biblia inatusihi hivi: "Jitunzeni katika upendo wa Mungu." (Yuda 21) Tunahitaji kukaa karibu na Yehova ili atusaidie tunapokabili hali ngumu. Lakini, tunaweza kufanya hivyo jinsi gani?

TENDA KULINGANA NA UPENDO WA MUNGU

4 Ili tukae karibu na Yehova tunahitaji kutambua

1, 2. Tunaweza kupata wapi kimbilio?
3. Tunaweza kumfanya Yehova kuwa kimbilio letu jinsi gani?
4, 5. Yehova ameonyesha jinsi gani kwamba anatupenda?

jinsi anavyotupenda. Fikiria mambo yote mazuri ambayo Yehova ametufanyia. Ametupatia dunia maridadi na kuijaza kwa mimea na wanyama wenye kupendeza. Pia, ametupatia vyakula vitamu na maji safi ya kunywa. Kupitia Biblia, Yehova ametufundisha jina na sifa zake nzuri. Zaidi ya yote, alionyesha kwamba anatupenda alipomtuma Mwana wake mpendwa, Yesu, aje duniani ili atoe uhai wake kwa ajili yetu. (Yohana 3:16) Kwa sababu ya dhabihu hiyo, tuna tumaini zuri la wakati ujao.

5 Yehova amesimamisha Ufalme wa Kimasihi, yaani, serikali ya mbinguni ambayo hivi karibu itaondoa mateso yote. Ufalme huo utaifanya dunia kuwa paradiso, ambayo kila mtu ataishi kwa amani na furaha milele. (Zaburi 37:29) Njia nyingine ambayo Yehova ameonyesha kwamba anatupenda ni kwa kutufundisha jinsi ya kuishi maisha bora sasa. Pia, anatualika kusali kwake, na sikuzote yuko tayari kutusikiliza. Kwa kweli Yehova ameonyesha kwamba anampenda kila mmoja wetu.

6 Tunapaswa kuitikia jinsi gani upendo wa Yehova? Mshukuru kwa yote aliyokufanyia. Inasikitisha kwamba watu wengi leo, hawana shukrani. Ilikuwa hivyo Yesu alipokuwa duniani. Wakati fulani, Yesu aliwaponya watu kumi wenye ukoma, lakini ni **mmoja tu** alimshukuru. (Luka 17:12-17) Tungependa kuwa kama mtu huyo aliyemshukuru Yesu. Sikuzote tunataka kuwa wenye shukrani kwa Yehova.

7 Pia, tunapaswa kumpenda Yehova. Yesu aliwaa-

6. Tunapaswa kuitikia jinsi gani upendo wa Yehova?
7. Tunapaswa kumpenda Yehova kadiri gani?

mbia wanafunzi wake kwamba lazima wampende Yehova kwa moyo, nafsi, na akili yao yote. **(Soma Mathayo 22:37.)** Inamaanisha nini?

8 Je, inatosha tu kusema tunampenda Yehova? Hapana. Ikiwa tunampenda Yehova kwa moyo, nafsi na akili yetu yote, tutaonyesha hivyo kwa matendo. (Mathayo 7:16-20) Biblia inafundisha wazi kwamba ikiwa tunampenda Mungu, tutatii amri zake. Je, ni vigumu kufanya hivyo? Hapana, kwa sababu "amri zake [Yehova] si mzigo mzito."—**Soma 1 Yohana 5:3.**

9 Tunapomtii Yehova, tunakuwa na furaha na maisha bora. (Isaya 48:17, 18) Hata hivyo, nini kitakachotusaidia kukaa karibu na Yehova? Acha tuone.

ENDELEA KUMKARIBIA YEHOVA

10 Ulianza kuwa rafiki ya Yehova jinsi gani? Kupitia kujifunza Biblia, umemjua zaidi Yehova na umeboresha urafiki pamoja naye. Urafiki huo ni kama moto ambao ungependa uendelee kuwaka. Kama tu moto unavyohitaji kuni ili uendelee kuwaka, unahitaji kuendelea kujifunza kumhusu Yehova ili urafiki wenu uwe imara zaidi.—Methali 2:1-5.

11 Unapoendelea kujifunza Biblia, utajua mambo mengi yanayogusa moyo wako. Ona jinsi wanafunzi wawili wa Yesu walivyohisi Yesu alipokuwa akiwafafanulia unabii wa Biblia. Walisema hivi: "Je, mioyo yetu haikuwa ikiwaka alipokuwa akisema nasi barabarani, alipokuwa akitufungulia Maandiko?"—Luka 24:32.

8, 9. Ni jinsi gani tunaweza kuonyesha kwamba tunampenda Yehova?


10. Kwa nini unapaswa kuendelea kujifunza kumhusu Yehova?

11. Utafaidika jinsi gani kwa kujifunza Biblia?

12 Kama tu mioyo ya wanafunzi wa Yesu ilivyoguswa walipoelewa Maandiko, huenda ulihisi hivyo ulipoanza kuielewa Biblia. Jambo hilo lilikusaidia kumjua Yehova na kumpenda. Hungependa upendo huo upoe. —Mathayo 24:12.

13 Mara tu unapokuwa rafiki ya Mungu, unahitaji kufanya yote unayoweza ili urafiki wenu uwe imara. Lazima uendelee kujifunza kumhusu Yehova na Yesu na utafakari mambo unayojifunza na jinsi unavyoweza kuyatumia maishani. (Yohana 17:3) Unaposoma au kujifunza Biblia, jiulize: 'Jambo hili linanifundisha nini kumhusu Yehova? Kwa nini ninapaswa kumpenda kwa moyo na nafsi yangu yote?'—1 Timotheo 4:15.

12, 13. (a) Upendo wetu kwa Mungu unaweza kuathiriwa jinsi gani? (b) Tunaweza kufanya nini ili upendo wetu kwa Yehova usipoe?



Kama moto, upendo wako kwa Yehova unahitaji kuni ili uendelee kuwaka

14 Unapokuwa na rafiki, unawasiliana naye kwa ukawaida, na jambo hilo linaimarisha urafiki wenu. Vivyo hivyo, tunapowasiliana na Yehova kwa ukawaida katika sala, upendo wetu kwake utaimarika zaidi. **(Soma 1 Wathesalonike 5:17.)** Sala ni zawadi bora kutoka kwa Baba yetu wa mbinguni. Tunapaswa kuwasiliana naye kutoka moyoni. (Zaburi 62:8) Hatupaswi kukariri sala zetu, badala yake tunapaswa kusali kutoka moyoni. Kwa kweli, ikiwa tutaendelea kujifunza Biblia na kusali kutoka moyoni, upendo wetu kwa Yehova utaimarika.

KUWAAMBIA WENGINE KUMHUSU YEHOVA

15 Pia, ikiwa tunapenda kuendelea kuwa karibu na Yehova, tunapaswa kuwaambia wengine kuhusu imani yetu. Kuwaambia wengine kuhusu Yehova ni heshima kubwa sana. (Luka 1:74) Na ni wajibu ambao Yesu aliwapa Wakristo wote wa kweli. Sote tunapaswa kuhubiri habari njema za Ufalme wa Mungu. Je, unafanya hivyo?—Mathayo 24:14; 28:19, 20.

16 Mtume Paulo aliiona kazi ya kuhubiri kuwa "hazina." (2 Wakorintho 4:7) Kuwahubiria wengine kumhusu Yehova na makusudi yake ndiyo kazi muhimu ambayo unaweza kufanya. Ni namna nyingine ya kumtumikia Yehova, na anathamini yale unayofanya kwa ajili yake. (Waebrania 6:10) Unapohubiri unajifaidi wewe mwenyewe na wale wanaokusikiliza kwa sababu kufanya hivyo kunawasaidia nyote kumkaribia Yehova na kupata uzima wa milele. **(Soma 1 Wakorintho 15:58.)** Hakuna kazi nyingine yoyote inayoridhisha kama kazi ya kuhubiri.

---

14. Sala inatusaidia jinsi gani kuimarisha upendo wetu kwa Yehova?
15, 16. Unaionaje kazi ya kuhubiri?

17 Kazi ya kuhubiri inahitaji kufanywa haraka sana. Tunapaswa 'kulihubiri neno,' na tunapaswa 'kufanya hivyo kwa bidii.' (2 Timotheo 4:2) Watu wanahitaji kusikia kuhusu Ufalme wa Mungu. Biblia inasema: "Ile siku kuu ya Yehova iko karibu. Iko karibu, nayo inaharakisha sana!" Mwisho 'hautachelewa!' (Sefania 1:14; Habakuki 2:3) Kwa kweli, hivi karibuni, Yehova atauharibu ulimwengu mwovu wa Shetani. Kabla ya hilo kutukia, watu wanahitaji kuonywa ili waweze kuamua kumtumikia Yehova.

18 Yehova anataka tumwabudu pamoja na Wakristo wa kweli. Biblia inasema: "Na acheni tufikiriane ili kuchocheana katika upendo na matendo mazuri, bila kuacha kukusanyika pamoja sisi wenyewe, kama vile wengine walivyo na desturi, bali tutiane moyo, na kufanya hivyo zaidi kwa kadiri mnavyoona siku ile kuwa inakaribia." (Waebrania 10:24, 25) Tunapaswa kufanya yote tunayoweza ili kuhudhuria mikutano yote. Kwenye mikutano tunapata fursa ya kutiana moyo na kuimarishana.

19 Unapohudhuria mikutano, utapata marafiki wazuri ambao watakusaidia kumwabudu Yehova. Utakutana na ndugu na dada wanaofanya yote wanayoweza ili kumwabudu Yehova kama wewe. Wao pia si wakamilifu na wanakosea. Wanapokosea uwe tayari kuwasamehe. **(Soma Wakolosai 3:13.)** Sikuzote kazia sifa nzuri za ndugu na dada zako Wakristo, kufanya hivyo kutakusaidia kuwapenda na kumkaribia zaidi Yehova.

---

17. Kwa nini kazi ya kuhubiri inahitaji kufanywa haraka?
18. Kwa nini tunapaswa kumwabudu Yehova pamoja na Wakristo wa kweli?
19. Ni nini kinachoweza kutusaidia kuwapenda ndugu na dada zetu Wakristo?

UZIMA ULIO WA KWELI

20 Yehova anataka rafiki zake wawe na maisha bora kabisa. Biblia inatufundisha kwamba wakati ujao maisha yetu yatakuwa tofauti kabisa na maisha ya leo.

21 Wakati ujao, hatutaishi kwa miaka 70 au 80 tu, bali tutaishi milele. Tutafurahia "uzima wa milele" tukiwa na afya njema, amani na furaha katika dunia paradiso. Huo ndio "uzima ulio wa kweli" unaotajwa katika Biblia. Yehova anatuahidi kutupatia uzima ulio wa kweli, hata hivyo ni lazima tufanye yote tunayoweza ili 'kuushika imara.'—1 Timotheo 6:12, 19.

22 Tunaweza 'kushika imara uzima ulio wa kweli' jinsi gani? Lazima 'tufanye mema' na 'tuwe matajiri katika matendo mazuri.' (1 Timotheo 6:18) Hilo linamaanisha kwamba tunahitaji kutumia yale tunayojifunza katika Biblia. Hata hivyo, uzima ulio wa kweli hautegemei jitihada zetu wenyewe. Uzima wa milele ni zawadi ambayo Yehova huwapa watumishi wake waaminifu, ni "fadhili zisizostahiliwa." (Waroma 5:15) Kwa kweli Baba yetu wa mbinguni anataka kuwapa watumishi wake waaminifu zawadi hiyo.


23 Jiulize, 'Je, ninamwabudu Mungu katika njia anayoikubali?' Ukitambua kwamba unahitaji kufanya mabadiliko fulani, fanya bila kukawia. Tunapofanya yote tunayoweza ili kumtii Yehova na kumtegemea yeye, atakuwa kimbilio letu. Atawalinda watu wake waaminifu katika siku za mwisho za ulimwengu mwovu wa Shetani. Kisha, Yehova atahakikisha kwamba tunaishi

---

20, 21. "Uzima ulio wa kweli" ni nini?
22. (a) Tunaweza 'kushika imara uzima ulio wa kweli' jinsi gani? (b) Kwa nini uzima wa milele ni zawadi?
23. Kwa nini unahitaji kufanya uamuzi unaofaa sasa?

milele katika paradiso kama tu alivyoahidi. Naam, unaweza kuwa na uzima ulio wa kweli ikiwa utafanya uamuzi unaofaa sasa!

Yehova anapenda ufurahie
“uzima ulio wa kweli.”
Je, utafurahia?



UKWELI WA 1 YEHOVA ANAKUPENDA

"Mungu aliupenda ulimwengu sana hivi kwamba akamtoa Mwana wake mzaliwa-pekee, ili kila mtu anayemwamini asiangamizwe bali awe na uzima wa milele."—Yohana 3:16

Mungu anaonyesha jinsi gani kwamba anakupenda?

Zaburi 91:2
Yehova ni kimbilio letu. Anaweza kutupatia kitulizo cha matatizo yetu.

Zaburi 37:29
Ametupatia tumaini zuri la wakati ujao.

1 Timotheo 6:12, 19
Mungu atatupatia uzima wa milele tukiwa wakamilifu. Tutafurahia amani, shangwe, na afya kamilifu katika paradiso maridadi

UKWELI WA 2 YEHOVA ANATAKA UMPENDE

"Lazima umpende Yehova Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa nafsi yako yote na kwa akili yako yote."—Mathayo 22:37

Upendo kwa Mungu unakuchochea kufanya nini?

Luka 17:12-17
Mshukuru Mungu kwa kila kitu ambacho amekufanyia.

Mathayo 7:16-20
Mpende Mungu kwa kufanya mapenzi yake kila siku.

1 Yohana 5:3
Tii amri za Mungu.

1 Timotheo 6:18
Jitahidi kuwatendea mema wengine.

UKWELI WA 3

IMARISHA UPENDO WAKO KWA YEHOVA

"Jitunzeni katika upendo wa Mungu."—Yuda 21

Ni nini kitakachokusaidia kukaa karibu na Yehova?

1 Wathesalonike 5:17
Sali mara kwa mara

Mathayo 28:19, 20; 2 Timotheo 4:2
Fanya yote unayoweza kuwahubiria wengine kuhusu Ufalme wa Mungu.

Methali 2:1-5
Endelea kujifunza kuhusu Yehova.

Waebrania 10:24, 25
Hudhuria mikutano kwa ukawaida. Ndugu na dada zako Wakristo watakusaidia kumkaribia zaidi Yehova.

1 YEHOVA

Yehova ni jina la Mungu na linamaanisha kwamba “Yeye Husababisha Kuwa.” Yehova ni Mungu mweza-yote na aliumba kila kitu. Ana uwezo wa kufanya jambo lolote ambalo angependa kufanya.

Katika Kiebrania, jina la Mungu liliandikwa kwa herufi nne. Katika Kiswahili herufi hizo hutafsiriwa kuwa “Yehova”. Jina la Mungu linapatikana katika maandishi ya awali ya Maandiko ya Kiebrania karibu mara 7,000. Ulimwenguni pote, watu wanaandika jina la Yehova kwa njia mbalimbali, na kulitamka kulingana na lugha zao.

▸ Sura ya 1, fu. 15

2 BIBLIA ‘IMEONGOZWA NA ROHO YA MUNGU’

Mungu ndiye mtungaji wa Biblia, hata hivyo, aliwatumia wanadamu kuiandika. Ni sawa na babu akimwomba mjukuu wake amwandikie barua. Mungu alitumia roho takatifu kuwaongoza waandikaji wa Biblia waandike mawazo yake. Roho ya Mungu iliwaongoza kwa njia mbalimbali, nyakati nyingine kupitia ndoto au maono.

▸ Sura ya 2, fu. 5

3 KANUNI

Ni mafundisho yanayofafanua kweli za msingi za Biblia. Kwa mfano, kanuni inayosema “mashirika mabaya huharibu tabia nzuri” hutufundisha kwamba watu tunaoshirikiana nao wanaweza kutuathiri kwa njia nzuri au mbaya. (1 Wakorintho 15:33) Pia, kanuni inayosema “lolote lile analopanda mtu, atavuna hilo pia” inatufundisha kwamba hatuwezi kuepuka matokeo ya matendo yetu.—Wagalatia 6:7.

▸ Sura ya 2, fu. 12

4 UNABII

Huo ni ujumbe kutoka kwa Mungu. Unaweza kuwa ni ufafanuzi unaohusu mapenzi ya Mungu, mafundisho ya maadili, amri, au hukumu. Pia unaweza kuwa ujumbe unaohusu jambo litakalotukia wakati ujao. Unabii mwingi ulio katika Biblia tayari umetimia.

▸ Sura ya 2, fu. 13

5 UNABII KUHUSU MASIHI

Yesu ndiye aliyetimiza unabii wa Biblia unaomhusu Masihi. Soma sanduku "Unabii Kumhusu Masihi."

▸ Sura ya 2, fu. 17, Maelezo ya chini.

6 KUSUDI LA YEHOVA KWA DUNIA

Yehova aliiumba dunia paradiso kwa ajili ya wanadamu wanaompenda. Kusudi lake halijabadilika. Hivi karibuni, Mungu ataondoa uovu na kuwapa watu wake uzima wa milele.

▸ Sura ya 3, fu. 1

7 SHETANI IBILISI

Shetani ni malaika aliyeanzisha uasi dhidi ya Mungu. Anaitwa Shetani, jina linalomaanisha "Mpinzani" kwa sababu anampinga Yehova. Pia, anaitwa Ibilisi, jina linalomaanisha "Mchongezi." Alipewa jina hilo kwa sababu yeye huwadanganya watu na kusema uwongo kumhusu Mungu.

▸ Sura ya 3, fu. 4

UNABII KUMHUSU MASIHI

TUKIO	UNABII	UTIMIZO
Alizaliwa katika kabila la Yuda	Mwanzo 49:10	Luka 3:23-33
Alizaliwa na bikira	Isaya 7:14	Mathayo 1:18-25
Mzao wa Mfalme Daudi	Isaya 9:7	Mathayo 1:1, 6-17
Yehova alimtangaza Yesu kuwa Mwana wake	Zaburi 2:7	Mathayo 3:17
Watu wengi hawakuamini kwamba Yesu alikuwa Masihi	Isaya 53:1	Yohana 12:37, 38
Aliingia Yerusalemu akiwa amepanda punda	Zekaria 9:9	Mathayo 21:1-9
Alisalitiwa na rafiki yake wa karibu	Zaburi 41:9	Yohana 13:18, 21-30
Alisalitiwa kwa vipande 30 vya fedha	Zekaria 11:12	Mathayo 26:14-16
Alikaa kimya alipokuwa akishtakiwa	Isaya 53:7	Mathayo 27:11-14
Mavazi yake yalipigiwa kura	Zaburi 22:18	Mathayo 27:35
Alitukanwa akiwa kwenye mti wa mateso	Zaburi 22:7, 8	Mathayo 27:39-43
Hakuna mfupa wake hata mmoja uliovunjwa	Zaburi 34:20	Yohana 19:33, 36
Alizikwa na tajiri	Isaya 53:9	Mathayo 27:57-60
Ufufuo wake	Zaburi 16:10	Matendo 2:24, 27
Alifufuliwa kwenda mbinguni akaketi kwenye mkono wa kuume wa Mungu	Zaburi 110:1	Matendo 7:55, 56

8 MALAIKA

Yehova aliwaumba malaika miaka mingi kabla hajaumba dunia. Waliumbwa waishi mbinguni. Kuna malaika zaidi ya milioni mia moja. (Danieli 7:10) Wana majina na utu wao unatofautiana. Malaika washikamanifu hawakubali kuabudiwa na wanadamu. Wanatofautiana vyeo na kazi zao. Baadhi ya kazi hizo ni kutumikia mbele ya kiti cha Ufalme cha Yehova, kutoa ujumbe wa Mungu, kuwalinda na kuwaongoza watumishi wake duniani, kutekeleza hukumu, na kutegemeza kazi ya kuhubiri. (Zaburi 34:7; Ufunuo 14:6; 22:8, 9) Wakati ujao, watashirikiana na Yesu katika vita vya Har–Magedoni.—Ufunuo 16:14, 16; 19: 14, 15.

▸ Sura ya 3, fu. 5; Sura ya 10, fu. 1

9 DHAMBI

Dhambi ni kufikiria au kutenda jambo lolote lililo kinyume na mapenzi ya Yehova. Kwa kuwa dhambi inaharibu uhusiano wetu na Mungu, ametupatia sheria na kanuni zinazotusaidia kuepuka kufanya dhambi. Mwanzoni, Yehova aliumba kila kitu kikiwa kikamilifu, lakini Adamu na Hawa walipochagua kutomtii Yehova, walifanya dhambi na wakapoteza ukamilifu. Walizeeka na kufa, na kwa sababu tulirithi dhambi kutoka kwa Adamu, sisi pia tunazeeka na kufa.

▸ Sura ya 3, fu. 7; Sura ya 5, fu. 3

10 HAR–MAGEDONI

Ni Vita vya Mungu vya kuuharibu ulimwengu wa Shetani na uovu wote.

▸ Sura ya 3, fu. 13; Sura ya 8, fu. 18

11 UFALME WA MUNGU

Ufalme wa Mungu ni serikali ambayo Yehova amesimamisha mbinguni. Mfalme wa serikali hiyo ni Yesu Kristo. Wakati ujao Yehova atatumia Ufalme huo kuondoa uovu wote. Ufalme wa Mungu utaitawala dunia.

▸ Sura ya 3, fu. 14

12 YESU KRISTO

Mungu alimuumba Yesu kabla hajaumba kitu kingine chochote. Yehova alimtuma Yesu duniani ili afe kwa ajili ya wanadamu wote. Baada ya Yesu kuuawa, Yehova alimfufua. Sasa, Yesu anatawala akiwa Mfalme wa Ufalme wa Mungu mbinguni.

▸ Sura ya 4, fu. 2

13 UNABII KUHUSU YALE MAJUMA 70


Biblia ilitabiri wakati ambao Masihi angetokea. Hilo lingetokea mwishoni mwa kipindi cha wakati kinachoitwa majuma 69, kilichoanza mwaka 455 K.W.K. na kuisha mwaka wa 29 W.K.

Tunajua jinsi gani kwamba majuma hayo yaliishia mwaka wa 29 W.K.? Majuma 69 yalianza mwaka 455 K.W.K., Nehemia aliporudi Yerusalemu na kuanza kujenga upya jiji hilo. (Danieli 9:25; Nehemia 2:1, 5-8) Kama tu neno “dazeni” linavyomaanisha 12, neno “juma” humaanisha *7*. Kulingana na kanuni ya kinabii ya “siku moja kwa mwaka mmoja,” majuma yanayotajwa katika unabii huu si majuma ya siku saba bali ni majuma ya miaka saba. (Hesabu 14:34; Ezekieli 4:6) Inamaanisha kwamba kila juma ni kipindi chenye urefu wa miaka saba, hivyo jumla ya majuma 69 ni miaka 483 (yaani 69 x 7). Tukihesabu miaka 483 kuanzia mwaka wa 455 K.W.K.,

inatufikisha mwaka wa 29 W.K. Huo ndio mwaka ambao Yesu alibatizwa na kuwa Masihi!—Luka 3:1, 2, 21, 22.

Unabii huo pia ulitabiri kuhusu juma lingine lenye miaka saba. Katika juma hilo, Masihi angeuawa mwaka wa 33 W.K. na kuanzia mwaka wa 36 W.K. habari njema za Ufalme wa Mungu zingehubiriwa katika mataifa yote na si kwa Wayahudi pekee.—Danieli 9:24-27.

▸ Sura ya 4, fu. 7



14 UTATU NI FUNDISHO LA UWONGO

Biblia inafundisha kwamba Yehova Mungu ni Muumba na alimuumba Yesu kabla ya kuumba vitu vingine vyote. (Wakolosai 1:15, 16) Yesu si Mungu Mweza-Yote. Hakudai kamwe kwamba alikuwa sawa na Mungu. Badala yake alisema: "Baba ni mkuu kuliko mimi." (Yohana 14:28; 1 Wakorintho 15:28) Hata hivyo, baadhi dini hufundisha Utatu, yaani, Mungu ni mmoja katika nafsi tatu, Baba, Mwana, na roho takatifu. Neno "Utatu" halipatikani katika Biblia. Hilo ni fundisho la uwongo.

Roho takatifu ni nguvu ya utendaji ya Mungu, ni nguvu yake isiyoonekana ambayo huitumia kutimiza mapenzi yake. Si mtu. Kwa mfano, Wakristo wa mapema '*walijazwa* roho takatifu,' na Yehova alisema: "*Nitaimimina* sehemu ya roho yangu juu ya kila namna ya mwili."—Matendo 2: 1-4, 17.

▸ Sura ya 4, fu. 12; Sura ya 15, fu. 17

15 MSALABA

Kwa nini Wakristo wa kweli hawatumii msalaba katika ibada?

(1) Msalaba umetumiwa na dini za uwongo kwa muda mrefu. Nyakati za kale msalaba ulitumiwa katika ibada ya viumbe na desturi za kipagani za ngono. Mwanzoni, Wakristo hawakutumia msalaba katika ibada zao hata miaka 300 baada ya kifo cha Yesu. Miaka mingi baadaye, Konstantino Maliki Mroma alianzisha matumizi ya msalaba kuwa alama ya Ukristo. Alifanya hivyo ili kujaribu kuufanya Ukristo uwe maarufu. Hata hivyo, msalaba hauna uhusiano wowote na Yesu Kristo. Kitabu *New Catholic Encyclopedia* kinasema hivi: "Msalaba ulitumiwa na watu walioishi kabla ya enzi za Ukristo na wale ambao hawakuwa Wakristo."

(2) Yesu hakufa msalabani. Neno la Kigiriki ambalo

limetafsiriwa "msalaba" kihalisi linamaanisha "nguzo," "ubao," au "mti ulionyooka." *The Companion Bible* inaeleza hivi: "Katika Maandiko ya Kigiriki [Agano Jipya] hakuna mahali panapotaja vipande viwili vya mbao." Yesu alikufa kwenye mti ulionyooka.

(3) Yehova hataki tutumie sanamu au mifano katika ibada.—Kutoka 20:4, 5; 1 Wakorintho 10:14.

▸ Sura ya 5, fu. 12

16 UKUMBUSHO

Yesu aliwaamuru wanafunzi wake wafanye Ukumbusho wa kifo chake. Wanafanya hivyo Nisani 14 kila mwaka, tarehe inayolingana na siku ambayo Waisraeli walisherehekea Pasaka. Mkate na divai, vinavyowakilisha mwili na damu ya Yesu hupitishwa kwa kila mtu wakati wa Ukumbusho. Wale watakaotawala na Yesu mbinguni hula mkate na kunywa divai. Wale walio na tumaini la kuishi milele duniani wanahudhuria Ukumbusho wakiwa watazamaji wenye heshima lakini hawali mkate au kunywa divai.

▸ Sura ya 5, fu. 21

17 NAFSI

Katika *Biblia Takatifu—Tafsiri ya Ulimwengu Mpya,* neno "nafsi" humaanisha (1) mtu, (2) mnyama, au (3) uhai wa mtu au mnyama. Ifuatayo ni mifano michache:

Mtu. "Katika siku za Noa, . . watu wachache, yaani, nafsi nane, walichukuliwa salama kupitia maji." (1 Petro 3:20) Hapa neno "nafsi" linamaanisha watu, yaani, Noa na mke wake, watoto wake watatu na wake zao.

Mnyama. "Mungu akaendelea kusema: 'Maji na yajawe na nafsi hai na viumbe vinavyoruka viruke juu ya dunia kwenye uso wa anga la mbingu.' Kisha akasema: 'Dunia na itokeze nafsi zilizo hai kulingana na aina zake, mnyama wa

kufugwa na mnyama anayetambaa na mnyama-mwitu wa dunia kulingana na aina yake.' Ikawa hivyo."—Mwanzo 1: 20, 24.

Uhai wa mtu au mnyama. Yehova alimwambia hivi Musa: "Watu wote waliokuwa wakiiwinda nafsi yako wamekufa." (Kutoka 4:19) Yesu alipokuwa duniani, alisema hivi: "Mimi ndiye mchungaji mwema; mchungaji mwema huitoa nafsi yake kwa ajili ya kondoo."—Yohana 10:11.

Kwa kuongezea, mtu anapofanya jambo fulani kwa "nafsi yote" hilo linamaanisha kwamba anafanya kwa hiari na kwa nguvu zake zote. (Mathayo 22:37; Kumbukumbu la Torati 6:5) Neno "nafsi" pia linaweza kutumiwa kuelezea tamaa au hamu ya kiumbe hai. Mtu aliyekufa au kiumbe aliyekufa anaweza kumaanisha nafsi iliyokufa.—Hesabu 6:6; Methali 23:2; Isaya 56:11; Hagai 2:13.

▸ Sura ya 6, fu. 5; Sura ya 15, fu. 17

18 ROHO

Maneno ya Kiebrania na Kigiriki yanayotafsiriwa "roho" katika *Biblia Takatifu—Tafsiri ya Ulimwengu Mpya* yanaweza kumaanisha vitu mbalimbali. Hata hivyo, mara nyingi yanamaanisha kitu kisichoonekana kwa macho ya wanadamu, kama vile upepo au pumzi ya wanadamu au wanyama. Pia, maneno hayo yanaweza kumaanisha viumbe wa kiroho na roho takatifu, ambayo ni nguvu ya utendaji ya Mungu. Biblia haifundishi kwamba sehemu fulani ya mtu huendelea kuishi baada ya kufa.—Kutoka 35:21; Zaburi 104:29; Mathayo 12:43; Luka 11:13.

▸ Sura ya 6, fu. 5; Sura ya 15, fu. 17

19 GEHENA

Gehena ni jina la bonde lililokuwa karibu na Yerusalemu ambapo takataka zilichomwa na kuharibiwa. Hakuna ushahidi unaoonyesha kwamba wakati wa Yesu, wanyama

au watu waliteswa au kuchomwa wakiwa hai katika bonde hilo. Hivyo, Gehena haimaanishi mahali pasipoonekana ambapo watu waliokufa wanateswa au kuchomwa kwa moto milele. Yesu alipozungumzia wale wanaotupwa katika Gehena, alikuwa akimaanisha kuharibiwa kabisa. —Mathayo 5:22; 10:28.

▸ Sura ya 7, fu. 20

20 SALA YA BWANA

Ni sala ambayo Yesu alitoa alipokuwa akiwafundisha wanafunzi wake jinsi ya kusali. Pia, inaitwa sala ya Baba Yetu au sala ya kielelezo. Kwa mfano, Yesu alitufundisha tusali hivi:

“Jina lako na litakaswe”

Tunasali Yehova alitakase jina lake kutokana na uwongo wote unaosemwa dhidi yake. Hilo linamaanisha kwamba kila mtu mbinguni na duniani aliheshimu na kulitukuza jina la Mungu.

“Ufalme wako na uje”

Tunasali serikali ya Mungu iharibu ulimwengu mwovu wa Shetani, itawale dunia, na kuifanya kuwa paradiso.

“Mapenzi yako na yatendeke duniani”

Tunasali kusudi la Mungu kwa dunia litimizwe ili wanadamu watiifu, na walio wakamilifu waweze kuishi milele katika paradiso kama Yehova alivyokusudia alipowaumba wanadamu.

▸ Sura ya 8, fu. 2

21 FIDIA

Yehova aliandaa fidia ili kuwakomboa wanadamu kutokana na dhambi na kifo. Fidia ni bei iliyohitajiwa kulipia uhai mkamilifu wa mwanadamu ambao mwanadamu wa kwanza, Adamu alipoteza, na kurudisha uhusiano ulioharibika kati ya Yehova na wanadamu.

Mungu alimtuma Yesu duniani ili afe kwa ajili ya wanadamu wote wenye dhambi. Kwa sababu ya kifo cha Yesu, wanadamu wote wana nafasi ya kuishi milele na kuwa wakamilifu.

▸ Sura ya 8, fu. 21; Sura ya 9, fu. 13

22 KWA NINI MWAKA 1914 NI MUHIMU SANA?

Unabii wa Danieli sura ya 4 unatufundisha kwamba Mungu angeusimamisha Ufalme wake mwaka wa 1914.

Unabii: Yehova alimwotesha Mfalme Nebukadneza ndoto ya kiunabii iliyohusu mti mkubwa uliokatwa. Katika ndoto hiyo, kisiki cha mti huo kilifungwa kwa pingu ya chuma na shaba ili kisikue kwa kipindi cha "nyakati saba." Baada ya hapo mti huo ungeanza kuchipua tena.—Danieli 4:1, 10-16.

Unabii huo unamaanisha nini?: Mti unawakilisha utawala wa Mungu. Kwa miaka mingi, Yehova alitumia wafalme walioishi Yerusalemu kutawala taifa la Israeli. (1 Mambo ya Nyakati 29:23) Hata hivyo, wafalme hao hawakuwa waaminifu na utawala wao ukakoma. Yerusalemu liliharibiwa mwaka 607 K.W.K. Huo ukawa mwanzo wa zile "nyakati saba." (2 Wafalme 25:1, 8-10; Ezekieli 21:25-27) Yesu aliposema: "Yerusalemu litakanyagwa-kanyagwa na mataifa, mpaka nyakati zilizowekwa za mataifa zitimie," alikuwa akimaanisha zile "nyakati saba." (Luka 21:24) Hivyo, zile "nyakati saba" hazikuisha Yesu alipokuwa duniani. Yehova aliahidi kumsimamisha Mfalme mwishoni mwa zile "nyakati saba." Utawala wa Mfalme huyo mpya, Yesu, ungewaletea baraka nyingi za milele watu wa Mungu duniani.—Luka 1:30-33.

Urefu wa zile"nyakati saba": Zile "nyakati saba" zilikuwa na urefu wa miaka 2,520. Tukihesabu miaka 2,520 kuanzia mwaka 607 K.W.K., tunafikia mwaka wa 1914. Mwaka huo, Yehova alimweka Yesu, ambaye ni Masihi, kuwa Mfalme wa Ufalme wa Mungu mbinguni.

NDOTO YA MTI YA NEBUKADNEZA
INATUFUNDISHA NINI KUHUSU UFALME WA MUNGU?

UNABII

Mti mkubwa
(Danieli 4:10, 11)



"Ukateni mti uanguke"
(Danieli 4:14)



Utawala | **Mwisho wa utawala**

UNABII HUO UNAMAANISHA NINI?

Wafalme wa Israeli waliotawala watu wa Mungu



Yerusalemu lilipoharibiwa, utawala wa wafalme Waisraeli ulifikia mwisho

Oktoba
607 K.W.K.



"Na nyakati saba zipite"
(Danieli 4:16)



"Ufalme wako utakuwa hakika kwako"
(Danieli 4:26)



"Nyakati saba"


Utawala warudishwa

Miaka 2,520

Yesu aanza kutawala mbinguni akiwa Mfalme wa Ufalme wa Mungu

K.W.K.	W.K.
Miaka 606 1/4	**Miaka 1,913 3/4**

Oktoba 1914 W.K.



"Yerusalemu litakanyagwa-kanyagwa . . . mpaka *nyakati zilizowekwa* za mataifa zitimie"
(Luka 21:24)

Tunapataje miaka 2,520? Biblia inasema kwamba nyakati tatu na nusu ni sawa na siku 1,260. (Ufunuo 12:6, 14) Hivyo zile "nyakati saba" ni siku 2,520. Siku 2,520 ni sawa na miaka 2,520 kwa sababu ya ile kanuni ya kinabii ya "siku moja kwa mwaka mmoja."—Hesabu 14:34; Ezekieli 4:6.

▸ Sura ya 8, fu. 23

23 MIKAELI YULE MALAIKA MKUU

Neno "malaika mkuu" linamaanisha "mkuu wa malaika." Biblia inataja malaika mmoja tu kuwa mkuu na jina lake ni Mikaeli.—Danieli 12:1; Yuda 9.

Mikaeli ni kiongozi wa jeshi la Mungu la malaika waaminifu. Ufunuo 12:7 inasema: "Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka mkubwa, . . . na malaika zake." Kitabu cha Ufunuo kinasema kwamba Kiongozi wa jeshi la Mungu ni Yesu, hivyo, Mikaeli ni jina lingine la Yesu.—Ufunuo 19:14-16.

▸ Sura ya 9, fu. 4

24 SIKU ZA MWISHO

Maneno hayo yanamaanisha kipindi cha wakati ambapo kutakuwa na matukio makubwa duniani kabla Ufalme wa Mungu kuharibu ulimwengu wa Shetani. Maneno mengine kama vile "umalizio wa mfumo wa mambo" na "kuwapo kwa Mwana wa binadamu," yanatumiwa katika unabii wa Biblia kumaanisha kipindi hichohicho. (Mathayo 24:3, 27, 37) "Siku za mwisho" zilianza mwaka 1914 Ufalme wa Mungu ulipoanza kutawala mbinguni na zitaisha ulimwengu wa Shetani utakapoharibiwa katika Har–Magedoni.—2 Timotheo 3:1; 2 Petro 3:3.

▸ Sura ya 9, fu. 5

25 UFUFUO

Kitendo cha Mungu kumrudishia uhai mtu aliyekufa huitwa ufufuo. Matukio tisa ya ufufuo yanatajwa katika Biblia. Eliya, Elisha, Yesu, Petro, na Paulo waliwafufua watu. Miujiza hiyo iliwezekana kwa sababu ya nguvu za Mungu. Mungu ameahidi kwamba atawafufua "waadilifu na wasio waadilifu" ili waishi duniani. (Matendo 24:15) Biblia inataja pia, ufufuo wa wale watakaoenda mbinguni. Ufufuo huo hufanywa wakati wale waliochaguliwa au waliotiwa mafuta na Mungu wanapofufuliwa wakaishi na Yesu mbinguni. —Yohana 5:28, 29; 11:25; Wafilipi 3:11; Ufunuo 20:5, 6.

▸ Sura ya 9, fu. 13

26 KUWASILIANA NA PEPO

Kuwasiliana na mashetani au roho kwa njia ya moja kwa moja au kupitia mtu mwingine kama vile mchawi, au mwaguzi. Watu wanaowasiliana na pepo, wanafanya hivyo kwa sababu wanaamini mafundisho ya uwongo kwamba roho za wanadamu zinaendelea kuishi baada ya mtu kufa na zinakuwa mizimu. Roho waovu pia huwashawishi watu wasimtii Mungu. Unajimu, uaguzi, uchawi, na ulozi ni kuwasiliana na pepo. Vitabu vingi, magazeti, kusoma nyota, sinema, mabango, na nyimbo hufanya kuwasiliana na pepo kuwe kama njia ya kujifurahisha na isiyo na madhara. Desturi nyingi za mazishi, kama vile dhabihu kwa ajili ya wafu, sherehe za mazishi, siku za maombezi ya wafu, siku za kuwatakasa wajane, na mikesha ya mazishi inahusisha pia kuwasiliana na pepo. Mara nyingi watu hutumia dawa za kishirikina ili kupata nguvu za pepo.—Wagalatia 5:20; Ufunuo 21:8.

▸ Sura ya 10, fu. 10; Sura ya 16, fu. 4

27 ENZI KUU YA YEHOVA

Yehova ni Mungu Mweza-Yote, na ndiye Muumba wa ulimwengu wote mzima. (Ufunuo 15:3) Kwa hiyo, vitu vyote ni mali yake, naye ndiye Mwenye-Enzi kuu na ana mamlaka kamili ya kutawala uumbaji wake wote. (Zaburi 24:1; Isaya 40:21-23; Ufunuo 4:11) Ameweka sheria kwa kila kitu alichoumba. Yehova pia ana mamlaka ya kuwaweka wengine wawe watawala. Tunaunga mkono enzi kuu ya Mungu kwa kumpenda na kumtii.—1 Mambo ya Nyakati 29:11.

▸ Sura ya 11, fu. 10

28 KUTOA MIMBA

Kutoa mimba ni kusababisha kimakusudi kifo cha kitoto ambacho hakijazaliwa. Hakusababishwi na tukio lisilotazamiwa au hali fulani ya asili katika mwili wa binadamu. Mimba inapotungwa, kitoto hakiwi sehemu ya mwili wa mama, bali ni mtu tofauti.

▸ Sura ya 13, fu. 5

29 KUTIWA DAMU MISHIPANI

Ni njia ya matibabu ambayo mtu hutiwa damu yenyewe mishipani au zile sehemu kuu nne za damu kutoka kwa mtu mwingine au damu iliyohifadhiwa. Sehemu hizo kuu nne za damu ni utegili, chembe nyekundu, chembe nyeupe, na chembe sahani.

▸ Sura ya 13, fu. 13

30 NIDHAMU

Katika Biblia, neno "nidhamu" halimaanishi tu kuadhibu. Kutiwa nidhamu ni kufundishwa, kuelimishwa, na kurekebishwa. Yehova si mkatili wala hawatendei kwa jeuri wale anaowatia nidhamu. (Methali 4:1, 2) Yehova ni mfano mzuri kwa wazazi. Nidhamu anayotoa inakuwa na matokeo mazuri hivi kwamba wale wanaoipata wanafurahia. (Methali 12:1) Yehova anawapenda watu wake, na anawazoeza. Anawapa mwongozo ambao unawasaidia kurekebisha mawazo yao mabaya na kujifunza kufikiri na kutenda kwa njia inayompendeza. Nidhamu ya wazazi inahusisha kuwasaidia watoto wao waelewe umuhimu wa kutii. Pia, inahusisha kuwafundisha kumpenda Yehova, kupenda Neno lake Biblia, na kuelewa kanuni zake.

▸ Sura ya 14, fu. 13

31 ROHO WAOVU

Ni viumbe waovu wasioonekana, wenye nguvu zisizo za kawaida. Roho waovu ni malaika waasi. Waliasi walipokataa kumtii Mungu, na hivyo wakawa adui zake. (Mwanzo 6:2; Yuda 6) Waliungana na Shetani kumwasi Yehova.—Kumbukumbu la Torati 32:17; Luka 8:30; Matendo 16:16; Yakobo 2:19.

▸ Sura ya 16, fu. 4

Ili upate habari zaidi, tembelea Tovuti ya **www.jw.org /sw** au wasiliana na Mashahidi wa Yehova.